# Nipashe

Jumanne Septemba 3, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580013

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




## Mrithi wa Tundu Lissu kuapishwa, mahakama yapiga kalenda uamuzi

UKURASA 2




UKURASA 13

# Adaiwa kukwepa kodi kontena 700

• **Ni** kiongozi mkubwa serikalini, amwangukia Rais amsamehe... *Ukurasa 2*



Rais John Magufuli akiwasikiliza watendaji wa kata katika mkutano na watendaji hao, wa kata zote za mikoa ya Tanzania Bara, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu Mkuu Ikulu, Dk. Moses Kusiluka. **PICHA: IKULU**

## Bei ya mahindi sasa ni tishio

UKURASA 4

## Magufuli awapa 'meno' watendaji wa kata

UKURASA 3


TAIFA STARS VS BURUNDI

SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA




215393302

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akifungua Mkutano wa 50 wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola kwa Kanda ya Afrika, katika ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahar Mbweni nje kidogo ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**.

# Kigogo adaiwa kukwepa kodi kontena 700

**Na Romana Mallya**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, amedai kuwapo kwa kiongozi mmoja mkubwa nchini anayedaiwa kuingiza mzigo wa kontena 700 bandarini.

Alidai kuwa kiongozi huyo alitaka kukwepa kodi ya kontena hizo kwa kutaka huruma ya Rais John Magufuli.

Polepole alitoa madai hayo mwishoni mwa wiki katika kongamano la umuhimu wa amani na mapambano dhidi ya rushwa kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, mwakani.

Kongamano hilo liliandaliwa na Jumuiya Waislamu wa Shia Tanzania na kuhudhuriwa na viongozi wa vyama vya siasa tawala na upinzani, viongozi wa dini na wadau mbalimbali.

Akifafanua kuhusu kiongozi huyo, Polepole alisema; "yupo kiongozi mmoja mkubwa sana Tanzania sitamsema hata Takukuru wanamfahamu, ila mniwie radhi sitamtaja jina, alikuwa na kontena 700 bandarini amekwepa kodi.

"Kila kontena moja lilikuwa na futi 40, huyu kiongozi alitaka Rais amsaidie, lakini Rais Magufuli alimwambia lipa kodi uende zako. Huyu kiongozi mpaka sasa amenuna," alidai.

"Hivi ninavyoongea mpaka sasa amenuna. Rais Magufuli kazi yake ni kushughulika na watu walionuna. Siku zote ukisimamia haki hupendwi. Mtume alisimamia haki hakupendwa, Yesu alisimamia haki Wayahudi wakamuua, Ayubu alisimamia haki akapoteza kila kitu hadi familia yake."

Alidai kuwa hakuna mtu anayesimamia haki na akaishi maisha ya starehe bali huishi kwa imani.

"Rais Magufuli anatekeleza miradi ya maendeleo, lakini wapo ambao bado wanasimama wanasema hafanyi kitu, amenunua ndege wapo waliobeza, ujenzi wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme, wapo waliopinga kwa kusema uharibifu wa mazingira."

"Rais Magufuli ndiye pekee ambaye ameweza kutumia fedha za ndani na huu ndio ugomvi mkubwa uliopo na wao, miradi ya kimkakati inayotekelezwa ni kwa fedha za walipa kodi."

Alisema tangu mwaka 1961 hadi awamu

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
30/08/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe 04/09/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEARS CONSTRUCTION & INVESTMENT** itasafirisha mizigo kutoka **INYONGA** kuelekea **DAR ES SALAAM** kupitia **TABORA-DODOMA** Magari yenye namba za usajili: **T389 BES/T 668 BCJ.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** – **mita 16**
   **Upana** – **mita 2.8**
   **Kimo** – **mita 4.8**

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM** hadi **INYONGA** kupitia TABORAgari litasafiri muda wa mchana tu.***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115399702


# Mikopo elimu ya juu kutikisa Bunge

**Na Agusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa 16 wa Bunge la 11 unaanza leo jijini Dodoma, huku madai ya uonevu katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, yakitarajiwa kuutikisa mkutano huo.

Mwezi uliopita, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia kwa msemaji wake katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Susan Lyimo, iliiambia Nipashe kuwa itawasilisha bungeni mwezi huu hoja mahsusi kuhusu kile ilichokiita uonevu katika marejesho ya mikopo hiyo.

Masharti yanayolalamikiwa katika urejeshaji wa mikopo hiyo inayotolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ni pamoja na mikopo kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka, hivyo wanufaika kushindwa kumaliza kulipa madeni yao.

Wanufaika wa mikopo hiyo pia wanalalamika kuhusu kuongezwa kwa kiwango cha makato ya mshahara kulipa deni hilo kutoka asilimia nane iliyokuwapo kabla ya Novemba 2016 hadi asilimia

INAENDELEA UK. 8

# Mrithi wa Tundu Lissu kuapishwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, jana ilishindwa kutoa zuio la muda la kuapishwa kwa Mbunge Mteule wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, baada ya kuahirisha kutoa uamuzi wa kusikiliza kesi ya msingi au la hadi Septemba 9, mwaka huu.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote na kumaliza kazi yake saa 3:00 usiku, Jaji Sirilius Matupa, anayesikiliza kesi hiyo, alisema mahakama inahofia kuharibu maombi ya msingi kwa kutoa zuio hilo.

"Mahakama yangu inahofia kuharibu kesi ya msingi kwa kuwa hata uchaguzi unapofanyika na mbunge akaapishwa wakati kesi iko mahakamani, ikibainika kuwa si halali, mahakama inaamuru kuachia kiti cha ubunge na kiapo chake," alisema Jaji Matupa.

Katika kesi hiyo, Lissu kupitia mawakili wake, aliiomba Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Dar es Salaam kutoa kibali cha kusikiliza maombi yake ya kuvuliwa ubunge pamoja na kitoa zuio la muda la kuapishwa mbunge mteule Miraji Mtaturu.

Lissu aliiomba mahakama kutoa zuio la muda kwa mlalamikiwa wa kwanza Spika wa Jamhuri ya Muungano, Job Ndugai, kusitisha tukio la kumwapisha Mtaturu katika mkutano wa bunge unaoanza leo mjini Dodoma.

Hoja hizo ziliwasilishwa jana na Wakili wa Lissu, Peter Kibatala, katika mahakama hiyo. Mbali na Spika Ndugai, mlalamikiwa mwingine ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa hati ya maombi hayo, mlalamikaji anaomba mahakama kusitishwa uamuzi uliofanywa na Spika, kuufanyia uchunguzi na kukiwasilisha.

Kibatala alidai kuwa sababu kubwa ya kuomba kibali ni kutokana na kazi ya mahakama kupitia nyaraka kama zinafaa kusikilizwa kama mlalamikaji anavyoomba.

"Katika kipindi cha miaka saba iliyopita, Lissu alikuwa anafanya kazi zake za uwakili wa wananchi vyema lakini alishambuliwa kwa risasi na kutibiwa jijini Nairobi, nchini Kenya na baadaye akahamishiwa Ubelgiji," alidai.

Akifafanua zaidi, alidai kuwa Lissu hakuwahi kupewa taarifa za kutenguliwa ubunge wake bali amesikia barabarani.

Mbali na kutenguliwa ubunge wake, Lissu pia anaomba mahakama hiyo kutoa zuio la muda kwa kumtaka Spika Ndugai kusitisha kumwapisha Mbunge mteule, Miraji Mtaturu, mpaka maombi ya msingi yatakaposikilizwa.

Alidai kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano linatarajia kuanza mkutano wake leo, hivyo mlalamikaji anaomba mlalamikiwa wa kwanza kusitisha kumwapisha mteule huyo.

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Ajali zaua 700 kwa miezi saba

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZAIDI ya watu 700 wameripotiwa kupoteza maisha kutokana na ajali za barabarani zilizotokea kati ya Januari hadi Julai mwaka huu.

Imeelezwa kuwa watu 1,529 walijeruhiwa, hali ambayo imesababisha taifa kupoteza rasilimali watu ambao ni tegemeo kubwa katika uzalishaji mali kuelekea uchumi wa kati wa viwanda.

Takwimu hizo zilitolewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya siku ya mabalozi wa usalama barabarani yaliyofanyika Jijini Mwanza, ikiwa ni kuhakikisha ajali barabani zinapungua.

"Ajali nyingi za barabarani zinasababishwa na vitu na mwendokasi, matumizi ya vilevi kama pombe na mihadarati, kutokuvaa kofia ngumu hasa kwa madereva wa bodaboda, kutokufunga mikanda, kutokuwa na mfumo maalumu wa siti za kuwalinda watoto na matumizi ya simu na vyombo vingine vya kiteknolojia kwa madereva," alisema Masauni.

Aliwataka watumiaji wa barabara husuan madereva wa vyombo vya moto kuwa makini wakati wa kuendesha vyombo hivyo kwa kuhakikisha wanazingatia sheria za usalama barabarani.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Muslim, alisema tangu serikali ya sasa ilipoingia madarakani, wamefanikiwa kupunguza ajali kwa zaidi ya asilimia 30, huku Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, akiwataka askari kutimiza majukumu yao pasipo kumuonea mtu yeyote.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Philis Nyimbi ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, alisema mkoa huo unaendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mwenyekiti wa Taifa wa Taasisi ya Mabalozi wa Usalama Barabarani, John Seka, alisema kwa kushirikiana na asasi nyingine za kiraia wataendelea kusimamia mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 ili kupunguza ajali za barabarani hadi kufikia asilimia 60.

Takwimu za ajali nchini zinaonyesha kati ya mwaka 2016 hadi Julai 2019 kumetokea jumla ya ajali 20,683 zilizosababisha vifo 8,399 na majeruhi 19,722, kiwango ambacho ni kikubwa ambapo taifa limepoteza nguvu kazi, fedha na vifaa.



Mafundi ujenzi wa Kampuni ya Kichina ya Stecol Corporation, wakiendelea na kazi kuandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kitega uchumi la Jiji la Dodoma litakalokuwa na ghorofa zaidi ya 10 katika eneo la Uhindini jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# JPM awapa 'meno' watendaji kata nchini

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amewataka watendaji wa kata nchini kutomwogopa mtu yeyote wakati wakitimiza majukumu yao na kwamba wao ni wawakilishi wake kwenye ngazi ya kata.

Amewaambia wao ndio chanzo cha maendeleo ya nchi, hivyo wanapaswa kutembea kifua mbele wakati wote.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, alipokutana na watendaji wa kata zote Tanzania Bara, ikiwa ni mwendelezo wake wa kukutana na watendaji wa serikali.

Alisema watendaji hao wasisite kutoa taarifa pindi wanapoona kiongozi wa serikali anakwenda kinyume au kufanya matendo ambayo ni kinyume cha utawala bora.

"Ninyi ni wasimamizi wa watumishi wa umma kwenye kata. Kama kwenye kata yako kuna Mkuu wa Mkoa, Waziri au Mkuu wa Wilaya usiogope kumwandikia taarifa kama anakwenda kinyume cha maadili ya kazi zake. Na ukimwona mkubwa sana nitumie nakala na mimi," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Cheo cha mtendaji wa kata si kidogo, ni kikubwa mno. Ninyi ni wawakilishi wangu ngazi ya kata. Tunapozungumza mafanikio ya serikali, ninyi ndio wasimamizi wa mwanzo katika mafanikio hayo. Kwa hiyo napenda kuwathibitishia ndugu zangu, tembeeni kifua mbele."

Rais Magufuli aliwataka watendaji wa kata kote nchini kuwaripoti viongozi wanaofanya vurugu katika kata zao ikiwamo wale wanaopigana kwenye baa.

"Utakuta kila siku kiongozi anapigana baa hadi anasababisha baa kufungwa na hiyo baa ipo katika kata yako, eti kwa sababu ni mkubwa unaacha kutoa taarifa, charaza kalamu ndiyo maana watendaji kata wana kalamu na saini zao," alisema.

Pia aliwataka watendaji kutokubali kudharaulika katika maeneo yao na kuwaeleza kuwa wanaoamua nani aende Ikulu ni wao na wananchi.

"Hapa Ikulu wamekaa hadi Wajerumani. Amekaa (Julius) Nyerere, akaondoka, akaja (Ali Hassan) Mwinyi akaondoka. Amekuja (Benjamin) Mkapa akaondoka, amekuja mzee (Jakaya) Kikwete akaondoka na mimi nitakaa na kuondoka ndiyo maana sikusita kuwakaribisha," alisema.

Aidha, aliwaeleza maofisa hao kuwa cheo cha mtendaji wa kata ni kikubwa na kinaweza kuwafikisha ngazi za juu.

"Aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda alikuwa mtendaji wa kata na amefanya kazi kwa miaka mine, lakini amepanda mpaka kuwa waziri wa viwanda, kwa hiyo kazi yenu msiidharau," alisema na kuongeza:

"(George) Mkuchika (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora) amefanya kazi na kuwa kiongozi awamu zote tano, amefanya kwenye utawala wa Nyerere, akaja Mwinyi, kwa Mkapa yupo amekuja Kikwete yupo, nimekuja mimi yupo na atakayekuja

INAENDELEA UK. 8

SOMA GAZETI LAKO LA THE GUARDIAN NA NIPASHE POPOTE ULIPO KUPITIA

epaper.ippmedia.com

UTAPATA GAZETI LA THE GUARDIAN NA NIPASHE KWA URAHISI ZAIDI
UTAPATA HABARI MPYA KILA SIKU
UTAPATA TAARIFA ZA ZABUNI (TENDER) NA NAFASI ZA KAZI



Ingia kwenye GooglePlay au ios (Apple Store) kisha tafuta **The Guardian-IPP Media**

Google Play · App Store · The Guardian · Nipashe

# Bei mahindi Mwanza tishio kwa upatikanaji wa chakula

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

UGALI ni chakula kikuu cha wakazi wengi wa Kanda ya Ziwa. Inaelezwa kuwa si rahisi wakazi wa mikoa ya kanda hiyo kupitisha siku bila kupata chakula hicho.

Hata hivyo uchunguzi uliofanywa na Nipashe, umebaini kana hiyo, hasa Mkoa wa Mwanza uko hatarini kukumbwa na njaa kutokana na kupaa kwa bei ya mahindi ambayo ndiyo nafasi muhimu katika utengenezaji wa unga wa ugali.

Nipashe imebaini kuwa bei ya mahindi katika masoko mbalimbali yaliyoko Jiji la Mwanza inazidi kupaa kutokana na mkoa huo kutozalishwa kwa wingi zao hilo msimu huu.

Nipashe imebaini kuwa bei ya mahindi imepanda kutoka wastani wa Sh. 70,000 hadi kufikia Sh. 98,000 kwa gunia katika kipindi cha wiki mbili zilizopita.

Katika soko la Nyanguge lililoko Wilaya ya Magu, Nipashe wiki iliyopita ilishuhudia mahindi yakiuzwa kwa Sh. 85,000 kwa gunia la kilo 100, wakati wiki mbili zilizopita, katika soko hilo, gunia la aina hiyo lilikuwa linauzwa kwa Sh. 76,000.

Kwenye soko la Kisesa wilayani Magu bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 linauzwa Sh. 86,000 na kwa bei ya rejareja 'kitini' kimoja kinauzwa Sh. 3,500 (katika gunia moja la kilo 100 kunakuwa na 'vitini' 28, hivyo bei ya gunia moja ni Sh. 98,000).

Bei za aina hiyo pia zilishuhudiwa na Nipashe kwenye soko la Mecco lililoko Ilemela jijini. Katika soko kuu la Mwanza, mahindi yanauzwa kwa Sh. 83,000 kwa gunia.

Lidya Erro, mkazi wa Mtaa wa Ihangilo, Kata ya Nyakato wilayani Ilemela kupaa kwa bei ya mahindi kumesababisha familia yake kubadili ratiba ya mlo. Alisema wakati mwingine wanalazimika kula mara moja tu.

"Nilikuwa napika uji asubuhi, mchana napika ugali na jioni makande au ugali, baadhi ya siku tunakula wali jioni, lakini sasa hivi ugali napika jioni tu kutokana na mahindi kupanda bei, tumelazika asubuhi tukinywa chai au uji, chakula kingine tunakuja kupata usiku.

"Siku ya Nanenane nilinunua mahindi debe moja wakati ule kitini moja kilikuwa kinauzwa Sh. 2,500, leo hii nimekuja kununua mahindi hapa Mecco ili nisage, naambiwa kitini 3,500, siyo siri nilishtuka, niliishiwa nguvu ukizingatia na familia zetu hizi ukijitahidi kubadilisha mlo unapika makande badala ya ugali, kweli ni changamoto," Erro alisema.

Sungura Milimoduu, mkazi wa Mtaa wa Mabatini wilayani Nyamagana, alisema ongezeko hilo la bei ya mahindi halijaishia kuzifanya familia kupunguza idadi ya milo, bali limewakumba pia wateja wa migahawa.

"Sisi ambao tunakula kwa mamantile na migahawani, bado hawajapandisha bei lakini wamepunguza kiwango kwenye sahani. Aisee unapewa ugali kama ngumi, ukichukua mara moja, mara ya pili ugali umeisha hata haujashiba, inabidi uongeze mwingine. Sasa hapo ndio unapoona athari ya kuongezeka kwa bei ya mahindi," alisema.

Mahamud Hassan, mfanyabiashara wa mayai katika Soko Kuu la Mwanza, alisema kupanda kwa bei ya mahindi pia kumechochea kupanda kwa bei ya mayai.

"Soko la mahindi bei imepanda, hata hawa wanaotuuzia mayai wametupandishia bei kwa sababu bei ya mahindi imepanda, mahindi ni chakula cha kuku," alisema.

Hassan aliiomba serikali kuwaruhusu wafanyabiashara kutoka mikoa mingine kupeleka mahindi Mwanza na ipunguze kiwango cha ushuru kwa wafanyabiashara hao.

"Kwa maoni yangu, serikali iwaruhusu watu walete mahindi kutoka kila mkoa, kila mtu mwenye uwezo alete mahindi, auze ili tupate unafuu wa bei. Pia sehemu wanazochukua hayo mahindi ushuru ushuke kwa sababu wanapotozwa kiwango kikubwa, wakileta hapa napo walipe ushuru, lazima bei iwe kubwa kwa walaji wa mwisho ambao ni sisi wananchi," alisema.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga

## WAFANYABIASHARA WANENA

Shibo Robert, mfanyabiashara wa mahindi katika Soko la Nyanguge wilayani Magu, aliambia Nipashe wiki iliyopita kuwa alisema bei ya mahindi imepaa kutokana na uhitaji wa soko.

"Haya mahindi nimeyachukulia Bariadi, niliyanunua Mei mwaka huu, gunia lilikuwa Sh. 50,000 hadi 56,000 lakini sasa hivi ninayauza gunia moja Sh. 85,000," alisema.

Mfanyabiashara huyo aliishauri serikali kuweka bei elekezi katika nafaka kama ilivyofanya katika mazao mengine kama vile pamba na korosho ili kukabiliana na kasi ya ongezeko la bei.

"Hii biashara mara nyingi haina bei maalum, haina bei elekezi kama ilivyo kwa mazao mengine, wa kulaumiwa hapa ni serikali, haijaboresha mambo vizuri, ingelikuwa inapanga bei, ingelikuwa vizuri zaidi," alishauri.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Mwanza, Hamad Nchola, pia alikiri kupaa kwa bei mahindi, akieleza kuwa kumesababisha adha kwa watumiaji ambao wanalazimika kupunguza kiwango cha matumizi.

"Kama mtu alikuwa ananunua mahindi kilo tano, atanunua kilo nne au mbili, kama hali itaendelea hivi, nina uhakika kufikia Novemba, bei itapanda zaidi. Kama hatua za haraka hazitachukuliwa, hali itakuwa mbaya zaidi," alisema.

"Wito wangu sasa, kwanza kabisa wafanyabiashara wenzangu wasipandishe bei ya vyakula hivi, wauze bei kwa maslahi, lakini wasitake maslahi makubwa sana, tuuze mahindi kwa bei ya kutomuumiza mlaji, tusiwaumize wananchi.

"Pili, niishauri serikali hasa viongozi wa juu, wajitahidi kutembelea maeneo ya wanyabiashara kama masoko kama haya, kuna shida gani, nini kinahitajika ili wenyewe wapeane taarifa Mkoa wa Mwanza una shida ya chakula, walete chakula mikoani.

"Viongozi huwa kuna bajeti zao wanazopewa kwa ajili ya kutembelea maeneo kama haya, lakini Waziri wa Biashara hatujamwona huku, ni muhimu sana kujua wafanyabiashara wote kwenye masoko haya kuna nini."

## OFISA BIASHARA MWANZA

Alipotafutwa na Nipashe jijini Mwanza wiki iliyopita kuzungumzia tishio hilo la njaa, Ofisa Biashara Mkoa wa Mwanza, Yesaya Sikindene, alikiri kupaa kwa bei ya mahindi kwa kipindi cha wiki mbili zilizopita mkoani.

Alibainisha kuwa bei ya mahindi kwa gunia wastani wa Sh. 70,000 hadi 86,000, akieleza kuwa hali hiyo imechochewa nguvu ya soko na kufunguliwa kwa mipaka ya biashara kati ya Tanzania na nchi jirani.

Alisema kufunguliwa kwa mipaka hiyo kumewapa fursa wafanyabiashara kutafuta mahindi kwa udi na uvumba ili kunufaika na soko la nje.

"Awali, kulikuwa na soko kubwa la ndani na soko kidogo la nje, lakini siku za hivi karibuni, kumekuwapo na ongezeko la utoaji wa mazao ya nafaka kwenda nje ya nchi hususan nchi za Congo, Kenya, Rwanda na Sudan.

"Sasa, hicho kitu kimeongeza mahitaji makubwa ya soko na bei ya mahindi kwenye nchi hizo ni kubwa zaidi kuliko ndani ya nchi kiasi kwamba wafanyabiashara wengi sasa wanatafuta mahindi kwa udi na uvumba ili kuweza kunufaika na masoko yaliyoko nje ya nchi kuliko masoko ya ndani," alisema.

Sikindene alisema huduma zote ambazo ziko kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya nafaka ambazo zinatumia mahindi na mchele kama malighafi katika uzalishaji wa bidhaa zingine, nazo bei ziko hatarini kupaa.

"Hii ni nguvu ya soko, kwenye nguvu ya soko huwa hatuzungumzii kupanga bei, kikubwa hapa tunazungumzia nguvu ya soko kwa maana ya 'supply and demand'.

"Kile ambacho kinapelekwa sokoni na kile ambacho kinahitajika, wiki mbili au mwezi moja uliopita, bei ilikuwa hivyo kwa sababu wahitaji walikuwa wachache, lakini hata wewe leo hii ungepeleka bidhaa ambayo kila mmoja anaihitaji 'automatically' nguvu ya soko inakwambia ongeza bei. Kwa hiyo, hali hii inatokana na nguvu ya soko," alisema.

Sikindene pia alisema uzalishaji wa mazao ya nafaka hauna ruzuku kutoka serikalini tofauti na mazao mengine kama pamba ambayo serikali inatia nguvu kwa inatoa pembejeo.

"Yapo maeneo ndani ya hii nchi tunavyoongea sasa ndio wametoka kuvuna. Kwa hiyo, bei ya mahindi inaweza kubadilika kwa maana ya kushuka kutokana na haya mazingira, maeneo kama Ludewa miezi ya Julai na Agosti ndio wanaanza kuvuna," alisema.

## KAULI YA WIZARA

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipoulizwa na Nipashe kuhusu suala hilo jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, alisema, hali ya chakula nchini ni nzuri kutokana na uzalishaji wa mazao ya chakula kufikia tani milioni 16.489.

Kiwango hicho cha uzalishaji ni kikubwa kwa kuwa mahitaji ya nchi kwa mwaka ni tani milioni 13, hivyo nchi ina ziada kubwa ya chakula.

"Tathmini iliyofanyika hivi karibuni, inaonyesha uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani milioni 16.489 ukilinganisha na mahitaji ya tani milioni 13 yaliyopo," Hasunga alibainisha.

Akifafanua zaidi kuhusu uzalishaji huo, Hasunga alisema tani milioni 9.79 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 7.44 ni mazao yasiyokuwa ya nafaka.

Alisema kiwango hicho cha mavuno kimewezesha nchi kujitosheleza kwa mahitaji yake ya chakula kwa asilimia 119.

Alisema mikoa iliyofanya vizuri katika uzalishaji wa chakula ni Ruvuma ambayo msimu huu imezalisha chakula kwa asilimia 227, ukifuatwa na Rukwa uliozalisha kwa asilimia 220.

Alisema kuna mikoa minane ambayo haijafikia uzalishaji mzuri ikiongozwa na Dar es Salaam uliozalisha asilimia tatu pekee.

Hata hivyo, Hasunga aliweka wazi kuwa kuna halmashauri 44 ambazo zina upungufu wa chakula wa kati ya asilimia 90 na 99.

Kuhusu kupaa kwa bei ya mazao ya nafaka, Hasunga alisema wizara yake haihusiki na bei za mazao hayo, lakini akasisitiza Tanzania inacho chakula cha kutosha kwa sasa.

## HABARI KITAIFA

# Wananchi wahofia aliyeachiwa kesi ya unyang'anyi wa silaha

**Na Enock Charles**

WAKAZI watano wa Kata ya Mapinga wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, wamelalamikia kuachiliwa huru na Jeshi la Polisi mtu anayedaiwa kuwa mtuhumiwa wa unyang'anyi wa kutumia silaha .

Wananchi hao wamesema kwamba kitendo cha kumwachia mtuhumiwa wa kosa hilo ambalo halina dhamana kisheria, ni hatari kwa usalama wao.

Wakizungumza na gazeti hili wiki iliyopita, walibainisha kuwa mtuhumiwa huyo (jina tunalihifadhi kwa sasa), ambaye alikamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi wa jeshi hilo, aliachiliwa huru, hivyo kuwa tishio kwa usalama wao.

"Tunachoshangaa ni kwamba mmoja ya watuhumiwa hao ameachiliwa huru na sasa tuna wasiwasi na hali ya usalama wetu," alisema mmoja ya wakazi hao.

Kwa mujibu wa wakazi hao, mtuhumiwa huyo ameshafikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo kusomewa shtaka la jinai la unyang'anyi wa kutumia silaha pamoja na wenzake wengine watatu .

Gazeti hili lilionyeshwa picha za baadhi waathirika hao wa tukio linalodaiwa la unyang'anyi wa kutumia silaha ambao baadhi yao wanadaiwa kuendelea na matibabu katika Zahanati ya Kerege iliyopo katika Kata ya Kerege wilayani Bagamoyo.

Kwa mujibu wa wakazi hao, mtuhumiwa huyo ameachiwa huru katika wakati ambapo upelelezi wa shauri lake ukiendelea, hivyo kuwapo hofu ya kuwatishia mashahidi katika kesi yake na kuvuruga upelelezi.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu madai hayo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliwataka wakazi hao kwenda kwake ili kupatiwa ufumbuzi wa tatizo lao kwa maelezo kuwa jeshi hilo lipo kwa ajili yao.

"Kama wamepata shida huko Bagamoyo waje kwangu mimi ndiye mkubwa wa hao walioko Bagamoyo," alisema kamanda Nyigesa na kuongeza:

"Usalama wao hauwezi kulindwa na vyombo vya habari, waambie waje."



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Dk. Agnes Kijazi (katikati), akifafanua jambo wakati wa warsha ya wanahabari kuhusu utabiri wa mvua za vuli, unaotarajiwa kutolewa leo. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa Mamlaka hiyo, Dk. Hamza Kabelwa, na Meneja wa Huduma za Utabiri, Samuel Mbuya. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**.

# Taharuki yaibuka basi la mwendokasi likiteketea

**Na Beatrice Moses**

TAHARUKI iliwakumba baadhi ya abiria wa mabasi ya mwendokasi, baada ya basi moja kuwaka moto na kuteketea wakati likiingia kwenye kituo cha Kimara jijini Dar es Salaam.

Tukio hilo limetokea juzi usiku, licha ya dereva wa basi hilo kufanikiwa kuwanusuru abiria na yeye mwenyewe, abiria waliokuwa kwenye mabasi mengine walitawaliwa na hofu kuwa miali ya moto huo kuwa unaweza kulipua magari mengine.

Baadhi ya abiria walitamani kuruka kupitia kwenye madirisha ili kunusuru maisha yao, baada ya kuona madereva wanajishauri kuhusu kufungua milango ili washuke kwa kuwa hapakuwa mahali sahihi na salama kushusha.

Kamanda wa Kikosi za Zimamoto na Uokoaji Kinondoni, Jenifer Shirima, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo akibainisha kuwa ni jambo la kushukuru kuwa hakuna binadamu aliyejeruhiwa ama kusababishiwa kifo na moto huo.

"Tulipokea taarifa ya kuzuka kwa moto huo saa 2:03. Mtambo wetu uliwasili eneo la tukio saa 2:15 ukiwa na maji lita 8,000 na kufanikiwa kuzima moto huo," alisema Kamanda Shirima.

Alibainisha kuwa taarifa za awali zinabainisha kuwa chanzo cha moto huo kilikuwa ni uvujaji wa mafuta ambao ulibainika gari likiwa katika eneo la Baruti, dereva aliwahakikishia kuwa watafika salama Kimara.

"Msuguano unaosababisha joto unapokutana na petroli kwa kuwa ni hewa ina uwezo wa kusababisha moto kuwaka, ndicho kilichotokea lilipokaribia kituoni basi lilianza kuwaka moto," alisema Kamanda Shirima.

Alisema uchunguzi zaidi unaendelea kufanywa kujiridhisha na chanzo cha moto huo kisha watatoa taarifa rasmi.

" Nawasihi wananchi wajitahidi kuhakikisha wanatoa taarifa haraka iwezekanavyo kwa kupiga namba 114 mara moto unapozuka, kisha ndipo waendelee na juhudi za kuzima, kwa tukio hilo tulifika kwa wakati kulingana na muda tuliopata taarifa," alisema.

Alisema basi hilo lilitoka mjini likiwa na abiria na lilipofika eneo la Kimara Mwisho walifanikiwa kushuka kabla halijateketea kwa moto.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na kukusanya taarifa zaidi za ajali hiyo, ikiwamo hasara iliyosababishwa na ajali hiyo.

Tukio hili si la kwanza kwa basi la Udart kuwaka moto kwani huko nyuma eneo la Ubungo Dar es Salaam liliwahi kutokea ila uliwahi kudhibitiwa.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# SUA inusuru upotevu huu

**SUALA** la njaa na ukosefu wa uhakika wa chakula ni tatizo linalowapasua vichwa watu wengi, lakini ni usumbufu kwa serikali.

Pamoja na kilimo cha Tanzania kwa kiasi kikubwa kutegemea mvua wakulima wanajitahidi kulima na wakati mwingine mazao mengi na kuifanya nchi kuwa na ziada ya chakula.

Hata hivyo, habari njema hizo, zinakwazwa na upotevu wa chakula baada ya kuvuna na eneo linalotajwa kuwa limeathirika zaidi ni la nafaka.

Mazao yanayopotea kwa wingi baada ya kuvunwa kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga ni pamoja na mahindi, mchele na mtama.

Ndiye anayedokeza kuwa kiwango cha upotevu wa nafaka baada ya mavuno ni asilimia 40.

Pamoja na maelezo yake, kwa mujibu wa utafiti wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO), wakulima nchini hupoteza hadi asilimia 40 baada ya mavuno kutokana na changamoto kama mtaji mdogo, ujuzi mdogo wa ubebaji mazao na ukosefu wa masoko na sera bora.

Utafiti mwingine wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, unaeleza kuwa pamoja na ongezeko la uzalishaji katika ngazi ya kitaifa linalokadiriwa kufikia wastani wa tani milioni 9.4 kwa mwaka, teknolojia zinazotumika kabla, wakati na baada ya kuvuna husababisha upotevu wa wastani wa tani milioni 3.7 kwa mwaka sawa na asilimia 40.

Hata hivyo kuna tatizo jingine la mazao kuliwa na wanyama waharibifu yakiwa shambani, kwa mfano panya.

Si hao pekee, wakati mwingine kuna wadudu waharibifu kama dumuzi, vipepeo na bungua wanayoyaharibu, hata mchwa nao wamekuwa ni tatizo kubwa hasa kwenye mahindi.

Licha ya wakulima kupambana na changamoto hizo kwa miaka mingi, mvua kunyesha baada ya mazao kukomaa yakiwa shambani nalo ni tatizo linalochangia upotevu wa chakula. Wakulima wengi huumizwa na mvua zinazonyesha wakati mahindi yakishakauka.

Aidha, baada ya mpunga kukomaa pia mvua hunyesha yote hayo huibua matatizo kama nafaka kuota, kuoza, kushambuliwa na mchwa na pia kuvunda kutokana na kuvu wanaoibuka kutokana na unyevunyevu.

Pamoja na utafiti huo wa SUA umefika wakati wa chuo kufanya kila jitihada kuwasaidia wakulima kuokoa mazao yao.

Hii ni kwa sababu taasisi hiyo ya umma pamoja na kupewa jukumu la kufunza wataalamu wa kilimo, mifugo na sekta nzima ya kilimo na ufugaji, uvuvi haitalitendea haki taifa iwapo kiwango kikubwa hicho cha chakula kitaachwa kupotea bila kunusuriwa.

Pengine taasisi hiyo inaweza kujitetea kuwa haina fedha au bajeti ya kuzuia hasara hiyo, lakini wakati umefika kwa Chuo Kikuu cha Kilimo kuwa mwokozi kwenye janga hilo.

Ni vyema kama ilivyofanya utafiti na kuibua asilimia za upotevu, ikachunguza pia na kuanzisha programu na miradi ya kuwasaidia wakulima kulinda mazao baada ya mavuno.

Licha ya kutafiti na kuibua changamoto hizo wananchi wanaweza kuendelea kupata hasara kama hakutakuwa na msaada wa kudhibiti upotevu wakulima wataendelea kuumia.

Tungependa kuona SUA ikianzisha programu za jinsi ya kuhifadhi nafaka pengine ikihusisha kujenga vihenge vya muda kwani suala la utunzaji duni mazao husababisha kupoteza chakula kingi.

Aidha, chuo kiangalie namna ya kuwafunza wakulima namna bora za kuchakata mazao mara moja baada ya kuvuna kuzuia yasiharibikie mashambani.

Halikadhalika kuwasaidia kubuni mbinu bora za kuyasafirisha ili kuzuia upotevu wa chakula unaotokea sehemu mbalimbali ambao pengine kiasi uzalishaji unavyopanda nao unaongezeka pia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Uanzishwe mfuko maalumu ili kuokoa zao la pamba, mengine



Na Sabato Kasika

**DHAMIRA** ya serikali kuwakwamua wakulima na hasa wadogo wadogo ambao ndio wanaunda sehemu kubwa ya Watanzania kwa maana ya shughuli kuu ya kiuchumi, ni ya msingi katika dhana nzima ya kujenga ustawi wao.

Serikali imefanya mengi ikiwamo hatua ya kuyatangaza baadhi ya mazao kuwa ya kimkakati kama vile pamba, korosho, kahawa, tumbaku na chai ili kuboresha maslahi ya wakulima.

Na ndiyo maana kunashuhudiwa ongezeko katika uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini, ikiwa ni hatua stahiki kwenye mwelekeo wa kujenga utajirisho kwa wananchi.

Utajirisho ambao kwa mujibu wa Rais Yoweri Museveni alipomtembelea Rais John Magufuli, Chato Julai mwaka huu, unapaswa kuwa lengo namba moja la kila raia ili ajiletee maendeleo yake binafsi na hivyo taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, dhamira hiyo ya serikali ya kuona wakulima wananufaika na juhudi na uwekezaji wao katika kilimo inaonekana kukumbana na tatizo la soko la mazao yao.

Muungwana anachukua somo lililopatikana kwenye sakata la bei ya korosho na mazongezonge yake hadi pale serikali ilipoamua kununua korosho yote kama msingi wa anachokijadili.

Hiyo ni baada ya kampuni za ununuzi kugomea bei elekezi ya kuanzia Sh. 3000 kwa kilo iliyokuwa imewekwa na serikali, zikitaka kununua korosho kwa bei chini ya hiyo.

Aidha, kama haitoshi, kadhia hiyo imehamia pia kwenye zao la pamba ambako ununuzi wake kutoka kwa kampuni za ununuzi unasuasua hadi sasa pamoja na jitihada za serikali za kuhakikisha wakulima wanalipwa fedha zao.

Kwamba pamoja na msimu wa pamba kuzinduliwa tangu mwezi Mei, hadi sasa bado pamba imejaa kwenye baadhi ya Maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS), huku baadhi ya wakulima hasa katika Kanda ya Ziwa, wakiwa bado hawajalipwa fedha zao.

Na ndiyo maana kuna taarifa kwa mfano wiki iliyopita ya baadhi ya wakulima mkoani Shinyanga kufika kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, wakitaka kulipwa fedha zao, baada ya kuwa wameuza pamba yao.

Aidha, taarifa kutoka mkoani Simiyu, zinabainisha kwamba katika baadhi ya wilaya ikiwamo ya Maswa, kuna kama 'kamgomo' kutoka kwa wanunuzi wa zao hilo.

Kwamba wanataka kwanza waisafirishe pamba kutoka kwenye maghala ya AMCOS kwenda katika viwanda vyao, ndipo walete fedha kufuatana na kiasi cha kilo walichokisafirisha, kinyume na msimamo wa serikali.

Kwamba serikali inataka wakulima wakishauza pamba yao walipwe palepale na si kukopeshwa kama 'matajiri' wanavyotaka.

Matokeo yake mpaka sasa bado baadhi ya maghala ya AMCOS kwa mfano katika Wilaya ya Maswa yamejaa pamba, huku wakulima wakiwa bado hawajalipwa.

Hilo linafanyika mwezi Septemba tayari ukiwa umeshaingia, ambao kimsingi huwa ni wa kumalizia maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu ujao.

Kadhia hii si kwamba inaathiri mwenendo mzima wa maandalizi ya msimu ujao, lakini dhana nzima ya utajirisho kwa mwananchi binafsi kama alivyoibainisha Rais Museveni kwenye ziara yake Chato ya kutaka kila mwananchi ajiletee maendeleo yake binafsi.

Maendeleo yatakayosaidia kuanzisha miradi binafsi kama ya ujenzi wa nyumba, hoteli, kupanua mashamba, mifugo na hivyo kukuza ajira na ustawi wa taifa.

Wakati Muungwana akiwahimiza wakuu wa mikoa na wilaya na hasa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kutoa uongozi utakaohakikisha wakulima wanalipwa fedha zao, ana ushauri kwa serikali.

Kwamba wakati umefika sasa wa kuwa na mfuko maalumu utakaokuwa mkombozi kwa wakulima pale kampuni binafsi za ununuzi zinapoleta 'kamgomo' kama inavyoendelea sasa kwenye zao la pamba au ilivyotokea katika zao la korosho.

Anasema hilo ni la msingi kwa sababu kutokana na somo lililoletwa na kadhia za ununuzi wa mazao hao mawili, kutegemea wanunuzi binafsi kunakwamisha dhamira njema ya serikali ya kuwajengea utajirisho wakulima.

## BARUA/MJADALA

# *Hii kero Mikese hadi lini?*

**Ndugu Mhariri**

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese, mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/ kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je kwa majibu haya kuna amani hapa?*

*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*


*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

**Ahsante ni sisi wanakitongoji,**
**Ukomanga-Fulwe, Mikese.**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Elimu hii iwe na matokeo chanya Nachingwea




**Na Sabato Kasika**

KODI ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya mapato ya serikali, ambavyo huvitumia kwa ajili ya maendeleo ya nchi, kutokana na ukweli kwamba nchi yoyote duniani inapata maendeleo kupitia kodi.

Kutokana na umuhimu huo wa kodi, serikali imekuwa ikikusanya kodi kwa wananchi kupitia njia tofauti ikiwamo watu kulipa kupitia biashara au shughuli wanazofanya na kudai risiti wanaponunua bidhaa.

Jambo kubwa la kuzingatia ili kuwafanya watu kuwa na utamaduni wa kulipa kodi bila shurti, ni kupewa elimu ya mlipakodi, inayowafanya watambue kuwa wana wajibu wa kulipa kodi.

Hilo ndilo limekuwa likifanyika maeneo mbalimbali nchini baada ya kubainika kuwa baadhi ya wananchi hawajui umuhimu wa kulipa kodi na badala yake wamekuwa wakidai kupata huduma tu zikiwamo za afya.

Kwa muda mrefu sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeendelea kutoa semina na elimu ya mlipakodi kwa wafanyabiashara na kwa vikundi mbalimbali vikiwamo vya wakulima ili kuongeza uhiari katika ulipaji wa kodi.

Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi ni miongoni mwa maeneo, ambayo hivi karibuni TRA ilitoa elimu hiyo ili kusaidia wakazi na wananchi kuwa na mazoea ya kulipa kodi na tozo za serikali bila kusukumwa.

Jumamosi iliyopita, wilaya hiyo ilihitimisha kilele cha 'Wiki ya Mlipakodi na Tozo za Serikali,' huku wananchi wakiwa wamefikiwa na kupewa elimu hiyo muhimu kwa maendeleo ya taifa lao.

Hatua hiyo ya kutoa elimu ilifanyika baada ya utafiti uliofanywa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Rukia Muwango, ambao ulibaini kuwapo kwa changamoto za ulipaji kodi kwa wakazi wa Nachingwea.

"Niliibua wazo hili la elimu ya mlipakodi baada ya kubaini wananchi wengi hawana uelewa wa mambo ya kodi na tozo za serikali, na hawatambui kwamba wana wajibu wa kufanya hivyo," anasema Muwango.

Anaongeza: "Hawatambui kuwa wana wajibu wa kutoa kodi na tozo kulingana na mahitaji, matokeo yake wanadai haki ya kupata huduma za serikali, kulaumu miundombinu kukosekana bila kujua kwamba hayo yote yanatokana na kodi, ambazo zinalipwa na sisi wenyewe Watanzania."

Kutokana na hali hiyo, alishirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Mashujaa FM, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na kampuni za Hyseas na Sunshine kusaidia kuhamasisha wananchi kuhudhuria mikutano ya utoaji wa elimu hiyo.

Mjadala huu unaunga mkono juhudi za mkuu huyo wa wilaya za kuhamasisha wananchi kulipa kodi, hasa kwa kuzingatia kwamba bila kodi hakuna maendeleo, hivyo hatua hiyo iwabadilishe wakazi wa Nachingwea.

Kodi ni kwa maendeleo ya nchi, kila mtu ana wajibu wa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo, si kudai haki tu bali kuna kutimiza wajibu pia, ambao ni kulipa kodi, vinginevyo ni kukwamisha maendeleo ya nchi.

Mkuu wa wilaya anasema si muda wa kunyosheana vidole, kulaumiana bali yeye na timu yake wanaendelea kuelimisha umma wa wakazi wa Nachingwea utambue kuwa kulipa kodi ni haki yao na waone fahari.

Kwa kuwa anasema utoaji wa elimu utakuwa endelevu kadri watakavyojipanga na timu yake, ni vyema kila mmoja kuhakikisha anaipata ili anapofanya biashara akumbuke kulipa kodi na tozo mbalimbali za serikali.

Nachingwea ni miongoni wa wilaya za Lindi, ambazo wananchi wake wanajishughulisha na kilimo cha korosho na ufuta ambavyo ni mazao makuu ya biashara, hivyo elimu hiyo iwe na matokeo chanya kwao.

Mkuu wa wilaya amechukua hatua ya kuita TRA kwa kutambua kwamba imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara kwa wadau mbalimbali ili kuhakikisha kila mlipakodi anafahamu maana ya kodi na umuhimu wa kuilipa.

Wakulima nao ni walipakodi kwani wanaingiza kipato kupitia mazao yao, kwa maana hiyo kila mtu mwenye kipato anatakiwa kulipa kodi, ambayo ndio itakayoiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake kwa wananchi wake.

Moja ya mambo muhimu, ambayo Rais Dk. John Magufuli huwa anahimiza Watanzania kila mara, ni kujenga tabia ya kulipa kodi kwa vile ndio msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yoyote duniani.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



# Kigogo adaiwa kukwepa kodi kontena 700

INATOKA UK. 2

ya nne vituo vya afya ambavyo vilijengwa vilikuwa ni 115, lakini kwa miaka miwili kuanzia mwaka 2017 Rais Magufuli amefanikiwa kuvijenga vituo 350.

"Hospitali zilizojengwa kwa awamu zilizopita zilikuwa 77, lakini kuanzia mwaka 2018/19 Rais Magufuli amejenga hospitali 67, zimebaki 10. Wapo waliokuwa wanatamani kuona korosho zinakwama, leo zinasombwa Mtwara malori kwa malori," alisema.

Pia, alisema serikali ilimkamata jambazi mmoja akiwa amejificha kwenye moja ya makabati Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, akiwa anajiandaa kutoroka nchini.

"Amejificha kwenye makabati kwenye maduka pale uwanja wa ndege, cha ajabu hakuonekana kwenye kamera yoyote uwanjani hapo namna alivyoingia kwenye makabati hayo, alikuwa anasubiria tangazo la kuingia kwenye ndege aliyokuwa akisafiri nayo ili akishaingia tushindwe kumkamata, lakini intelijensia yetu ilimkamata na sasa hivi yupo Segerea," alidai.

"Naipongeza Shia kwa kuandaa kongamano hili ambalo limetukutanisha wanasiasa na viongozi wa dini ili tuzungumze, nawaomba makongamano kama haya muwe mnayaandaa kila mara," alisema.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Msafiri Mtemelwa, alipopewa nafasi ya kuzungumza alilalamika kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara na vikao vya ndani. Hata hivyo, akijibu hoja hiyo Polepole alisema siyo kweli kwamba vikao vya ndani vimezuiliwa na kutoa mfano wa majimbo mawili ya upinzani la Arusha na Mbeya Mjini ambako kote wanavifanya.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Ally Mfuru, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wake, alisema taasisi hiyo inajipanga vyema kuhakikisha wanafanya kampeni kuanzia chini ili kuwakumbusha wananchi kutojihusisha na rushwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuelekea Uchaguzi Mkuu, mwakani.

Mhadhiri katika chuo cha Swadiq chini ya kiongozi Mkuu Maulana Sh Hamed Jalala, Saidy Othman, aliiomba serikali ili kutengeneza fikra na mitazamo mipya somo la rushwa lifundishwe shuleni wanafunzi waanze kujua ubaya wake tangu wakiwa wadogo.

Alisema vitendo vya kubaka, dhuluma na kula rushwa vyote vinafanywa na binadamu bila kushirikisha akili.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Dk. Mohamed Ahmed, alisema, yeyote atakayejaribu au mwenye mawazo ya kusababisha matatizo hatakuwa na nafasi Tanzania.



Mawakili wa Serikali, Vicent Tangoh (katikati), akiwaongoza wenzake, Alicia Mbuya (kulia) na George Mandepo, katika kesi ya kutetea upande wa Jamhuri dhidi ya aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, kuvuliwa ubunge katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

## JPM awapa 'meno' watendaji kata nchini

INATOKA UK. 3

atamteua na hakuanzia ngazi ya uwaziri."

Rais Magufuli aliwaeleza maofisa hao kuwa wao ni wawakilishi wa serikali katika maeneo yao hivyo hawana budi kuisemea na kuitetea.

"Mnafahamu dira ya serikali pamoja na ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, mnafahamu jitihada mbalimbali zinazofanywa pamoja na miradi inayotekelezwa," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Rais Magufuli aliwaonya viongozi wakubwa wa serikali ambao wanawanyanyasa watendaji wa kata, pamoja na baadhi ya watendaji kata wanaowanyanyasa wananchi.

"Nitashangaa baada ya kikao hiki nisikie mkurugenzi au watendaji wa halmashauri wanakwenda kuwanyanyasa watendaji wa kata. Nitamwona hatoshi, wala mtendaji wa kata ambaye ananiwakilisha kwenye kata ile aende akawaonee wananchi wangu maskini waliokaa kwenye jua na mvua kunipigia kura nitamwona naye hatoshi," alisema.

# Mikopo elimu ya juu kutikisa Bunge

INATOKA UK. 2

15 baada ya Bunge kuridhia marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Mwaka 2004.

Vilevile, wanufaika wa mikopo hiyo wanalalamika deni kuongezeka kwa asilimia moja inayokatwa kwa ajili ya uendeshaji wa HESLB, wakieleza kuwa bodi hiyo inapewa ruzuku na serikali ili kuendesha shughuli zake na watumishi wake ni waajiriwa wa serikali.

Katika mahojiano na Nipashe mwezi uliopita jijini Dar es Salaam, Lyimo alisema kambi yao itautumia mkutano wa Bunge wa mwezi huu kulishauri Bunge na serikali kufanya marekebisho kwenye sheria iliyoanzisha HESLB ili kufuta makato aliyoyaita ya kinyonyaji yanayolalamikiwa na wanufaika wa mikopo hiyo.

Takwimu za HESLB zinaonyesha kati ya Watanzania 479,779 waliopewa mikopo hiyo, tangu serikali ianze kuitoa mwaka 1994, ni wanufaika 11,214 waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao, sawa na asilimia 2.3.

Sababu kubwa inayotajwa kuwakwamisha wanufaika wengi kumaliza kulipa madeni yao ni deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka.

Hata hivyo, Ofisi ya Bunge ilisema jana kuwa miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kuapishwa mrithi wa Tundu Lissu.

Kwa mujibu wa ratiba ndogo iliyotolewa jana, Bunge litaanza na kiapo cha uaminifu kwa Mbunge mteule wa Jimbo la Singida Mashariki, Miraji Mtaturu (CCM).

Pamoja na kiapo hicho, pia ratiba hiyo inaonyesha kutakuwa na azimio la kumpongeza Rais John Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kwa kuendesha vyema mkutano wa 39 wa jumuiya hiyo.

Baada ya azimio hilo, ratiba hiyo inaonyesha kutakuwa na kikao cha kamati ya uongozi ya bunge na kikao cha wabunge wote.

Juni 28, mwaka huu, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitangaza kumvua ubunge Lissu huku akitoa sababu mbili zilizofanya kufikiwa uamuzi huo ni kutoonekana bungeni bila Spika kuwa na taarifa ya maandishi na kutojaza fomu ya tamko la mali na madeni.

## Mrithi wa Tundu Lissu kuapishwa

INATOKA UK. 2

Kibatala aliongeza kudai kuwa bila kutoa zuio hilo, kazi ya mahakama itakuwa ngumu zaidi na hata mlalamikaji kusimamia haki yake itakuwa ngumu.

Alisisitiza kwamba mahakama kutoa zuio dhidi ya Spika si mara ya kwanza kwamba haitakiwi kushindwa kwa chombo chochote kile.

Mawakili wa walalamikiwa Mawakili wa Serikali Wakuu Vicent Tangoh, Lucas Malunde na Abubakar Mrisha, kwa nyakati tofauti walipinga mahakama kukubali ombi la Lissu kwa yana upungufu ya kisheria.

Tangoh alidai kuwa kiapo cha mlalamikaji hakina miguu ya kusimamia kwa sababu hakijaambatanishwa na nyaraka muhimu za kisheria.

Mrisha alidai kuwa hoja zote za Lissu hazina mashiko mahakama itupilie mbali ikatae kuzisikiliza.

Katika maombi ya msingi, maombi hayo ya kuvuliwa ubunge yalifunguliwa na Lissu kupitia mawakili wake hao chini ya hati ya dharura, kupitia kwa kaka yake Wakili Alute Mughwai, ambaye amempa mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa maombi namba 18 la mwaka 2019, Lissu anaiomba mahakama hiyo, impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika Ndugai ampe (Lissu) taarifa yake ya kumvua ubunge.

Anaiomba mahakama hiyo itengue na kutupilia mbali uamuzi huo wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

Mwombaji huyo anaomba mahakama itoe amri ya kusimamisha kuapishwa kwa Mbunge mteule wa jimbo hilo, Miraji Mtaturu wa Chama cha Mapinduzi.

Katika hati ya dharura Lissu anaiomba mahakama hiyo isikilize na kutoa uamuzi wa maombi yake haraka kwani vinginevyo, Mtaturu ambaye Julai 19 mwaka huu alitangazwa na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo ataapishwa kushika wadhifa huo.

Hivyo anadai atakuwa ameathirika kwa kuwa atapoteza haki zake zote, kinga na maslahi yake yote yanayoambatana na wadhifa wake huo wa ubunge.

Uamuzi wa kumvua ubunge ulitangazwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, Juni 28, 2019, wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge, huku akitaja sababu mbili.

Spika Ndugai alizitaja sababu hizo kuwa ni kushindwa kuhudhuria vikao vvya bunge kwa muda mrefu bila kumjulisha Spika kwa maandishi mahali aliko na sababu ya pili ni kutokuja taarifa za mali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Hata hivyo Spika Ndugai alijitetea kuwa si yeye aliyemvua ubunge bali ni Katiba ya Nchi.

HABARI MIKOANI

# Wananchi watakiwa kuona fahari ya kulipa kodi, tozo

**Na Sabato Kasika,** NACHINGWEA

WANANCHI wametakiwa kuona fahari kulipa kodi na tozo mbalimbali za serikali, huku wakitambua kwamba nchi zote duniani zinapata maendeleo kupitia kodi zinazolipwa na wao.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, wakati akifungua kampeni ya Wiki ya Mlipakodi na Tozo za Serikali wilayani Nachingwea.

"Ndio maana Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imepewa dhamana ya kusimamia, kutoza kodi na kuelimisha umma kujua umuhimu wa kulipa kodi," alisema Zambi.

Alisema bila wananchi kutoa kodi, nchi haiwezi kuendelea, na amewataka wakazi wa Nachingwea kuzingatia elimu waliopata kwa muda wa wiki moja ili walipe kodi bila kusukumwa.

Aliwataka wakazi wa Nachingwea walipata elimu hiyo kuwa mabalozi kwa wengine, ambao hawajaipata, ili kuhakikisha Nachingwea nzima inajua umuhimu kulipa kodi.

"Kumbukeni kwamba huduma zote zinazotolewa na serikali zinatokana na kodi, hivyo kila mmoja aone fahari kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo yake na nchi kwa ujumla," alisema.

Alifafanua kuwa baadhi ya watu huwa wanadai huduma mbalimbali zikiwamo za afya na kuwataka watambue kuwa kudai haki huwa kunakwenda sambamba na kutimiza wajibu.

Wajibu wenu ni kulipa kodi na tozo za serikali, mkifanya hivyo mna haki ya kudai huduma mbalimbali za serikali, lakini msipolipa kodi mnakosa uhalali wa kudai haki kutoka serikalini," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango ambaye aliandaa kampeni ya elimu hiyo, alisema alifikia hatua hiyo baada ya kubaini watu wengi hawajui umuhimu wa kulipa kodi.

"Lakini katika kufanikisha hili kuna wadau mbalimbali ambao wametuunga mkono wakiwamo Mashujaa FM, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na kampuni kama Hyseas na Sunshine," alisema.

"Baada ya kubaini hilo niliamua kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo TRA, Mashujaa FM, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na kampuni kama Hyseas na Sunshine, ambao wamsaidia sana katika kampeni hizi," alisema.

Alisema Nachingwea kuna wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo zaidi ya 300 ambao wote ni muhimu wapate elimu hiyo ili waweze kulipa kikamilifu kodi na tozo mbalimbali za serikali.

Alisema walikwenda kwenye tarafa zote tano za wilaya ambazo ni Kilimarondo, Naipanga, Nambambo, Lionja na Ruponda na kuitisha mikutano.

"Elimu iliyofika kwenye tarafa itashushwa kwenye kata, serikali za mitaa hadi kwa wananchi wote na itakuwa ni endelevu," alisema Muwango.

Alisema kwa sasa siyo wakati wa kulaumiana na wananchi, bali ni elimu na kisha taratibu za kisheria zitafuata kwa wale ambao hawataki kulipa kodi, huku wakijua wanatakiwa kufanya hivyo kwa maendeleo ya nchi.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hoteli ya Impala jijini Arusha, Joram Lemanya (kushoto), akijibu swali la mmoja wa waandishi wa habari (hawapo pichani) katika mahojiano juu ya mwelekeo wa sekta ya utalii na hoteli nchini na namna inavyochangia katika kukuza pato la taifa na ajira kwa vijana. Kulia ni mshauri mwelekezi wa hotel hiyo, Jois Kahigi (kulia). **PICHA: MPIGAPUCHA WETU**

# Serikali yaombwa kupunguza masharti usajili, kupata nembo

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANAWAKE wajasiriamali mkoani Mwanza wameiomba serikali kupunguza masharti usajili na upataji nembo ya ubora wa bidhaa kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ili kuwawezesha kupata fursa ya soko la nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) Mkoa wa Mwanza, Mariam Munanka , katika mkutano wanachama wa chemba hiyo na wadau ukiwa na lengo la kuwakutanisha wanawake wajasiriamali ili kujua changamoto zao, kubadilishana uzoefu na kuwakutanisha na taasisi zinazohusika na utoaji vibali na kifedha na kujua wapi aende na masharti ni yapi.

Munanka alisema, suala la kupata nembo ya ubora kutoka TBS ambayo inasaidia mjasiriamali kwenda kuuza nje bidhaa anazozalisha limekuwa kikwazo katika kupanua wigo wa kibiashara na masoko, kwani vigezo vyake ni vigumu ukilinganisha na mitaji walionayo wajasiriamali wadogo ambayo haifiki Sh. milioni nne.

"Ili kupata nembo ya ubora kutoka TBS, unatakiwa uwe umekidhi vigezo husika ikiwamo jengo lenye kiwango ambalo thamani yake si chini ya Sh. milioni 10, wakati ukiangalia mjasiriamali ana mtaji wa milioni moja, hali ambayo si rahisi kutimiza na kufanikiwa kuipata, hivyo ombi letu kwa serikali ni kupunguza masharti magumu ili kumwezesha mjasiriamali kupata fursa za masoko ya nje," alisema Munanka.

Alisema wapo wanachama zaidi ya 1,000 ila wenye nembo ya TBS hawazidi watatu, hali inayochangia kuwavunja moyo wajasiriamali wengine kujiunga na TWCC kwani anaona hatopata faida kama malengo ya kuanzishwa chemba hiyo yalivyo.

# JPM apewa tano kuboresha sekta utalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MABORESHO mbalimbali ya sheria za kodi yanayofanywa na Serikali ya Rais John Magufuli katika sekta ya utalii, yamechangia ongezeko la watalii wanaokuja hapa nchini, kuchangia mapato na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu changamoto na mwelekeo wa sekta ya utalii na huduma nchini, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hoteli ya Impala, Joram Lemanya, alisema sekta ya utalii ipo katika mwelekeo mzuri na idadi ya watalii imeongezeka.

"Juhudi za serikali na wadau katika sekta ya utalii imeanza kuzaa matunda. Hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau sekta ya utalii zimeshaanza kuzaa matunda," alisema Lemanya.

Alisisitiza kuwa sekta ya utalii nchini imepata msukumo mkubwa na pia kupongeza juhudi kubwa zinazofanywa za kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii kimataifa ikilinganishwa na hapo awali.

"Hoteli ya Impala imejipanga vizuri kupokea idadi ya wageni wengi kutoka kila pembe ya dunia kwani mwelekeo wa sekta ya utalii umekuwa nzuri na kupelekea vyumba ambavyo vilikuwa havitumiwi sasa vinaboreshwa kutokana na idadi ya watalii kuzidi kuongezeka," alisema Lemanya.

Alisema miezi miwili iliyopita kundi la watalii 5,000 kutoka China

waliingia nchini na kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo na wameahidi kuwa mabalozi wa kuitangaza Tanzania na vivutio vyake kwa Wachina wengine hivyo tunahakika idadi itazidi kuongezeka zaidi.

"Tayari nchi yetu inasoko la watalii kutoka Israel, Ujerumani, China na Marekani hivyo ni jukumu letu kuendelea kuboresha miundombinu ili wageni wazidi kumiminika na kuwafanya wafurahie kuja Tanzania na kuwa mabalozi wa kuitangaza nchi yetu," alisema.

Lemanya aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Maliasali na Utalii pamoja na taasisi zake kama Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro kwa kufanyia kazi changamoto zilizokuwapo kwa kuweka mazingira mazuri kuweka katika sekta ya utalii.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu huyo, Mkoa wa Arusha chini ya Mkuu wa wake, Mrisho Gambo pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama vimefanya kazi nzuri ya kuhakikisha sekta ya utalii inapiga hatua kwa kudhibiti vitendo vya aina yoyote ya uhalifu.

# RC awapa ma-DC, watendaji kibarua cha mimba shuleni

**Na Sabato Kasika,** NACHINGWEA

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, ameonyesha kukerwa na tatizo la mimba kwa wanafunzi na kuwaagiza wakuu wa wilaya na watendaji wote kusimamia ili kuhakikisha tatizo hilo linaisha.

Alisema inasikitisha kuona serikali ikikazania watoto wa kike kupata elimu, lakini bado kuna watu wanaendelea kuwapa mimba na kukatisha ndoto zao, huku baadhi ya wazazi wanashiriki kuficha wahusika wa mimba hizo.

Zambi alisema hayo juzi alipokuwa akihitimisha kampeni ya Wiki ya Mlipakodi na Tozo za Serikali iliokuwa ikiendeshwa kwa muda wa wiki moja wilayani Nachingwea.

"Kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu, zimeripotiwa mimba 100, bahati mbaya baadhi ya wazazi wanahusika katika tatizo hili, wakuu wa wilaya na watendaji wote fuatilieni," alisema Zambi.

Alisema wazazi wanaokubaliana na watu wanaowapa watoto wao mimba wanapokea fedha ya laana na kuagiza wote wafuatiliwe na kufikishwa kwenye vyombo vya dola ili kukomesha tabia hiyo.

Alitolea mfano tukio la mwanafunzi wa darasa la tatu katika moja ya shule za wilayani Kilwa kupewa ujauzito, huku babu yake akishiriki kumtafutia wanaume, na kusema kuwa watu wa aina hiyo siyo wa kuvumiliwa.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wazazi wawe na mazoea ya kufuatilia nyendo za watoto wao na wasiwape uhuru kupita kiasi, kwa vile matokeo yake ni kuwapo kwa mimba ambazo zinakatisha ndoto zao kielimu.

"Watu wanaowapa wanafunzi mimba wanazima ndoto zao kielimu na miongoni mwao ni madereva wa bodaboda na baadhi ya walimu ambao hawazingatii maadili ya kazi yao," alisema.

Zambi alifafanua kuwa mkoani mwake kuna zaidi ya walimu kumi wamewapa mimba wanafunzi na kukimbia vituo vyao vya kazi na hadi sasa hawajulikani walipo, lakini vyombo vya dola vinaendelea kuwatafuta.

"Vilevile kuna suala la jando na unyago, ambalo sitaki kupingana nalo, lakini wazazi acheni kuwapeleka watoto wenu huko wakati wa masomo, mnawaharibia maendeleo yao ya shule," alisema.

Alisema ni marufuku kupeleka watoto kwenye jando na unyago wakati shule zinaendelea na masomo, huku akiagiza viongozi na watendaji wa kata kufuatilia suala hilo kwa ukaribu ili kulikomesha.

"Siyo kwamba ninazuia mila na desturi bali ninachotaka ni kutowatoa watoto shule na kuwapeleka kwenye mambo hayo...waachwe wasome, hayo mambo mengine yafanyike baadaye," alisema.



Joel Muura (mwenye kofia) na Amos Muura, ambao ni wanachama wa kikundi kinachojishughulisha na kilimo cha bustani za mboga na mazao mengine cha Nyakabhungo, Kijiji cha Kanderema, Kata ya Bugoji, Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, wakihudumia bustani ya nyanya ya kikundi hicho juzi. Kikundi hicho ni miongoni mwa vilivyonufaika na fedha za Mfuko wa Jimbo. **MPIGA PICHA WETU**

## Sababu Mwenge kukacha madarasa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKIMBIZA Mwenge wa Uhuru mwaka 2019, Mzee Mkongea Ali, amegoma kufungua mradi wa ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Chang'a iliyopo Kata ya Tumbi Manispaa ya Tabora, kutokana na utata wa gharama.

Hatua hiyo aliichukuliwa jana baada ya kutilia shaka taarifa iliyotolewa kuhusiana na gharama za ujenzi wa madarasa hayo ambayo iliainishwa kuwa yalitumia mamilioni yaliyotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Mkongea Ali alisema kwamba kutokana na maelezo ya wataalamu kupishana katika kutoa taarifa za mradi huo, ambapo baadhi ya taarifa ilionyesha fedha iliyotolewa na kutumika ni shilingi milioni 3, na sio shilingi milioni saba.

Mkimbiza mwenge huyo alimwangiza Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufuatliia hesabu sahihi ya fedha zilizotolewa na kutumika hasa Sh. milioni nne na kumpatia maelezo hayo ndani ya wiki mbili.

Katika hatua nyingine, aliwataka wakazi wa mkoa wa Tabora kutunza vyanzo vya maji na miundombinu kwa kuwa serikali inatekeleza mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria ambapo zaidi ya Sh. bilioni 600 zimetolewa ili wananchi waweze kunufaika na mradi huo.

Alisema kwamba serikali inawajali wananchi wake, ndio maana inatekeleza mradi huo mkubwa katika mkoa wa Tabora ambapo zaidi ya wananchi milioni moja watanufaika na maji hayo.

Aidha, alisema kupitia kauli mbiu ya Mwenge mwaka huu inayosema "maji ni haki ya kila mtu, tuvitunze vyanzo vya maji' hivyo kila mwananchi anawajibu wa kupata huduma ya majisafi na salama kwa ajili ya afya.

Alisema kuwa serikali imetoa mamilioni ya fedha kwa halmashauri zote nchini ili kuboresha miundombinu na huduma mbalimbali za kijamii hivyo akawataka wadau wengine kuendelea kuunga mkono juhudi hizo ili kuwezesha upatikanaji wa huduma bora katika maeneo yote nchini.

# SMZ sasa kuombwa mamlaka vianzio maji

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KAMATI ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi, imesema itaishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kuanzisha mamlaka itakayoshughulikia vianzio vya maji pekee, ili kudhibiti na kulinda maeneo ya vianzio hivyo yasiharibiwe.

Akizungumza baada ya kuwasilishwa ripoti ya Mamlaka ya Maji Zanzibar Tawi la Pemba, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Hamza Hassan Juma, alisema, ni vyema kwa mamlaka kuvitafuta vianzio vyote vya maji na kuvidhibiti ili visiharibiwe na wananchi.

Alisema baadhi ya wananchi huharibu kwa kujenga kwenye maeneo ambayo ni vianzio vya maji, jambo ambalo linahatarisha usalama wa maji hayo.

"Tunapojenga nyumba zetu lazima tutajenga vyoo na makaro, iwapo tutajenga kwenye vianzio vya maji tutaharibu usalama wa maji, hivyo tutaishauri serikali kuanzisha mamlaka inayojitegemea ambayo itashughulikia vianzio vya maji tu, hii itasaidia kudhibiti wananchi wasijenge kwenye maeneo hayo," alisema.

Akiwasilisha ripoti hiyo Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Juma Bakar Alawi, alisema, jumla ya vituo (vianzio vya maji) 17 kisiwani Pemba vimefanyiwa matengenezo kwa kurekebishwa, kurejeshwa kisimaji na kubadilishwa pampu za maji.

Aidha, alisema Sh. 239,302,118 sawa na asilimia 68 zilikusanywa kutokana na mauzo ya maji pamoja na mapato ya ada za huduma kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

"Tulifunga mita 117 sawa na asilimia 19.5, tulisajili wateja 641 sawa na asilimia 77, kwa sasa wateja wa huduma ya maji wamefikia 47,597. Vile vile zilisomwa mita 1605 na mita 2827 sawa na asilimia 61 hazikusomwa," alisema.

Alieleza kuwa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma ya majisafi na salama haujafikia lengo, kutokana na wananchi wengi kutolipa huduma hiyo kwa wakati, ambapo mikakati yao ni kuwapitia wananchi majumbani kudai mapato hayo na kuondoa huduma kwa wadaiwa sugu.

Akiwasilisha ripoti ya Shirika la Nyumba Pemba, ofisa huyo alisema katika kipindi cha robo ya nne shirika lilikadiria kukusanya Sh. 700,000,000 kutoka kwenye vianzio vyake vya mapato, ambapo hadi kufikia Juni mwaka huu wamekusanya Sh. 635,003,700 sawa na asilimia 91 ya makadirio.

Waziri wa Wizara hiyo, Salama Aboud Talib, akielezea kuhusu deni wanaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuwa na mikataba kwa wapangaji wa shirika, kulipa kodi kwa wakati na matumizi bora ya nyumba hizo na kusema kuwa anaamini watafahamu na watalipa kodi bila ya usumbufu.

# Waaswa kufuatilia watoto badala ya kuchati

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Jerry Muro, amewaasa wazazi kutumia muda wao mwingi kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni badala ya kung'ang'ana na simu.

Aidha, Muro aliwaambia kuwa wanatumia muda mwingi kuchati kwenye simu badala ya kufanya mambo ya maendeleo yakiwamo kuangalia masomo, mitihani na maendeleo ya watoto shuleni.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika mahafali ya kwanza ya darasa la saba ya Shule ya Tumaini Mission iliyopo kata ya Imbaseni wilayani humo.

Muro alisema kuwa, wazazi wengi siku hizi wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenye simu za mkononi na kusahau majukumu ya kuwalea watoto wao, hali inayochangia kuharibika kwa watoto hao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

"Unajua wazazi wa siku hizi wapo bize sana na simu za mkononi kuliko watoto wao. Utamkuta mzazi anachati muda wote badala ya kukaa na watoto wao na kukagua madaftari ili kujua maendeleo ya masomo yao na kuweza kuwatia moyo, ambapo mwisho wa siku inachangia kupata matokeo mabaya katika masomo yao," alisema Muro na kuongeza:

"Wazazi nawaombeni sana jamani mjitahidi kuwa bize katika kufuatilia maendeleo ya watoto wenu shuleni kwani tunapowaacha watoto bila kuwaangalia wanaishia kuwa wahalifu na wavuta bangi. Ikiwa hivyo watakaoteseka ni sisi wenyewe wazazi, hivyo ni vizuri mkawaandaa watoto wetu vizuri ili kuepuka mambo hayo," alisema.

Kwa upande wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Namnyaki Leng'ida, alisema kuwa shule hiyo ilianza rasmi mwaka 2012 ikiwa na wanafunzi 16 ambapo hadi sasa ina jumla ya wanafunzi 298.

Namnyaki alisema kuwa, shule hiyo inafadhiliwa na marafiki kutoka nchini Denmark ambapo jumla ya watoto 100 wanaotokea katika mazingira magumu wananufaika huku wengine wakichangia gharama kwa ajili ya uendeshaji wa shule hiyo.

Alizitaja baadhi ya changamoto kuwa ni uhaba wa vitabu vya kufundishia.

Alisema wanashindwa kutambua kipi ni kitabu cha kiada kiongozi cha mwalimu na kipi cha ziada hivyo akaomba kupatiwa ufumbuzi wa changamoto hiyo.

Kwa upande wa mfadhili wa shule hiyo kutoka nchini Denmark, Torkild Jensen, alisema kuwa wanawasaidia watoto wanaotokea mazingira magumu katika kuhakikisha wanapata elimu iliyo sawa na wengine.

Pia alisema shule hiyo sio ya kwanza kusaidiwa bali wanasaidia na shule zingine katika kuhakikisha wanainua kiwango cha elimu nchini.

"Sisi tumekuwa tukijichanga fedha kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki wenzetu wa nchini Denmark kwa ajili ya kufanikisha suala zima la elimu kwa watoto wanaotokea mazingira magumu, ili nao wapate haki yao na tunaiunga mkono serikali kupitia Rais John Magufuli kutoa elimu bure," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya Shule hiyo ya Tumaini Mission Trust, Phillipo Petro, aliwataka wanafunzi hao kuwa mabalozi wazuri wa kutangaza shule hiyo popote waendapo huku wakiepukana na makundi yasiyofaa ambayo mwisho wa siku huwakatisha ndoto zao.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, akitoa maagizo ya serikali kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

## Wananchi waelekezwa fursa bomba la mafuta

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MKUU wa Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara, Chelestino Mofuga, amewataka wananchi wa eneo hilo, kuzitafuta na kuzichangamkia fursa zitokanazo na bomba la mafuta kutoka Uganda.

Mofuga aliyasema hayo juzi wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

Aliwaambia wana Mbulu wanapaswa kuchangamkia fursa mbalimbali kwenye mradi huo unaopita katika mkoa wa Manyara, ikiwamo kufanya biashara za aina mbalimbali.

Alisema mradi wa bomba hilo la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi jijini Tanga kupitia Manyara litapitia wilaya za Kiteto na Hanang.

"Tuwape elimu wananchi wetu ili wachangamkie fursa zitakazojitokeza kwenye mradi huo, ili wasiwe watazamaji huku wakiwaachia wajasiriamali wengine wafaidi ilhali uwezo wa kuchangamkia fursa wanao," alisema Mofuga.

Alisema kila kambi ya ujenzi wa bomba hilo itakuwa na watu 2,000 hivyo ni wakati sahihi wa kuchangamkia nafasi hiyo ikiwamo kufanya biashara ya vitunguu na kuku na siyo kuwa watazamaji.

"Tuwaandae wananchi wetu wapate elimu ya ufanikishaji hilo kwa kuwa na bidhaa bora na tutawaita wataalamu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ili wawape elimu zaidi," alisema Mofuga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Hudson Kamoga, alilieleza baraza hilo kuwa ujenzi wa miradi ya hospitali mpya ya wilaya na jengo la utawala la halmashauri inaendelea.

"Tunamshukuru Rais John Magufuli, kwa kutupatia fedha mbalimbali za miradi hiyo zikiwamo za hospitali mpya na makao makuu mapya ya halmashauri katika Kata ya Dongobesh," alisema Kamoga.

Diwani wa Kata ya Dongobesh, Elimiana Shishi, alisema atatumia nafasi hiyo kwa kuwaeleza wananchi wa eneo hilo kuchangamkia fursa ya ujenzi wa bomba hilo la mafuta.

# Wapigwa marufuku kucharaza viboko

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WALIMU wanaofundisha watoto wa shule za awali wamepigwa marufuku kuwachapa viboko wanafunzi wao hao wadogo ili kuepusha uwezekano wa kukimbia shule.

Aidha, wameambiwa kuwa kuwatandika watoto hao kutawakimbiza shule kwa vile bado ni wadogo na wanaogopa.

Marufuku hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Ofisa Elimu Taaluma wa Halmashauri ya Babati, Joyce Uronu, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu matumizi ya zana za kufundishia kwa wanafunzi wa awali.

Alisema wanafunzi hao wanastahili kuanza shule wakiwa na miaka minne hadi mitano, hivyo hawatakiwi kuchapwa.

"Walimu wa awali wanatakiwa kuwapenda sana watoto hawa ili wasiwachukie na kuchukia shule, maana muda mwingi mwalimu inabidi awafanyie vitu vya kuwafurahisha," alisema Uronu.

Alisema halmashauri hiyo ilibahatika kuwapatia mafunzo walimu wa awali 138, katika mpango wake wa kufundisha walimu hao namna ya kutumia zana za kufundishia uliofanywa na serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Lanes.

Joyce alisema lengo la mpango huo ilikuwa ni kuwasaidia walimu wa awali, kuandaa zana za kufundishia watoto hao kwa vitendo na kuepusha kutumia nadharia ambayo inawafikirisha wanafunzi.

Alifafanua kuwa zana zipo za aina tofauti ambazo ni za kutengeneza kama vile jembe, kiti, meza na zingine ni za kununua mfano mpira, midori na picarp.

Aidha, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Babati, Getrude Kavishe, alisema watoto wa awali wanatakiwa kusoma miaka miwili ambapo mwaka wa kwanza hatakiwi kufundishwa masomo ya darasani, badala yake ni nyimbo na michezo mingine na kufundishwa vitu ambavyo vipo kwenye mazingira.

Kavishe alisema mwalimu anapotumia zana inamsaidia mwanafunzi katika ukuaji wa ubongo kwa kuwa mbunifu, zana zinamsaidia kujenga kumbukumbu na kulipenda somo.

Mwalimu wa awali Jemima Njidile kutoka Shule ya Msingi Dudumera alisema wanafunzi wa awali hawatakiwi kuchanganywa na wengine, maana mitaala yao ni tofauti na wanafunzi wa shule ya msingi.

Njidile alikiri kuwa watoto hao hawatakiwi kuchapwa maana wakichapwa wanakata tamaa na wanaogopa mwisho wanakimbia.

# Rasilimali madini yaibua maswali Same

**Na Godfrey Mushi,** SAME

UTAJIRI wa madini ya vito ya green na red tormeline, rubi na dhahabu katika Wilaya ya Same, unaacha maswali lukuki ya kwa nini bado wananchi wake wanaishi katika lindi la umaskini, licha ya kugunduliwa idadi kubwa ya madini ya aina mbalimbali.

Juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, alithibitisha kugunduliwa kwa aina mpya ya madini ya green na red tormeline.

"Ni kweli mimi na kamati yangu, tumekwenda kujiridhisha kwa kutembelea maeneo mbalimbali yanayopatikana madini kama green na red tormeline, bauxite, almandite, blue sapphire na zilicon," alisema.

Maeneo yaliyogunduliwa kuwa na utajiri wa madini hayo ni Kata za Kisiwani, Gonja, Ruvu na Same.

Kutokana na kugunduliwa kwa madini hayo, Senyamule ambaye ni Mkuu wa Wilaya hiyo, ameagiza wachimbaji wote wadogo wanaofanya kazi hiyo wawe wamerasimishwa ndani ya siku 30.

"Naelekeza sasa, ofisa madini na timu yako, endeleeni na zoezi la kurasimisha maeneo yote ya uchimbaji wa madini yaliyopo ndani ya wilaya hii ili wachimbaji wachimbe madini kwa kuzingatia sheria na taratibu zinazoongoza biashara ya madini. Hata hivyo, nawapongeza kwa kuleta madini sokoni na ninawahakikishia madini yaliyopo wanunuzi watakuja na kipato chenu kitaongezeka," alieleza zaidi. Alisema wilaya hiyo inayo hazina kubwa ya madini ambayo yameshagundulika na kuanza kuchimbwa na kwamba kuwepo kwa soko la madini katika Wilaya ya Same kumeongeza uhakika wa soko kwa wachimbaji wa madini ya vito na metali.

Hata hivyo, kuwapo kwa utajiri huo wa vito ni tofauti na matarajio kwamba eneo hilo lingekuwa na miundombinu mizuri ya barabara, upatikanaji wa huduma za kijamii na kukua kwa uchumi kwa eneo hilo kutokana na kuwa na madini adimu, lakini wilaya hiyo iko nyuma kiuchumi.

Katika kata hizo za Kisiwani, Gonja, Ruvu na Same, hakuna uwekezekaji mkubwa uliofanywa na watu binafsi katika migodi, huku barabara za kuingia na kutoka kata hizo zikiwa na vumbi, licha ya kuwa halmashauri tangu mwaka 1984.

Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, inawataka wachimbaji kuwa na leseni za uchimbaji ambazo zinatolewa na Wizara ya Madini na hutakiwa kupelekwa kwenye halmashauri husika kwa ajili ya kutoa taarifa na kuendelea na uchimbaji.

## Ashangaa malalamiko kwa viongozi kitaifa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIBU Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji) wa Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Msoka, amesema ni jambo la aibu kuona wananchi wanaendelea kupeleka malalamiko yao kwa viongozi wa kitaifa, kwa sababu ya watendaji wa serikali za mitaa, vijiji na kata kuweka kando wajibu wao.

Hayo yamo katika maelekezo yaliyotolewa kwa halmashauri saba za mkoa wa Kilimanjaro na Katibu Tawala wa mkoa huo, Aisha Amour, akitaka kila halmashauri kujiuliza hayo kwenye vikao kazi vya maofisa watendaji.

Katika maelekezo hayo, imeelekezwa kwamba wakati wowote ukiona idadi kubwa ya wananchi wanapanga foleni kila uchao katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya au Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika, akili yako inapaswa kujielekeza kwa kujiuliza maswali ya walipo watendaji wa chini yake.

"Ukikuta wananchi wengi wamejaa kwenye ofisi ya Mkurugenzi au Mkuu wa Wilaya ni lazima wewe kama mtendaji wa mtaa, kijiji au kata, ujiulize kama kweli unatosha kwenye nafasi yako," alieleza Msoka.

Kutokana na watendaji wengi kujisahau majukumu yao, ofisi hiyo imetoa wito kwa watumishi wa umma kutimiza wajibu na majukumu ya kazi zao kwa uadilifu na kuimarisha huduma kwa wananchi walio kwenye maeneo yao.

Aidha, ofisi hiyo pia imeelekeza watendaji hao kuhakikisha wanatatua kero za wananchi kwenye maeneo yao ili kupunguza malalamiko yanayopelekwa na wananchi kwa viongozi wa kitaifa.



Mkuu wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule (kushoto), akizungumza na wachimbaji wadogo wa madini ya vito katika Kijiji cha Ruvu-Marwa, Kata ya Ruvu jana, baada ya kutembelea machimbo hayo ya madini ya Bauxite. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## Watendaji, wenyeviti vijiji watakaoua miradi kukiona

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WILAYA ya Same, imeahidi kuwachukulia hatua kali za kinidhamu watendaji wa kata, watendaji na wenyeviti wa vijiji watakaosababisha kufa kwa miradi ya maendeleo iliyofadhiliwa na Shirika la World Vision Tanzania.

Maelekezo hayo yametolewa wilayani hapa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, wakati wa hafla ya kukabidhiwa miradi miwili ya Nakombo na Makindube AP iliyokuwa ikifadhiliwa na World Vision.

Senyamule alisema muda wa miaka 15 kwa mradi wa Makindube na miaka 17 kwa Nakombo imegusa maeneo muhimu kwa binadamu hivyo ni muhimu ikapewa nafasi ya kuendelezwa kama ilivyokuwa kwa wafadhili.

"World Vision walitushika mkono sasa wanaondoka, tujione kama tunaweza kufanya wenyewe wajibu wetu ni kuona kazi waliyoianzisha tuifanye iwe endelevu. Serikali itachukua hatua kwa kiongozi yeyote atakayefanya uzembe kwenye miradi hii nikija kwenye maeneo yenu moja ya taarifa nitakazotaka kusikia ni miradi ya WVT inaendeleaje," alisema Senyamule.

Kwa upande wake Mwakilishi wa World Vision Australia waliofadhili mradi wa Nakombo AP Tarafa ya Mwembe Mbaga, Steven Dunham, aliwapongeza wananchi hao kwa kuchukua fursa ili kuboresha maisha yao.

Naye Mwenyekiti wa Mradi wa Makindumbe uliopo Tarafa ya Ndungu Zacharia Mohamed, alisema, mradi huo umechangia kuleta mabadiliko chanya miongoni mwa wanajamii hasa watoto wa eneo la mradi.

Alitaja baadhi ya mafanikio ya mradi huo kuwa ni pamoja na kuwezesha asilimia 87.3 ya jamii ya Makindube kujitosheleza kwa chakula kwa mwaka mzima asilimia 93 ya kaya wana uwezo wa kula milo mitatu kwa siku.

Alisema katika kuchangia lengo la elimu mradi umejihusisha na kuongeza miundombinu, kuboresha mazingira ya kusomea na taaluma kwa ujumla ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kupandisha kiwango cha ufaulu.

"Asilimia 97.2 ya watoto wanaenda shule ukilinganisha na asilimia 76.7 mwaka 2004," alisema Mohamed.

Aidha, Mwenyekiti wa Mradi wa Nakombo AP uliopo Tarafa ya Mwembe Mbaga, Senge Mkwizu, alisema lengo la mradi wa afya na lishe lilikuwa kuchangia ustawi wa afya na lishe ya watoto ifikapo mwaka 2019.

"Mradi kwa kushirikiana na wadau wa afya umechangia mabadiliko makubwa katika sekta hii ili kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa na afya na lishe nzuri wakati wote. Kumekuwa na ongezeko la watoto wanaopata vyakula mchanganyiko vyenye lishe kutoka asilimia 53 mwaka 2012 hadi asilimia 65.4 mwaka 2019."


Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 3, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 14



**Tanzania bila ya dawa za kulevya inawezekana**

Ukurasa 18



## JE, WAJUA?

Wakati moto ukiiteketeza Amazon, msitu Bonde la Kongo unawaka



Ukurasa 17

## JIELIMISHE

**Elimu ya wakimbizi iko katika janga: UNHCR**



# Mahakama ikitumiwa ipasavyo italinda mazingira nchini

Ukurasa 15

ELIMU KUTOKA POLISI

# Tanzania bila ya dawa za kulevya inawezekana



Mtumiaji wa dawa za kulevya, akijidunga sindano ya dawa hizo. **PICHA: MTANDAO**

TATIZO la dawa za kulevya hapa nchini bado linaendelea kuathiri taifa na jamii kiujumla.

Kosa la dawa za kulevya ni miongoni mwa makosa ya jinai ambalo kisheria limekuwa likipewa mtazamo wa kipekee kulingana na athari zake kijamii na Kitaifa.

Kosa hili limekuwa tishio kwa usalama wa wananchi na taifa kwani limekuwa likizalisha makosa mengine ambayo ni makubwa na yanaathiri jamii.

Makosa kama vile usafirishaji haramu wa binadamu (human trafficking), utakatishaji wa pesa (Money laundering) na makosa mengine yanayovuka mipaka ya nchi (trans-national organized crime). Serikali ikishirikiana na wadau wengine ndani na nje ya nchi imekuwa ikifanya jitihada katika kuzuia na kupambana na tatizo hili kwa kutumia vyombo vyake vya Dola.

Vyombo vinavyohusika katika udhibiti na upambanaji wa dawa za kulevya, Polisi chini ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ikisaidiana na wadau wengine wanaohusika kwenye ukamataji na upelelezaji wa makosa haya kuhakikisha tatizo hili linadhibitiwa katika nyanja zote za kijamii na kitaifa.

### MIKAKATI YA KUKABILIANA NA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA

Jeshi la Polisi limeanzisha madawati maalamu yanayoshughulika katika Ukamataji, Upelelezi na Ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia kwa makosa ya dawa za kulevya, ikisaidiana na kitengo cha Polisi Jamii katika Mikoa yote pamoja na kanda zake.

Uelimishaji wa jamii katika athari za matumizi ya dawa za kulevya, uuzaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, kwa kutumia fursa hizo katika makongamano mbalimbali, warsha, sherehe za kitaifa ili kupunguza tatizo hilo haraka kuliko kupambana na raia moja moja au vikundi vidogo vidogo.

Uimarishaji wa doria, misako na Operesheni katika vijiwe na mitaa yote ambayo wahalifu hao wamekuwa wakikaa na kufanya biashara hiyo ya dawa za kulevya, hivyo kupunguza tatizo hilo kwa baadhi ya mitaa na vijiwe vingine kupelekea kusambaratishwa kabisa.

Kuimarisha doria za majini na ulinzi mipakani mfano Airport na mipaka ya nchi kavu kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kiserikali na zile za binafsi katika kupambana na wahalifu ambao wamekuwa wakitumia maboti na majahazi ya kisasa kuingiza dawa za kulevya, pia usafiri wa ndege katika kuingiza na kutoka nje ya nchi.

Mafunzo ya kuwajenga wapelelezi na watafutaji wa taarifa (intelligence) yamekuwa yakitolewa ndani na nje ya nchi kwa udhamini wa wadau mbalimbali kutoka nchi wahisani ambayo yamekuwa yakidhaminiwa kwa kiasi kikubwa na taasisi hizo, hivyo kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kusaidia kupunguza tatizo la dawa za kulevya.

### MIKAKATI KIJAMII

Kuimarika kwa mfumo wa utoaji taarifa kutoka kwa jamii husika kutokana na uhamasishaji na uelimishaji kuhusu athari za dawa za kulevya, unaotolewa na Jeshi la Polisi pamoja na wadau wake.

Vilevile kutokana na mzigo ambao familia, jamii husika na taifa imekuwa ikipata kutokana na kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya, hivyo jamii yenyewe wamehamasika katika kushiriki moja kwa moja kwenye utoaji wa taarifa za uhalifu na wahalifu wa dawa za kulevya bila shuruti.

Taasisi binafsi, baadhi ya wananchi wazawa, taasisi za kidini na wadau wengine wameshiriki kwenye vita hii ya kupambana na dawa za kulevya kwa kujenga na kuanzisha vituo vya kulelea waathirika wa dawa za kulevya (Sober houses) katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanashiriki katika udhibiti na upambanaji wa janga la dawa za kulevya kwa watoto na vijana kwa kuunda vikundi vya michezo mbalimbali inayohusisha makundi ya vijana wa mitaani.

Pia watoto walio katika kambi za kulelea watoto/wanaoishi katika mazingira magumu, na wanafunzi waliopo kwenye vyuo mbalimbali.

### MIKAKATI KITAIFA

Kutungwa kwa sheria mpya Na 5 ya mwaka 2015 ambayo imefanya baadhi ya marekebisho katika sheria ya zamani kwa kuweza kuziba mianya na mapungufu yote ambayo wahalifu wamekuwa wakitumia katika kukwepa mkono wa sheria.

Kuundwa kwa Mamlaka Ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ambayo imepewa nguvu ya kukamata, kupeleleza, kukusanya taaarifa za uhalifu na wahalifu wa dawa za kulevya, hivyo kusaidia Jeshi la Polisi na taasisi nyingine zisizo za kiserikali zinazojihusisha katika kupambana na uhalifu huu kupunguza kasi za ongezeko la tatizo.

Wizara ya Afya kama Wizara simamizi katika kutibu, kuratibu na kutoa ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa za kulevya imeruhusu na kuendelea kutengeneza mazingira mazuri kwa wadau wa taasisi binafsi, mashirika ya dini na wananchi wenyewe kuanzisha vituo vya kulelea waathirika wa dawa za kulevya (sober houses) kwa gharama ndogo ambazo familia au jamii wanaweza kupeleka waathirika hao kwa tiba na ushauri nasaha.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya Uhusiano***
***Makao Makuu ya Polisi.***
***S.L.P. 9141,***
***DAR ES SALAAM***



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Anayepandisha wengine ngazini ...

"ANAYEPANDISHA wengine ngazini, hupigwa teke menoni." Maana yake mtu anayewabeba na kuwapandisha wengine ngazini huishia kupigwa teke menoni na wanaopanda kwa kuwa hawaangalii nyuma.

Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu aliyemtendea mwingine hisani fulani kisha asipate shukrani au fadhila.

Najifananisha na anaowapandisha wengine ngazini kwa jinsi nisivyoeleweka na waandishi wenzangu. Ingawa napata wakati mgumu kusahihisha maneno ya Kiswahili yatumiwayo na waandishi wa magazeti ya michezo wasiofuata maelekezo niwapayo kila Jumanne katika gazeti hili, sitochoka kuitetea lugha yetu ya taifa.

"Taratibu ndio mwendo" kwani mwendo ulio sawa ni wa taratibu. Methali hii hutumiwa kumkanya mtu anayefanya mambo yake kwa pupa au vishindo na kuishia kuyaharibu.

Wahenga walisema: "Asiyesikia hujionea mwenyewe." Maana yake mtu asiyesikiliza ushauri wa anayemzidi maarifa hufikwa na balaa au hupatwa na matatizo. Ni methali ya kutumiwa kutunasihi tuyathamini mashauri tupewayo na wanaotuzidi maarifa.

Sithubutu kusema nawazidi maarifa waandishi wenzangu ila waendapo arijojo (hali ya kupotea; hali ya kupoteza mwelekeo) nawajibika kuwaonesha njia sahihi. Ninachopigania ni matumizi halisi (-enye dhati ya asili; kindakindaki) ya lugha ya Kiswahili. Pia mpangilio wa maneno ya sentensi zinazoeleweka kwa watu wa rika zote mijini na vijijini.

"Kagere kaanza balaa mapemaa" ni kichwa cha habari cha gazeti maarufu la michezo nchini. Nimeeleza mara nyingi kuwa 'balaa' au 'baa' maana yake ni janga lililoenea katika jamii au kwa mtu binafsi; beluwa. Pia ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku.

Ibara (kifungu cha maelezo kinachojitosheleza; paragrafu) ya pili chini ya kichwa cha habari hiyo iliandikwa:

"Lakini wakati nyota wakiendelea kujifua waliwaacha nyuma mastaa wanne, akiwamo Meddie Kagere ambaye ndani ya siku mbili tu za mazoezi licha ya kuchelewa kujiunga na wenzake tayari ameanza mambo ya hatari." Yafaa waandishi watambue kuwa "tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena." Twakumbushwa kwamba jambo lolote zuri huwa na mipaka.

Sentensi haianzwi na neno 'lakini' kama ilivyotumiwa na mwandishi wa habari ninayoikosoa. 'Lakini' ni tamko la kuonesha upungufu, kasoro ya jambo au hitilafu. Mfano: 'Saa mbili kasa (kasoro) robo) n.k.

'Fua' ni kitendo cha kusafisha nguo kwa maji na sabuni ukitumia mikono au mashine. 2) Toa makumbi kutoka kwenye nazi kwa kutumia kitu chenye ncha kilichokitwa chini. 3) Tengeneza kitu kwa kutumia chuma, dhahabu, fedha au metali (madini magumu yoyote yanayoweza kupitisha joto la umeme) nyingine. 4) Kitendo cha kumfanyia mtu dawa ili kumwondolea nuhusi (nuksi); kisirani. Je, wachezaji 'hujifuaje?' Nani aliyewasababishia kisirani hicho na kwa sababu gani?

Sentensi ingeandikwa: "Wakati wachezaji wakiendelea na mazoezi, nyuma walikuwa wanne akiwamo Meddie Kagere ambaye licha ya kuchelewa kujiunga na wenzake, mazoezi aliyofanya siku mbili tu alithibitisha umuhimu wake.

" ... (jina la gazeti husika) ambalo limepiga kambi hapa Rustenburg linafahamu Kahata ambaye ni miongoni mwa usajili uliokuwa mapendekezo ya Aussems alikuwa na maelewano na washambuliaji Kagere, John Boko na Wilker Henrique ambao walikuwa wakitumia vyema krosi na pasi ambazo alizokuwa akiwapatia. (maneno 38) .

Wahenga watwambia: "Chungu kiinjike (kiweke chombo cha kupikia juu ya jiko; teleka) moto ukishawaka." Maana yake ni vizuri kuwasha moto kwanza kabla ya kuteleka chungu mekoni. Methali hii yatufunza umuhimu wa kufanya mambo hatua kwa hatua, kwa mpango. Yafaa kujua mambo ya kutangulizwa au ya kupewa kipaumbele na yapi ya baadaye.

Kwa kuwa ukurasa huo una jina la mwandishi, picha yake na maandishi: "Kutoka kambi ya Simba Afrika Kusini" hakuwa na sababu ya kuandika "... (jina la gazeti) ambalo limepiga kambi hapa Rustenburg." Kwa kuwa yajulikana timu ya Simba ipo kambini Afrika ya Kusini, hakuna sababu ya kurejelea (pitia jambo au kitu kwa mara nyingine) maelezo hayo.

Ingeandikwa: "Kahata anaelewana vizuri na washambuliaji Kagere, John Boko na Wilker Henrique wakitumia vizuri krosi (upigaji wa mpira kutoka eneo la pembeni kuelekea golini) na pasi (kumpigia mpira mwenzako wakati wa mchezo) alizowapa."

**Methali: Asiyeuliza hana ajifunzalo.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# ELIMU

NA FRANSISKO MPANGALA

# Mahakama ikitumiwa ipasavyo italinda mazingira nchini



Uchafuzi kama huu katika miji yetu unaweza ukadhibitiwa kikamilifu kwa kuitumia Mahakama. **PICHA: MTANDAO**

MOJA ya vitu muhimu kwenye maisha yetu ya kila siku ni kuwa na mazingira safi na salama.

Kwa kulitambua hili, zimekuwapo juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira nchini.

Hatua hizo ni pamoja na kusimamia na kutekeleza sera, sheria, mikakati na mipango mbalimbali ya kuhifadhi mazingira, kutoa elimu kwa umma ya namna gani wanaweza kulinda mazingira pamoja na kusaini mikataba ya kimataifa yenye lengo la kulinda mazingira nchini.

Juhudi hizi za serikali zinalenga kukabiliana na hali halisi ya kimazingira isiyoridhisha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na NAFORMA (National Forestry Resources Monitoring and Assessment) inabainisha kuwa nchi inapoteza takriban hekta 372,000 za misitu ya asili kila mwaka.

Taarifa hii inaonyesha kuwa endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa, kuna hatari nchi yetu ikageuka jangwa siku za usoni.

Kama uharibifu wa mazingira hautadhibitiwa, basi tutarajie majanga yanayosababishwa na ukame kuongezeka, vyanzo vya maji kuzidi kuharibika, mvua kutotabirika, rutuba ya ardhi kupungua na afya za watu kuendelea kuwa hatarini.

Kwa maana hii, pamoja na kuwapo juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kulinda mazingira, ipo haja ya mihimili mingine ya dola kuzidi kutumia mamlaka zake kuiongeza nguvu serikali.

Moja ya mhimili wa dola unaoisaidia serikali kulinda mazingira ni Mahakama.

Mahakama inayo nafasi ya kutoa mchango mkubwa wa kulinda mazingira nchini.

Makala hii itatoa elimu na kufafanua ni kwa namna gani Mahakama inaweza kulinda mazingira.

### MAANA YA MAHAKAMA

Mahakama ni moja ya mihimili mitatu ya dola. Ina mamlaka ya kutoa maamuzi katika migogoro baina ya pande mbili, kusimamia utawala wa sheria na kufanya maamuzi kuhusu mashauri ya jinai na madai kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mahakama ni mhimili ulio na kauli ya mwisho katika utoaji wa haki nchini. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 107A (I) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Yawezekana msomaji wa makala hii ukajiuliza, kama jukumu kuu la Mahakama ni kutoa haki, Je ni kwa namna gani chombo hiki cha kutenda haki kinaweza kulinda mazingira nchini?

> Mbali na kusaidia kulinda mazingira, Mahakama pia inasaidia kutoa fidia kwa watu mbalimbali wanaoathiriwa na shughuli za kuchafua au kuharibu mazingira.

Mahakama inalinda mazingira kwa namna mbili.

### ZUIO

Kwanza, Mahakama ina mamlaka ya kutoa zuio dhidi ya shughuli zozote zinazohatarisha afya za watu au kusababisha uharibifu wa mazingira.

Katika kesi ya Festo Belegele dhidi ya Baraza la mji wa Dar es Salaam (Mahakama Kuu ya Tanzania, Kesi ya Madai namba 90 ya mwaka 1991), Mahakama ilieleza kuwa kitendo cha Baraza la Mji kutupa taka na uchafu kwenye maeneo ya Kunduchi Mtongani, kilikuwa kinyume na Sheria za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982.

Pia, kitendo cha Baraza la Mji kutupa taka eneo la Kunduchi Mtongani kilikuwa kinyume na Mwongozo Mkuu wa Mji, kwani mbali na kuwaletea kero na usumbufu wakazi wa maeneo hayo, kilihatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo.

Mahakama ilitoa amri kwa Baraza la Mji kusitisha mara moja zoezi hilo la utupwaji taka na uchafu kwenye maeneo ya makazi ya watu kwa kuwa kitendo hicho kilihatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo na kilikuwa kinyume na Ibara ya 14 ya Katiba ya nchi inayotoa haki ya ulinzi wa maisha kwa wananchi wote.

Kupitia hukumu hii, tunaona kuwa Mahakama ina mamlaka ya kuzuia shughuli zozote zinazoharibu mazingira kupitia maombi yanayoletwa mbele yake.

Ieleweke kuwa si lazima mtu asubiri mpaka shughuli za kuharibu mazingira zianze ndipo akimbilie mahakamani. Mtu anaweza kwenda mahakamani kuomba zuio la kimahakama akijiridhisha kuwa zipo dalili za wazi na ushahidi wa kutosha kuwa mhusika fulani ana mpango wa kuharibu mazingira kutokana na shughuli anazotaka kufanya.

### FAIDA

Faida kubwa ya mazuio haya ya Kimahakama ni kuepusha mazingira kutoharibiwa kabisa au kutoharibiwa zaidi.

### ADHABU

Pili, Mahakama inalinda mazingira kupitia adhabu za vifungo au faini (au vyote kwa pamoja) inazotoa kwa watu, kampuni au taasisi mbalimbali zinazokutwa na hatia ya kuharibu au kuchafua mazingira kinyume na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Adhabu hizi za faini na vifungo hutolewa na Mahakama kwa lengo la kubadili tabia ya mkosaji, kumfanya mkosaji ajutie kuharibu mazingira na kumpa elimu mkosaji kuwa vitendo vya kuharibu mazingira haviruhusiwi kwa mujibu wa sheria.

Isitoshe, adhabu zinazotolewa na Mahakama hutumika kama mifano kwa watu wengine kwenye jamii kuwa endapo wataharibu mazingira kinyume na sheria ya mazingira, watakabiliana na adhabu kali kama walizopewa wakosaji wengine waliokutwa na hatia ya kuharibu mazingira.

Adhabu hizi zinazotolewa na Mahakama zina faida katika kulinda mazingira kwa kuwa zinaelimisha, zina adabisha na kujenga hofu kwa watu kuwa wakiharibu mazingira kinyume na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, watakabiliwa na adhabu kali na hivyo kufanya watu kuacha kuharibu mazingira kinyume na sheria.

Mbali na kusaidia kulinda mazingira, Mahakama pia inasaidia kutoa fidia kwa watu mbalimbali wanaoathiriwa na shughuli za kuchafua au kuharibu mazingira.

Fidia hizi zinatolewa pale tu Mahakama inapojiridhisha kuwa vitendo vya watu, taasisi au kampuni kuchafua au kuharibu mazingira vimehatarisha afya na vimeleta usumbufu kwa wananchi kwenye maeneo yao.

### CHANGAMOTO

Zipo changamoto mbili zinazoikabili Mahakama katika kuitumia nafasi yake kulinda mazingira nchini. Kwanza, kuna idadi ndogo ya Mahakama nchini.

Kwenye utafiti uliofanyika kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kata zilizopo nchini ni 3,957. Mahakama za mwanzo zipo katika kata 976 tu kati ya kata 3,957.

Hii ni kama asilimia 24.6 ya kata zote nchini ndio zinazopata angalau huduma ya Mahakama ya Mwanzo.

Ingawa hizi ni takwimu za mwaka 2015 na huu ni mwaka 2019, sidhani kama kuna ongezeko kubwa la idadi ya Mahakama kiasi cha kuathiri hoja yangu kuwa kuna idadi ndogo ya Mahakama nchini.

***Barua Pepe; fransiscompangala08@gmail.com***

SHERIA

**NA MASHAKA MGETA**

# Sheria iboreshwe kudhibiti ajali za barabarani nchini



Matukio ya ajali za barabarani kama hizi ambazo zinachangiwa na sababu mbalimbali zikipoteza maisha na mali za watu **PICHA ZOTE: MTANDAO**

HIVI sasa Taifa linaomboleza vifo vya watu zaidi ya 100 waliopoteza maisha kutokana na ajali ya gari la mafuta kupinduka na kuwaka moto mkoani Mogororo.

Ajali hiyo ni mwendelezo wa ajali nyingi za barabarani na maeneo mengine ya usafiri zinazotokea na kugharimu maisha ya watu, uharibifu wa mali na kuharibu mifumo ya uchumi nchini.

Jambo la msingi linalotarajiwa na wadau wengi, ni kuiona Tanzania inaendelea pasipokuwa na ajali za barabarani.

Pasipo kujielekeza katika ajali iliyotokea mkoani Morogoro, matukio kama hayo yanasababishwa na vyanzo tofauti, miongoni mwao vimeainishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Maeneo matano yanayoainishwa na WHO ni mwendokasi, ulevi, kutovaa kofia ngumu kwa waendesha pikipiki, kutofunga mikanda na ukosefu wa viti vya watoto kwenye magari.

Nchi mbalimbali zimejiwekea mifumo ikiwamo ya kisheria, inayolenga kudhibiti vyanzo vyote vya ajali za barabarani.

Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo ambayo licha ya kuwa na sheria ya usalama ya mwaka 1973, lakini imeonekana kuwa na upungufu unaohitaji maboresho ya haraka ili kusaidia udhibiti wa ajali hizo.

Moja ya vipengele 'vinavyopigiwa upatu' ili vifanyiwe marekebisho katika maboresho ya sheria hiyo nchini ni kinachohusiana na ulevi.

> “ Ningependa sana kiwango hicho cha kilevi kiwe sifuri kwa hapa nchini, lakini kwa vile mwili wa binadamu una ming'emenyo inayotengeneza kiwango kidogo cha kilevi mwilini, hatuna namna.



Askari wa usalama barabarani (kushoto) akimpima dereva kiwango cha ulevi.

Vyanzo tofauti vimethibitisha kuwa uendeshaji wa gari wakati dereva akiwa amelewa unaathiriwa kwa kukosekana umakini na kusabisha uchovu, ikiwa ni miongoni mwa mambo yanayoweza kusababisha kutokea kwa ajali.

Damu yenye kilevi na udhibiti dhidi ya madereva walevi ni miongoni mwa vifungu vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973, kuanzia vifungu cha 44 hadi cha 49

Maeneo yanayotajwa na vifungu vyake kwenye mabano ni kuendesha gari ukiwa umeathiriwa kwa kilevi ama dawa za kulevya (44), kuendesha gari ukiwa na zaidi ya kiwango cha ukomo wa kilevi kwenye damu (45), upimaji kiwango cha kilevi kwenye damu (46) na upimaji kilevi kwa njia ya kuvuta hewa (46A).

Vifungu vingine ni kupima kilevi kwa kutumia kifaa kinachojulikana na alcometer (46B), watu waliodhinishwa na kupima na kutoa majibu ya damu (47), kuwaweka ndani washukiwa wa ulevi (48).

Tafsiri ya ukomo wa kiwango cha kilevi kwenye damu ipo kwenye kifungu cha 49. Kwa mujibu wa tafsiri hiyo, kiwango cha ulevi kilichoainishwa katika sheria hiyo ni 0.08g/dl.

Kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa ni kiwango kilichoainishwa au kupitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ambacho ni 0.05g/dl na 0.02g/dl kwa dereva asiyekuwa mzoefu.

Tathimini ya mwandishi wa makala haya imebaini kuwa sheria hiyo ina mapungufu mengine ambayo haitofautishi kiwango na uzoefu wa dereva na vinasaba vya ulevi katika damu zao.

Kwa mfano, kwa mujibu wa ripoti ya WHO, vijana wako katika hatari kubwa ya ajali za barabarani zinazohusiana na unywaji pombe.

Ripoti ya WHO inaeleza kuwa idadi hiyo inaweza kupunguzwa kwa asilimia 24 kama kutakuwa na sheria zinazodhibiti kiwango cha ulevi kuwapo mwilini kuwa 0.02g/dl kwa madereva vijana au wasio na uzoefu wa udereva.

Kwa misingi hiyo, wadau wa usalama barabarani bado wanaiona sheria hiyo kuwa na upungufu na kuhitaji marekebisho yatakayochagiza kasi ya udhibiti wa ajali za barabarani.

Wadau hao kikiwamo kikosi cha usalama barabarani, wanasema kiwango hicho kinapaswa kushuka kufikia 0.05g/dl kwa madereva wote na 0.02g/dl BAC kwa madereva vijana na wale wanaoanza kuendesha magari, ili kuwiana na viwango vya kimataifa.

Sababu ya mabadiliko hayo inatajwa kuwa, sheria ya sasa inaruhusu kiwango kikubwa kinachotoa fursa pana ya kumuathiri dereva na kusababisha ajali za mara kwa mara.

**MOI YAREKODI ONGEZEKO**

Taasisi ya Mifupa (MOI) iliyopo kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili, ni miongoni mwa wadau wanaoguswa kwa utoaji huduma kwa majeruhi wa ajali, ingawa kwa asili na maadili yao, hawahitaji chanzo kama ulevi katika kusababisha ajali kwa wateja wao.

Lakini takwimu zilizotolewa na idara ya takwimu ya MOI zinaonesha kuwa idadi ya madereva wa magari na pikipiki waliopata ajali na kuorodheshwa MOI imeongezeka kwa asilimia 52.52 na 18.04 kwa kipindi cha kati ya 2017 na 2018.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, idadi ya madereva wa magari waliorekodiwa kupata ajali na kufikishwa MOI kwa mwaka 2018 walikuwa 754, ikiwa ni ongezeko la 396 kutoka 358 wa mwaka 2017.

Kwa upande wa madereva wa pikipiki, idadi yao kwa mwaka 2018 ilikuwa 1,813 wakati mwaka 2017, waliofikishwa MOI walikuwa 1,486.

Takwimu hiyo ni sehemu ya taarifa iliyopatikana MOI kwa waandishi wa habari wanaoshiriki mpango wa alumni wa usalama barabarani unaoratibiwa na Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), iliyotolewa mwezi uliopita.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa na Magonjwa ya Ajali wa MOI, Dk Kennedy Nchimbi, anasema baada ya serikali kupiga vita matumizi ya pombe maarufu kama 'viroba' mwaka juzi, idadi ya ajali kwa madereva waliopata ajali na kufikishwa kwenye taasisi hiyo ilipungua.

Kauli ya Dk Nchimbi inawiana na taarifa ya kitengo cha takwimu cha MOI inayoonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2016, madereva wa magari waliopata ajali na kufikishwa kwenye taasisi hiyo walikuwa 381 wakati wa pikipiki wakiwa 1,799.

"Kwa hiyo utaona kwamba baada ya 'viroba' kupigwa marufuku 2017, idadi ya madereva waliopata ajali ilishuka," anasema na kufafanua kuwa sababu hiyo inatokana na ulinganishi wa matukio na nyakati na si matokeo ya utafiti.

Dk. Nchimbi anasema madereva wanaopata ajali na kufikishwa MOI hawapimwi ili kuwabaini kama wametumia kilevi au vinginevyo.

"Wakati mwingine tunawasikia jamaa zao wanaowaleta wakielezea kwamba wamelewa, ama wakati mwingine kupitia harufu tu, tunabaini kwamba mhusika fulani alikuwa amekunywa kilevi na pengine ikachangia kupata ajali," anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Nchimbi, sehemu kubwa ya madereva wanaosadikiwa kutumia kilevi wakati wa kuendesha magari na kupata ajali, wanabainika wakati wa mwisho wa juma, hususani nyakati za usiku au wakati wa sikukuu mbalimbali.

"Lakini hata kama akisadikiwa kunuka pombe ama ndugu zake kuthibitisha kwamba dereva mhusika alitumia kilevi kabla ya kupata ajali, kitaaluma hatuandiki hivyo kwa maana itakuwa sawa na kumshutumu mgonjwa," anasema.

Kwa upande wake, takwimu kutoka kikosi cha usalama barabarani zinaonesha katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 2009, ulevi umekuwa miongoni mwa vyanzo vya ajali.

Takwimu hizo zilizotolewa na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Musilimu, zinaonesha kuwa mwaka 2010 kulikuwa na kiwango kikubwa cha ulevi kurekodiwa kwa madereva, kilipofikia 580.

Miaka mingine na kiwango chake kwenye mabano ni 2009 (221), 2011 (1717), 2012 (112), 2013 (91), 2014 (95), 2015 (66), 2016 (97), 2017 (93) na 2018 (61). Kamanda Musilimu, anasema marekebisho ya sheria hiyo yapo katika hatua nzuri baada ya kupitishwa na kikao cha makatibu wakuu wa wizara tofauti zinazohusiana na usafirishaji na uchukuzi.

"Ningependa sana kiwango hicho cha kilevi kiwe sifuri kwa hapa nchini, lakini kwa vile mwili wa binadamu una ming'emenyo inayotengeneza kiwango kidogo cha kilevi mwilini, hatuna namna," anasema.

Kwa mujibu wa Kamanda Musilimu, ulevi kwa madereva ni miongoni mwa masuala muhimu yanayotajwa kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani.

Kamanda Musilimu, anaunga mkono azma ya kuwapo mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani ili kudhibiti ulevi.

> “ Nchi mbalimbali zimejiwekea mifumo ikiwamo ya kisheria, inayolenga kudhibiti vyanzo vyote vya ajali za barabarani.

Anasema ingefaa sana sheria hiyo itamke dereva asikutwe na kiwango chochote cha kilevi kwenye damu yake, lakini kwa sababu mwili wa binadamu una ming'emenyo inayosababisha pia hali hiyo, ni vizuri ikafikia kiwango kinachotambulika kimataifa.

Sheria ya usalama barabarani inazuia matumizi ya kilevi kwa madereva, ingawa sheria yenyewe inaonyesha mapungufu ambayo ni kiwango cha juu cha ulevi katika damu cha 0.08 abc wakati Shirika la Afya Duniani (WHO) limeweka kiwango hicho kuwa ni 0.05 abc na kiwango cha 0.02 abc kwa madereva wasio na uzoefu.

Mapendekezo ya wadau wa usalama barabarani wanashauri kipengele hicho cha WHO kiwekwe kwenye maboresho ya sheria za usalama barabarani.

***Makala haya yameandikwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa alumnae wa habari za usalama barabarani unaoratibiwa na Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF). Mwandishi anapatikana kupitia simu 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@***

JIELIMISHE

## Elimu ya wakimbizi iko katika janga: UNHCR



Mtoto mkimbizi kutoka Burundi, akikamilisha kazi yake ubaoni kwenye Shule ya Msingi Jugudi katika kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu mkoani Kigoma nchini Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

ZAIDI ya nusu ya watoto wakimbizi milioni 7.1 wa umri wa kwenda shule hawaendi shule.

Hiyo ni kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), iliyotolewa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Ripoti hiyo iliyopewa jina la 'Ongezeko: Elimu ya Wakimbizi Katika Janga,' inaonyesha kuwa kadri watoto wakimbizi wanavyozidi kukua, ndivyo vikwazo vinavyowazuia kutopata elimu vinavyozidi kuwa vigumu kuvivuka.

"Ni asilimia 63 ya watoto wakimbizi ambao wanaenda shule za msingi ikilinganishwa na asilimia 91 ya kidunia. Inakuwa mbaya zaidi unapofikia kwenye ngazi ya sekondari, kwani ni asilimia 24 tu ya wakimbizi ambao hupata fursa hiyo ikilinganishwa na asilimia 84 ya kidunia," anasema Melissa Fleming, Msemaji wa Kamishna Mkuu wa UNHCR na kuongeza:

"Vikwazo vya elimu kwa wakimbizi vinazidi kuongezeka wanavyozidi kukua…kwa hiyo hili linatengeneza mzunguko usiokuwa na mwisho… usipokuwa na watoto katika sekondari, hawataweza kupata elimu ya juu hata kama ingekuwepo."

Melissa anasema kupungua kwa kasi kwenye suala la kuwaandikisha wakimbizi kati ya shule za msingi na sekondari, ni matokeo ya moja kwa moja ya upungufu wa ufadhili kwa elimu ya wakimbizi.

Anabainisha, hiyo ni kwa mujibu wa Ripoti ya UNHCR.

Kwa upande wake, Kamishna Mkuu wa Shirika hilo Filippo Grandi anasema:

"Shuleni ni mahali ambapo wakimbizi wanapatiwa fursa ya pili. Tunawaangusha wakimbizi kwa kutowapatia fursa ya kukuza stadi na maarifa wanayoyahitaji kuwekeza katika mstakabali wao."

Na ndiyo maana UNHCR imetoa wito kwa serikali, sekta binafsi, mashirika ya elimu na wachangiaji kuwasilisha michango yao ya kifedha kwa mkakati mpya unaolenga kupeleka mbele elimu ya sekondari kwa wakimbizi. **HABARI UN**

UTAFITI

# Mbinu ya kukabiliana na msongo wakati wa ujauzito yagunduliwa



Utafiti umegundua njia za kuondoa msongo wa mawazo kwa wajawazito kama mama huyu. **PICHA: MTANDAO.**

KARIBU watu milioni 450 duniani wanakabiliwa na tatizo la msongo wa mawazo, hali inayofanya wengi wao kupata matatizo ya kiafya.

Baadhi ya watu hao wanakabiliwa na wakati mgumu kutafuta matibabu, kutokana na unyanyapaa unaohusishwa na matatizo ya kiakili.

Wanawake wajawazito wako katika hatari zaidi ya kufa au kupoteza watoto wao wanapojikuta katika hali hiyo.

Nchini Kenya kwa mfano, dalili za msongo wa mawazo kama vile uchovu na kukosa usingizi wakati mwingine huchukuliwa kama dalili za ujauzito, na wakati mwingine husingiziwa kuwa ni hali inayosababishwa na uchawi.

Ukosefu wa huduma za Afya na viwango vya juu vya mzozo majumbani, vilichangia asilimia 0.5 ya vifo vya kinamama wajawazito nchini humo kwa mwaka 2015.

Msongo wa mawazo baada ya kujifungua pia unahusishwa na kuzaa mtoto mwenye uzani wa chini, mama kuwa mgonjwa au kupata matatizo wakati wa kunyonyesha.

Kenya ina wataalamu wawili pekee wa afya ya akili kwa kila watu 100,000 na wote wanapatikana maeneo ya mijini.

Hii inamaanisha kuwa baadhi ya maeneo ya vijijini ambako wanaishi mamilioni ya watu hawana mtaalamu wa magonjwa ya akili.

Inakadiriwa kuwa asilimia 75 ya watu walio na matatizo ya kiakili wanaoishi katika maeneo vijijini, hawana uwezo wa kupata matibabu.

Hali inayowafanya kutafuta msaada kwa waganga wa kienyeji na wafanyakazi wengine wa afya, badala ya wataalamu waliohitimu.

Watafiti wamegundua kuwa ipo haja ya kuwapa mafunzo zaidi kundi hilo la watu katika jamii kwani itasaidia kupunguza idadi ya watu walio na matatizo ya kiakili wasio na uwezo wa kupata matibabu.

Ili kuimarisha matokeo ya utafiti huo, wakunga wa kienyeji walijumuishwa katika mafunzo hayo ili kuwabaini kinamama wajawazito walio na msongo wa mawazo.

Zaidi ya wanawake wajawazito 1,700 walihusishwa katika utafiti huo uliofanywa na Shirika la utafiti wa afya ya akili barani Afrika.

Utafiti ulifanyika katika eneo la Kusini Mashariki mwa Kenya, uliangazia zaidi maeneo yanayokaliwa na watu maskini yasiyokuwa na mtaalamu yeyote wa masuala ya Kisaikolojia.

### MZOZO WA NYUMBANI

Matokeo ya uchunguzi huo yalikuwa ya kushangaza.

Robo ya kinamama walioshirikishwa katika utafiti huo walikutwa na matatizo kidogo ya usumbufu wa akili.

Theluthi tatu walinyanyaswa na wapenzi au waume zao iwe ni kingono au kisaikolojia.

Karibu asilimia 60 ya kinamama hao walikutwa na msongo wa mawazo na kupewa matibabu na wakunga wa jadi kulingana na mwongozo wa tiba wa Shirika la Afya Duniani (WHO) uliotolewa kwa watu wasiokua wataalamu wa matibabu.

Kinamama hao walikuwa na umri wa miaka 26 huku wengine walioshirikishwa katika utafiti huo wakiwa na umri wa kati ya miaka 12 na 24.

Mmoja wao alikuwa, Ndanu ambaye alikutwa na tatizo la kiakili.

Ndanu anasema: "Laiti kama mpango huo haungekuwapo na nisingepata huduma ya mkunga wangu, ningelimpoteza mwanangu kwa sababu sidhani kama ningelienda kliniki."

"Mkunga alinishauri nitunze afya yangu na ya mtoto wangu kwa kuhakikisha nafika kliniki kama ilivyopangwa... aliniahidi kuwa mlango wake upo wazi wakati wowote nitakapojihisi kusema naye," anaongeza. **BBC**

JE, WAJUA?

# Wakati moto ukiiteketaza Amazon, msitu Bonde la Kongo unawaka

MOTO wa Amazon umeanza kusababisha matatizo ya kupumua kwa wananchi wa Brazil, huku shirika la kulinda mazingira la Greenpeace likionya kwamba moto pia unaharibu msitu wa Bonde la Kongo barani Afrika.

Serikali ya Jimbo la Amazon la Rondonia, inaonya kwamba moshi unaotokana na moto huo unaweza kuchafua sana hewa na kuweka maisha ya wengi hatarini.

Na matatizo ya kiafya tayari yameshaanza kujitokeza katika Jimbo hilo.

Moshi huo umeshaanza kusababisha wasiwasi kwa wananchi wa Brazil wanaosema matatizo ya kupumua hasa kwa watoto pia yanaongezeka kadri moto huo unavyoteketeza eneo la msitu huo.

Idadi ya watu waliotibiwa kutokana na matatizo ya kupumua imeongezeka katika siku za karibuni kwenye Hospitali ya watoto ya Jimbo la Rondonia.

Lakini licha ya hayo, suala la moto wa Amazon limetawalia zaidi na mvutano na majibizano ya maneno kati ya Rais wa Brazil, Jair Bolsonaro na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron.

Awali Bolsonaro alidai kwamba Macron alimtusi na hatopokea msaada wa mataifa tajiri duniani yanayounda kundi la G7 hadi Macron amuombe msamaha.

Lakini alibadilisha kauli yake Jumamosi iliyopita kupitia kwa msemaji wake, Otavio Rego Barros, na kusema Brazil iko tayari kupokea msaada wa kigeni wa kusaidia kuzima moto katika msitu wa Amazon.

"Serikali ya Brazil kupitia Rais Bolsonaro iko tayari kupokea msaada wa kigeni, lakini msaada huo usiikuke uhuru wa nchi na Brazil ndiyo itaamua jinsi ya kuzitumia fedha hizo," anasema Barros.

Katika mkutano ya kilele wa kundi la mataifa yaliyoendelea sana katika sekta ya viwanda G7, kuliahidiwa msaada wa kifedha wa dola milioni 20, mbali na zilizoahidiwa na Uingereza ambazo ni dola milioni 12 na nyingine dola milioni 11 kutoka Canada.

Hata hivyo, Rais Bolsonaro anatilia mashaka msaada huo akidai kuwa ni njama ya kutaka kutumia rasilimali za msitu wa Amazon pamoja na kudhoofisha ukuaji wa maendeleo ya Brazil.

### MSITU WA BONDE LA KONGO PIA WATEKETEZWA KWA MOTO

Wakati hayo yakijiri, shirika la kimataifa la ulinzi wa mazingira Greenpeace limezitaka serikali za mataifa yaliyo katika Bonde la Kongo kuchukua hatua zaidi kupambana na moto wa msitu wa Afrika ya Kati, katika kipindi ambacho ulimwengu umeelekeza macho yake kwenye moto unaoteketeza msitu wa mvua wa Amazon huko Brazil.

Msitu ya Bonde la Kongo, sehemu inayofunika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Gabon, Congo-Brazzaville na Cameroon unashika nafasi ya pili duniani baada ya msitu wa Amazon.

Kama ilivyo kwa msitu wa Amazon, msitu wa bonde la Kongo unachangia kusafisha hewa chafu ya kaboni kwa kiasi kikubwa na ni njia muhimu kwa mujibu wa wataalamu ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi. **DW**



Umande katika msitu wa mvua Bonde la Congo Magharibi. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

**NA MICHAEL ENEZA**

# Vyuo vikuu vinapotumia Elimu ya Kujitegemea kuwavusha vijana

MOJA ya maajabu katika mabadiliko ya mfumo na matazamio ya elimu tangu uhuru ni jinsi elimu ilivyoshuka daraja ikawa siyo jambo la kawaida, ila hata la kudharauliwa.

Kwa upande fulani taifa lilijitakia lenyewe hali hiyo, na yaliyobaki yalitokea kutokana na yale ya kwanza, bila kutazamia, kwani katika kipindi cha uhuru kulikuwa na juhudi ya kujitambulisha.

Kwa upande wa Mwalimu Julius Nyerere na 'wazungumzaji' katika vyombo vya habari - ba 'baba kabwela,' yaani mkulima (maskini) kijijini au mkazi 'hohehahe' mjini.

Rais Nyerere akazuia kupandisha ovyo mishahara serikalini, kuunda matabaka.

Ni baada ya Azimio la Arusha (1967) ambako utambulisho huu ulikolea, ukachukua sura kama ya China wakati huo, iliyokuwa imegubikwa na 'mapinduzi ya kitamaduni.'

Ila hayakuwa ya kitamaduni bali ya kiitikadi, kufuta hisia za ubepari, mali binafsi, uhuru wa kujieleza, kuanzisha shughuli ya kipato, n.k. ndani ya Chama cha Kikomunisti.

Azimio lilikuwa ni mapinduzi ya utamaduni serikalini wakati wa uhuru, kwani kabla ya hapo ilikuwa Rais Nyerere anawabana viongozi kama mtawala, lakini baada ya hapo akapewa rungu la kiitikadi, yaani 'miiko ya uongozi.' Ikawa ndiyo kielelezo halisi cha Ujamaa.

Moja ya tunu za Azimio ilikuwa ni 'kukataa fedha kama msingi wa maendeleo,' dhana ambayo ilitoa mwanya mpana wa kupinga kuwapo au ushawishi wa ubepari duniani, kwani huku Afrika ulikuwa pia na sura ya ubeberu, ukoloni mkongwe au 'mamboleo' (nchi inakuwa huru halafu kila kitu bado kinaamuliwa nje).

Ndilo jambo Nyerere alilolikataa ili kuendeleza azma yake ya kuunga mkono mapambano ya ukombozi Kusini mwa Afrika, akiwa yuko 'peke yake' baada ya kupinduliwa kiongozi wa Ghana Dk. Kwame Nkrumah mwaka uliotangulia. Wengine walifuata baadaye, au walifikia uhuru kwa juhudi hizo.

Akifafanua itikadi ya Ujamaa, Mwalimu alichambua maeneo mawili ya maisha ya jamii kwa kina akitaka yabadilike na kuchukua sura nyingine, yaani elimu na maisha vijijini.

Vijitabu viwili alivyoviandika kuhusu maeneo hayo mawili vilisomwa kote duniani na bado ushawishi wake upo, kwani dunia ya viwanda tangu mwanzo wa karne ya 19 imetafuta njia ya kuondoa hitilafu za kina katika jamii, ambako nchi inakuwa na 'mabilionea 10 na mafukara milioni 10.'

Nyakati hizo 'ubilionea' haukuwepo ila umilionea, kwani milioni ya wakati huu si ajabu ni sawa na elfu kumi ya wakati huo, wakati dola ya Marekani iliuzwa shilingi saba, na sasa ni karibu na Sh. 2,500 kuonyesha kuzidisha kwa mara 80, hivi.




Chuo Kikuu cha Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

Kwa upande wa insha hiyo kuhusu elimu, Mwalimu alijaribu kutafuta njia ya kuondoa hulka tegemezi ya kupata ajira ofisini kama jambo la msingi kuweza kufaulu katika maisha.

Alitoa taswira ya mfumo wa elimu unaojikita katika kufanya kazi kwa mikono na kufahamu stadi zinazoendana na kumudu maisha kwa njia hiyo kwa kijana anayemaliza shule ya msingi.

Alichovuna Nyerere ni wakuu wa shule kutoa mfano kwa kulima mashamba makubwa kiasi, na wanafunzi kuchoshwa kiakili, elimu ikaanza kushuka lakini kwa vile ni yeye mwenyewe alitoa mkakati huo, hakutofautiana nao, akawapongeza, suala likaisha.

Ila suala la kujitambulisha na 'baba kabwela' sasa likachukua mpangilio halisi wa kitamaduni, ikawa ni fedheha mtu (mwanafunzi wa shule au chuo) kuongea Kiingereza nje ya shughuli za kielimu, na hasa ndani ya chumba cha darasa au ofisini kwa mwalimu.

Tabia ya kuongeaongea Kiingereza ikawa ni moja ya 'mabaki ya ukoloni,' na uzalendo ukawa ni kuongea lugha yetu ya Kiswahili, na hatua kwa hatua uwezo wa kuongea lugha hiyo ukapungua. Kwingineko Afrika Mashariki wananchi wa kawaida huitumia sana.

Ndiyo msingi wa Kiswahili kuwa lugha pendwa, na jinsi Kiswahili kilivyokua ndivyo Kiingereza kilivyoendelea kufutika hatua kwa hatua, kiasi kwamba hivi sasa hata vyuo vikuu vinajiuliza mara mbili mbili kama waitishe mhadhara wa kitaaluma unaotumia Kiingereza.

Na ukiwepo ni wa 'chemba' ambako waalimu (wahadhiri) ndiyo wanaohusika ili wanafunzi wasikifedheheshe chuo kwa lugha mbovu, na ndiyo mazingira yanayozuia kuwekeza katika viwanda vya teknolojia nyeti kwani kupata wafanyakazi wa mishahara ya kawaida wenye Kiingereza safi ni tatizo.

Si chanzo halisi ajira kupungua ila inachangia.

Ni katika mazingira haya ambako vyuo vinatafuta njia za kutumia Elimu ya Kujitegemea kuwezesha vijana kupata mwanga wa nini cha kufanya baada ya shule, siyo ile ya msingi bali ya vyuo na vyuo vikuu.

Tena cha kushangaza ni kuwa kwa watu wa kada za chini au 'wasiosoma' tatizo la ajira si kubwa kiasi hicho, kwani wanapachikwa hapa na pale kwa urahisi, akiwa anajua ufundi wa aina mbalimbali, ambao hasa ndiyo ulilengwa na Elimu ya Kujitegemea.

Shida siyo kuitumia fikra hiyo kusomea ufundi na kupata kazi kwani elimu yao hailingani na kazi hizo, ila kuitumia nyumbani apate riziki kwa shughuli ya ndani.

Mwelekeo wa sasa wa kuunda vikundi vya kilimo ni wa kubahatisha, kwani jambo la msingi baada ya kumaliza chuo ni kuanza maisha, ambayo ni pamoja na maskani ya familia.

Inatakiwa mwelekeo wa kuanzisha shughuli za kawaida za kipato usilenge kilimo cha biashara bali cha nyumbani kisichohitaji eneo kubwa, na mipangilio ya manispaa au miji midogo kutoka maeneo hata kwa mpangilio wa uwekezaji ili ziendelezwe kwa maana ya kutengeneza nafasi ya kulima mboga kwa mitungi, na kufuga kuku, bata, n.k.

"Ni katika mazingira haya ambako vyuo vinatafuta njia za kutumia Elimu ya Kujitegemea kuwezesha vijana kupata mwanga wa nini cha kufanya baada ya shule, siyo ile ya msingi bali ya vyuo na vyuo vikuu.

Ni shughuli ambayo kwanza inalenga kupata sehemu ya chakula, na ziada iuzwe mahitaji yatimie.

Njia hiyo inaweza kumpa kila kijana shughuli ya kufanya katika maskani (kwa mfano kundi la vijana wasio na familia kulima bustani au kumiliki 'fremu' kadhaa za kilimo cha mboga kwa mitungi na nyingine za kuku wa mayai, n.k.

Wengi zaidi watapendelea wawe na shughuli yao wenyewe, ambayo ina maana mtu anapata chumba cha kukaa na eneo la kupangisha ili kuendeleza shughuli zinazohakikisha kuwa sehemu isiyo ndogo ya mahitaji ya ndani inapatikana kwa kujituma wao wenyewe.

Si mpaka auze kitu apate kipato naye anunue, au ajiweke barabarani mtu akitaka 'deiwaka' ndipo amchukue, au alale tu.

Tatizo la mfumo uliopo wa uzalishaji mali ni kuwa unalenga bidhaa, na maskani ya watu ni mahali tu pa kulala na kuamka, kufua na kupiga pasi na labda kulea watoto lakini si pa kupatia kipato au kujihakikishia mahitaji ya msingi ya chakula.

Kubadili mtindo huo ni kama kuleta vijiji mijini, kwani kule hakuna mtu 'asiye na kazi' na kinachoweza kuwavuruga ni mabadiliko ya hali ya hewa mvua inapokosekana, mazao kuharibiwa na wadudu au kukosa soko endapo mavuno ni makubwa msimu huo.

Hivyo mipango miji sasa inatakiwa ibadilike itenge maeneo kila mahali kujengwe ghorofa za kupangisha watu kwa fedha kidogo, walime mbogamboga na kufuga kuku au bata ili wapate mahitaji ya msingi nje ya ajira, biashara.



WADAU

SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

BAADHI ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wamelalamika kuhusu kile wanachokiita uonevu katika marejesho ya mikopo hiyo, na hasa tozo ya asilimia sita ya kulinda thamani ya fedha, asilimia moja ya ada ya uendeshaji na makato ya adhabu ya asilimia 10 wanayotozwa na Bodi (HESLB).



**MUSA AMOSI (MTUMISHI CHUO CHA MIPANGO, MWANZA)**

BODI hii imekuwa kimbilio kwa wanafunzi wanaotoka katika familia fukara au wanafunzi yatima lakini pia hata familia za kawaida. Kulingana na marekebisho ya sheria ya marejesho ya mkopo, huwa unaanza kurejeshwa baada ya miezi 24, mwanafunzi akishahitimu masomo yake.

Riba ya mkopo ni asilimia sita kwa kila mwaka ambao mkopo utakuwa ukirejeshwa. Kwenye mkopo ghafi bodi inakata asilimia 15 ya mshahara au pato ghafi la kila mwezi kutoka kwa mnufaika wa mkopo. Ila pia mnufaika kwa hiari yake baada ya kuwasiliana na bodi anaweza kulipa zaidi ya hizo zilizotajwa kwenye utaratibu wa kawaida ili awahi kumaliza kulipa deni.

Tatizo lililopo si ukubwa wala riba inayotozwa katika deni la mkopo bali ni ufinyu wa uelewa miongoni mwa wanufaika. Kwanza baadhi ya wanufaika wa mikopo wanatumia sehemu ya mikopo hiyo kwa mambo mengine nje ya malengo hivyo baadaye wanaona kama vile wakati wa marejesho wanaonewa.

Pia baadhi ya wanufaika wa mikopo hawawezi kutofautisha kati ya mkopo na msaada wa masomo, badala yake wanadhani ile pesa ni ya msaada wa serikali wakidhani haitarejeshwa. Katika hili panatakiwa pawapo na washauri wa mikopo kwa kijana anayetarajia kuchukua mkopo ili mwisho wa masomo ajue kabisa kwamba pesa aliyochukua anatakiwa airejeshe na riba yake.

Tatizo hili ni kubwa zaidi, kwani unaweza ukakuta kijana familia ina uwezo wa wastani na imeweza kumsomesha bila tatizo kwa gharama zao hadi diploma/stashahada.



**JUSTA MWAITUKA (MKURUGENZI WA KIWOHEDE TANZANIA)**

MAONI yangu ni kwamba utaratibu na namna ya kuwalipisha lazima ubadilishwe, kwa sababu inaonekana mfumo wa ukokotoaji wa riba umewekwa kibiashara zaidi.

Ni vyema riba iwekwe mara moja tu sio kila mwaka kama inavyofanyika sasa, huko ni kuwaweka wanafunzi kwenye kitanzi cha maisha magumu na msongo wa mawazo maisha yao yote.

Hali hii inaweza kuwa inasababisha kuwapo kwa wadaiwa sugu wanaotajwa na bodi hiyo. Kama mtu atakuwa ameajiriwa serikalini au sekta binafsi, kwa sababu mtu anapotaka kuajiriwa ni lazima apeleke vyeti vyake, vinavyomuonyesha ana elimu gani na amesoma wapi.

Kama ni chuo ni lazima itajulikana, iwapo atakuwa amepata mkopo au hakupata pia itakuwa wazi na hasa kama kutakuwa na utaratibu wa vyuo kupeleka majina ya wanafunzi waliohitimu ambao walipewa mkopo ili iwe rahisi kukatwa fedha na kurudishwa bodi.

Kimsingi uwezekano wa kuwapata wanafunzi wote waliokopa fedha upo, lakini tatizo ni hizo ada, tozo na riba, ambavyo kama nilivyosema kuna haja ya kubadilisha mfumo huo, ambao kwa kweli unaonekana uko kibiashara zaidi hadi kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wakopaji, ambao sasa wanaiona bodi kama adui wao.

Niishauri bodi kwamba ukokotoaji wa riba utazamwe upya ili kuhakikisha wadaiwa wanalipa mikopo yao kwa uhuru, vinginevyo kila siku tutaendelea kusikia malalamiko yasiyo na mwisho kutoka kwa wadaiwa kwenda kwenye bodi.



**LUCAS MSIMBETE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MIKOPO inayotolewa na Bodi ya Elimu ya Juu (HESLB) kwa ajili ya elimu ya juu nia yake bila shaka ni kuwawezesha Watanzania wengi hususan vijana kupata elimu ya chuo kikuu.

Changamoto inayojitokeza kwa wanafunzi (wakopeshwaji) juu ya marejesho ya mkopo inapaswa kutazamwa katika picha kubwa ya mchakato wa mkopo kuanzia utoaji, mikataba na urejeshwaji.

Katika urejeshaji wa mkopo, riba na tozo inabidi kutazamwa kwa makini kwanza.


Ni suala la makubaliano, yaani mkataba wa mkopo na mchakato wa urejeshaji. Makubaliano ya mkataba wa mkopo yanapaswa kuainisha jinsi ya urejeshaji na tozo na ukomo wake.

Inafaa ikiwa tozo inaweza kulenga wakopaji, ambao walishindwa kurejesha mikopo kwa wakati na kwa makusudi ikiwa wana sifa za kufanya hivyo.

Kwa hiyo jambo la msingi katika suala zima za urejeshwaji ni vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba na uhalisia.

Kwa mfano ingefaa ikiwa mkopaji ambaye hana sifa ya kurejesha kwa maana ya kipato kuwekewa taratibu, ambao utapunguza mzigo wa riba na tozo.

Mikataba ya mkopo pia inapaswa kupitiwa ili kuongeza vipengele mahsusi vyenye kuweka taratibu kulingana na changamoto halisi zinazojitokeza sasa kwa wakopaji.



**VICTORIA JOHN (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIJUI kama ipo siku mkakati huu utafanikiwa, kwasababu kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya kuwapata wanufaika wa mikopo, ambao hawaingii kwenye sekta rasmi ya ajira.

Ninatambua juhudi zinazofanywa na bodi hadi kufikia kushirikisha TRA na Brela kupata taarifa zao. Hii ni kwa sababu wale ambao hawako katika mfumo rasmi sio kwamba ni maskini hawawezi kulipa, bali tatizo ni namna ya kuwapata.

Hivyo uamuzi wa bodi kutumia hata TRA na Brela kupata taarifa ni mzuri, kwani kuna uwezekano mkubwa wa kujua kama wamefungua kampuni au wana leseni ya biashara na wako wapi kwa sasa.

Inawezekana wapo wahitimu ambao wana maisha mazuri tu, lakini hawajulikani walipo na wanafanya nini, kwasababu hawapo kwenye ajira rasmi.

Nikirudi kwenye swali lako la msingi, suala la penati, ada na tozo kwa wakopaji vinaweza kuwa kikwazo kikubwa kwao kurejesha mikopo.

Umefika wakati sasa bodi ingeangalia njia mbadala ambayo kwa namna moja au nyingine itaweza kuondoa kero hiyo inayosumbua wahitimu wengi.

Ni kweli inawezekana wapo walioajiriwa, waliojiajiri na wengine bado, lakini suala la msingi ni kwamba wanatakiwa kurejesha kile walichokopeshwa wakati wakisoma, ili kisaidie wengine wanaojiunga na elimu ya juu.



**GODSON MHEMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

BINAFSI ninakuwa na mashaka kidogo kuhusu malalamiko ya wanufaika wa mikopo, yawezekaana kukawa na sababu nyingi zinazochangia baadhi ya wanufaika wa mikopo kushindwa kuirejesha kwa wakati.

Sababu ya kusema hivyo ni kwamba miaka ya nyuma kila tulikuwa tukisikia polisi wakitumia mabomu ya machozi kuwatawanya wanafunzi wa vyuo vikuu wanapogoma au kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), kufuatilia mikopo yao.

Matukio haya yalikuwa ni ya kawaida kwenye utawala uliopita, lakini sasa ni kama yamepungua, ila kilichopo bodi sasa kuwatafuta wanafunzi waliopewa mikopo, ambao tayari walishamaliza vyuo ili wairejeshe.

Mimi ninadhani kwamba wapo walioamua kulipiza kisasi cha kusoteshwa na bodi hiyo enzi hizo walipokuwa wakisoma ili nayo ione machungu ambayo walikuwa wakiyapata yakiwamo ya kupigwa mabomu wakati wakitafuta haki yao.

Lakini suala kwamba tozo na penati zimezidi, sidhani kama kuna ukweli ndani yake na kama ni kweli, basi kuna haja ya kuandaa utaratibu mzuri ambao utawafanya wahitimu wote walipe mikopo yao bila manung'uniko ili fedha hizo zitumiwe na wanafunzi wengine wanaojiunga na vyuo. Kwa kawaida mtu anapodaiwa anatakiwa kufuatiliwa pale anapolegalega, kwani si rahisi ajipeleke mwenyewe alipe.

# RC aingia mitaani kukamata Bajaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameungana na Jeshi la Polisi mtaani kufanya operesheni ya kuwashughulikia madereva wa pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la 'Bajaji' wasiokuwa na leseni za udereva ili kupunguza makosa ya barabarani.

Operesheni hiyo ilifanyika jana asubuhi katika vituo mbalimbali vya bajaji jijini Mbeya na idadi kubwa ya madereva hao walibainika kufanya kazi hiyo bila kuwa na leseni, jkambo ambalo limeelezwa kuwa ni hatari kwa watumiaji wa vyombo hivyo.

Akizungumza wakati wa operesheni hiyo, Chalamila alisema aliamua kuungana na polisi baada ya kupokea malalamiko ya madereva hao wakidai wanaonewa na jeshi hilo kwa kuwakamata bila makosa.

Chalamila alisema alishangaa kuona wengi wao wanaendesha vyombo hivyo wakiwa hawana leseni, huku wakijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Nina malalamiko yenu mengi sana ofsini kwangu ambayo mnalilalamikia Jeshi la Polisi kuwa linawaonea. Nimeona nishiriki kwenye ukaguzi huu ili nijiridhishe kabla ya kuanza kuchukua hatua zingine lakini ninachokishuhudia ni tofauti na malalamiko yenu," alisema Chalamila.

Alisema katika opereshani hiyo aliwakagua zaidi ya madereva 120, lakini kati yao ni 10 pekee ambao walionekana wakimiliki leseni za udereva na wengine wote wakiwa hawana.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kwa sasa wanaendelea kukagua na kutoa elimu kwa madereva hao, ili kuhakikisha wanasomea kazi hiyo na kuwa na leseni ili waifanye kihalali.

# Viwanda vya mpunga vyalia uhaba malighafi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAMILIKI wa viwanda vya kusindika mpunga Mbarali mkoani Mbeya, wamesema kiwango cha zao hilo kinachozalishwa na wakulima wilayani humo hakikidhi mahitaji ya viwanda vyao kwa ajili ya kuviwezesha kufanya kazi katika kipindi chote cha mwaka.

Mwenyekiti wa wamiliki wa viwanda hivyo, Venance Mgeni, alisema jana kuwa kiwanda cha aina yoyote kinahitaji kuwa na uhakika wa malighafi, lakini viwanda vya Mbarali vinategemea mpunga kama malighafi kutoka kwa wakulima wadogo ambao nao hawazalishi kwa tija.

Pia alisema kuna mashamba mengi ndani ya wilaya hiyo ambayo yanafaa kwa kilimo cha mpunga, lakini hayalimwi bila sababu.

Mgeni aliiomba serikali kufanya sensa ya mashamba ili kubaini yasiyolimwa na kuwagawia wamiliki wa viwanda ili washiriki kuzalisha mpunga kwa ajili ya viwanda vyao.

"Tunaiomba serikali ifanye sensa ya mashamba kwa ajili ya kuainisha mashamba ambayo hayalimwi bila sababu za msingi na wakishajua wayagawe kwa wamiliki wa viwanda ili na wao wazalishe na kuwa na uhakika wa malighafi za viwanda vyao," alisema Mgeni.

Alisema kutokana na uhaba wa malighafi, viwanda vingi vinafanya kazi kwa msimu kutokana na uhaba wa malighafi, hali ambayo inasababisha uendeshaji kuwa mgumu na kuwakosesha wananchi ajira zenye uhakika.

"Ukosefu wa mpunga wa kutosha kwa ajili ya viwanda vyetu unasababisha tufanye kazi kwa msimu. Sasa ule muda ambao tunafunga viwanda kwa kukosa malighafi tunalazimika kuzuia ajira za baadhi ya wafanyakazi ili kuepuka hasara," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema mavuno ya mpunga katika msimu uliopita hayakuwa mazuri kutokana na uhaba wa mvua, ingawa mashamba yaliyolimwa yalivuka lengo la makisio ya halmashauri ya wilaya hiyo.

Mfune alisema makisio ya halmashauri hiyo yalikuwa kulima hekta 125,388 za mpunga na kuvuna tani 555,720, lakini kiwango hicho hakikufikiwa kutokana na mtawanyiko wa mvua kutokuwa mzuri kama walivyotarajia.

"Kwenye kulima tulivuka lengo maana tulilima hekta 129,912 lakini kutokana na changamoto ya mvua, tulishindwa kufikia lengo la mavuno kwani tulivuna tani 334,214.36 pekee," alisema Mfune.

Alisema baadhi ya mashamba ya wilaya hiyo yanategemea kilimo cha umwagiliaji lakini kutokana na mvua kutonyesha kwa kiwango kinachotakiwa, mito nayo haikuwa na maji ya kutosha.

Aliwataka wamiliki wa viwanda kuwa na umoja na kushirikiana katika kutatua changamoto zinazowakabili kwenye uzalishaji wao na kwamba serikali itaendelea kushirikiana nao katika kutatua changamoto zao.



Baadhi ya wananchi wa Kata ya Ruanda, wakibomoa majengo chakavu tayari kwa kuanza ujenzi wa madarasa nane na ofisi katika Shule ya Msingi Weru 2, iliyopo wilayani Mbozi mkoani Songwe jana. **PICHA: IBRAHIM YASSIN**

# Waomba punguzo bei mbegu ya maharage

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wadogo wa maharage Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameiomba serikali kupunguza bei ya mbegu ya zao hilo kwa lengo la kuwasaidia kumudu kuinunua na kuzalisha kwa tija.

Wakizungumza kwenye kikao cha wadau wa maharage Kanda ya Nyanda ya Juu Kusini kilichofanyika mwishoni mwa wiki mjini hapa, baadhi ya wakulima hao walisema bei kwa sasa ni Sh. 4,000 kwa kilo ambayo ni kubwa na hawawezi kuimudu kutokana na hali duni ya kipato chao.

Rashid Babuya, mkulima wa maharage mkoani Mbeya alisema kutokana na bei za mbegu kuwa juu, wakulima wadogo wanalazimika kupanda mbegu za kienyeji ambazo haziwapatii mavuno mazuri.

"Tunatamani sana na sisi wakulima wadogo tununue na kupanda mbegu bora, lakini hali yetu ya kipato hatuwezeshi kumudu kuzinunua, hivyo tunaiomba serikali itusaidie kupunguza bei hiyo ili na sisi tuzipate na hatimaye tuweze kuzalisha mazao bora na mengi," alisema Babuya.

Alisema wakulima wengi wadogo wanapata hasara kwa kupanda mbegu za kienyeji kwa vile wanatumia gharama kubwa kuhudumia shamba lakini wanaambulia mavuno kidogo, hali ambayo inachangia kuwaongezea umaskini.

Babuya aliongeza kuwa serikali inaweza kuweka ruzuku kwenye mbegu za maharage ili mkulima azipate kwa bei nzuri japo kwa miaka michache ili kuwawezesha kupata faida na hatimaye kuwa na uwezo wa kununua kwa bei halali ya mbegu hizo.

Ofisa Kilimo wa Manispaa ya Iringa, Lucy Nyalu, alisema kutokana na wakulima wengi kushindwa kumudu bei ya mbegu bora za maharage, wanalazimika kwenda kununua maharage sokoni ambayo ni maalum kwa ajili ya chakula na kwenda kupanda mashambani kama mbegu.

Alisema hali hiyo inawafanya wakulima wengi kupata mavuno kidogo licha ya kwamba wanatumia gharama kubwa kuhudumia shamba, hivyo kujikuta wanapata hasara badala ya faida.

"Wakulima wengi wanashindwa kununua mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na badala yake wanakwenda kununua chakula sokoni na kwenda kukipanda shambani wakidhani ni mbegu. Matokeo yake wanaishia kupata hasara hata wakihudumia vizuri mashamba yao," alisema Nyalu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema bei ya mbegu bora za maharage bado ni za kawaida ikilinganishwa na faida ambayo wakulima wanaweza kuipata endapo wataitumia.

Alisema endapo wakulima watajitahidi kununua mbegu hizo, watapata faida maradufu kuliko kutumia mbegu za kienyeji ambazo haziwezi kuwaletea tija.





# Watakiwa kutumia fursa utalii wa ndani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wametakiwa kutumia fursa ya uzinduzi wa mpango maalum wa safari za utalii wa ndani jijini hapa, ili kujifunza mambo mbalimbali yaliyomo ndani ya hifadhi.

Mwakilishi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Ahmed Mbugi, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mpango maalum wa safari za utalii zijulikakanazo kama 'Dodoma City Tour' zinazotarajiwa kufanyika kila mwezi.

Mbugi alisema mpango wa safari za utalii wa ndani za Jiji la Dodoma ni kwa ajili ya wageni wote wanaotembelea mkoani hapa, lakini wenyeji nao wanapaswa kutumia fursa hiyo kujifunza mambo mbalimbali.

Alisema kampuni ya Mbuyu Travel kwa kushirikiana na Tanapa zimekubaliana kufanya safari za utalii wa ndani kila mwisho wa mwezi kuanzia mwezi huu.

"Naomba wakazi wa Dodoma tumieni fursa hii kwa ajili ya kwenda kuona vivutio vilivyomo ndani ya hifadhi," alisema Mbugi.

Alisema hakuna sababu ya wao kubaki nyuma na kuachia wageni pekee kutembelea vivutio hivyo na kwamba kinachotakiwa ni kujitokeza kwa wingi kwa sababu gharama ni ndogo tofauti na ilivyo katika siku za kawaida.

Mbugi alisema Mbuyu Travel kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika kitengo cha uwekezaji, iko mstari wa mbele kuhakikisha sekta ya utalii inakuwa mkoani hapa ikiwamo watu kupata uwelewa juu ya utalii wa ndani.

Alisema Tanapa kwa kushirikiana na Mbuyu Travel zimekubaliana kufanya safari za kila mwezi za utalii wa ndani jambo ambalo litaongeza ufahamu na uwelewa wa utalii kwa wakazi wa Dodoma.

Alitaja baadhi ya vivutio ambavyo Dodoma City itakuwa ikienda ni pamoja Swagaswaga, Tarangire, Kondoa Irangi na jengo la boma Dodoma.

Mbali na sehemu hizo, pia alisema wamepanga kutembelea Kongwa katika makumbusho ya wapigania uhuru, utalii wa sokoni, mashamba ya zabibu, utalii wa kitamaduni na Mbuyuni.

Mratibu wa maonyesho ya bidhaa zinazotengenezwa na Watanzania ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mbuyu Travel, Japhet Jackson, alisema mpango huo wa safari ni muhimu kwa wakazi wa Dodoma na jamii kwa ujumla kutokana na ukweli kwamba utasaidia watu wengi kujua vivutio vilivyomo ndani ya nchi.

Alisema utalii wa ndani utawapa watu uelewa na ujuzi wa kazi za asili zikiwamo bidhaa na vyakula vya asili ambavyo vinafanywa na jamii ya Kitanzania.



Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Idda Siriwa (kushoto), akitoa elimu kwa wanavikundi na wananchi wilayani humo juzi, wakati akiwahamasisha kuepukana na upokeaji wa rushwa kwa wagombea katika kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchi nzima mwezi Oktoba mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC aagiza utaratibu usimamizi miradi TSCP

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza uongozi wa Jiji la Dodoma kuandaa utaratibu wa namna ya kusimamia na kuendesha miradi ya uendelezaji miji mkakati (TSCP) ambayo iko mbioni kukamilika.

Miradi hiyo ni pamoja na soko kuu, kituo cha kisasa cha mabasi na eneo la kupumzikia ambayo kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi uliopo, inatarajiwa kukamilika Desemba 30, mwaka huu.

Akizungumza jana baada ya kukagua ujenzi wa miradi hiyo, Dk. Mahenge alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi huo ambao kwa sasa umefikia asilimia 75.

"Uwekezaji huu ni mkubwa, hivyo ni lazima jiji lianze kuandaa namna ya kusimamia matumizi yake. Sisi Watanzania usipoweka vizuri utaratibu soko hili utashangaa linachafuka. Ningeshauri muanze kuratibu leo," alisema.

Alimpongeza mkandarasi, kampuni ya Mohammed Builders, ambaye anajenga miradi mitatu kwa wakati mmoja na yote iko katika ubora unaotakiwa.

"Kwa kweli nimeridhika, naona faraja kufanya kazi na mkuu wa wilaya na mkurugenzi wake wanaosimamia vizuri miradi hii," alisema.

Aidha, aliwataka kuheshimu maeneo ya wazi yaliyopo kwa kuyatambua, kuyaorodhesha na kuwasilisha orodha hiyo ofisini kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma ili kutambua maeneo hayo kama yapo.

"Lazima tuheshimu maeneo ya wazi, ipatikane orodha ya sehemu zote katika jiji hili, na kusiwe na mtu anayevamia maeneo hayo yaliyotengwa, kama kuna mtu amejenga ajiandae kuondoka," alisema.

Akitoa maelezo ya miradi hiyo, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 77.8.

"Miradi hii inaendana na hadhi ya makao makuu na ni miradi bora kabisa, Dodoma tunayoijenga sasa baada ya miaka 2 au 3 itakuwa ni eneo ambalo mtu atataka kuja kutembea na kutalii, alisema Kunambi."

# Wajawazito wahimizwa kuhudhuria kliniki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAJAWAZITO wametakiwa kuhudhuria kliniki kwa wakati ili kupata elimu juu ya lishe wanayotakiwa kupata katika kipindi cha ujauzito na wanapojifungua.

Akizungumza na Nipashe jana, daktari wa watoto kutoka Kituo cha Afya cha Makole jijini hapa, Janeth Usiri, alisema moja ya mambo yanayofundishwa wakati wa kliniki ni aina ya vyakula ambavyo mjamzito anatakiwa kula ambavyo vinasaidia kujenga mfumo wa mtoto kiakili kwenye hatua ya awali hadi anapozaliwa.

Dk. Usiri alisema kuna aina ya madini yanasaidia kurejesha mfumo wa mtoto kiakili ambayo hutokana na baadhi ya vyakula vikiwamo vidonge ambavyo hupewa wajawazito wanapohudhuria kliniki.

Mtaalamu huyo alisema kutokana na umuhimu huo, ni vyema mjamzito kuhudhuria kliniki ili afundishwe juu ya faida za mahudhurio ya kliniki.

Alisema wajawazito wengi wamekuwa na mwamko mdogo wa kuanza kliniki katika hatua za awali za ujauzito.

"Wengi wao hujitokeza ikiwa zimebaki siku chache kwenda kujifungua jambo ambalo si sahihi. Mtu akihudhuria kliniki mapema, inamsaidia kwa kiasi kikubwa kujua matatizo aliyo nayo na kupatiwa matibabu mapema ambayo yanasaidia hata kumkinga kiumbe aliyeko tumboni," alisema.

Akizungumzia suala la lishe kwa watoto wenye ulemavu, alisema wanahitajika kupewa lishe bora kwa sababu inawasaidia kupunguza changamoto za afya ya akili.

"Suala la lishe ni muhimu sana kwa jamii hususan watoto wenye ulemavu kwa sababu linasaidia kuongeza madini ambayo amepungukiwa," alisema.

Alisisitiza suala la unyonyeshaji kwa watoto kwa muda wa miezi sita bila kumpa kitu chochote na baada ya hapo ndipo aanze kupewa chakula cha aina yoyote ile.

"Baada ya miezi sita ya kunyonyesha mtoto anaruhusiwa kula chakula cha aina yoyote ile hususani vile ambavyo vinaleta lishe bora," alisema Dk. Usiri.

Alisema lengo ni kuona watoto wanakuwa katika afya nzuri jambo ambalo linasaidia hata kuwa na uelewa mkubwa kutokana na kwamba amepata lishe inayotakiwa kiafya.



# Dk. Shein ataka CPA kuzingatia mabadiliko ya kimtandao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MABUNGE ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA) yametakiwa kuzingatia zaidi mabadiliko makubwa ya matumizi ya mtandao katika shughuli zao ili kufikia malengo ya demokrasia na utawala bora.

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, wakati akifungua mkutano wa 50 wa CPA uliofanyika mjini hapa.

Alisema matumizi ya teknolojia ya mtandao katika matumizi ya mabunge ya jumuiya hiyo yatasaidia kuwaunganisha wananchi na kujua taarifa mbalimbali zinazofanywa na vyombo hivyo.

Dk. Shein alisema taasisi za mabunge ni chombo muhimu ambacho kinatakiwa kufanya kazi zake kwa uwazi zaidi katika misingi ya demokrasia, utawala bora na uwajibikaji.

Alisema misingi hiyo muhimu katika mfumo wa demokrasia itafikiwa kama mabunge hayo yatafanya kazi zake kwa malengo ya wananchi kujua taarifa mbalimbali.

"Mabunge ya Jumuiya ya Madola sasa yanatakiwa kufanya kazi zake katika mwelekeo wa mawasiliano ya mtandao ambayo yatawawezesha wananchi kupata taarifa mbalimbali kwa wakati," alisema.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kufanya mawasiliano yake na wananchi kwa kutumia Tehama ya serikali mtandao katika huduma zake zote muhimu za jamii.

Alieleza wizara mbalimbali zimeunganishwa na serikali mtandao na sasa huduma za afya na matibabu zinafanyika kwa njia ya mawasiliano ya kisasa kwa kuziunganisha na hospitali za dunia.

"Huduma za upasuaji zinafanyika kwa kutumia mawasiliano ya mtandao kati ya daktari mmoja na mwenzake katika hospitali hizo," alisema.

Alisema hata malipo ya mishahara kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na malipo ya kodi yanayokusanywa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) na taasisi zake ikiwamo walipakodi yanafanywa kwa kutumia mtandao (E- goverment).

"Tumepunguza urasimu na tumerahisisha mambo mengi yanayohusu mapato ya serikali pamoja na walipa kodi...huo ndiyo utawala bora na uwajibikaji," alisema.

Dk. Shein aliwaambia wajumbe wa mkutano huo wapatao 400 kwamba Muungano wa nchi mbili ya Zanzibar na Tanganyika unaendelea vizuri na wa kuigwa katika bara la Afrika.

Alisema Muungano huo ambao umeundwa na waasisi wa mataifa hayo mawili umekuwa imara, huku wananchi wa pande mbili wakifaidi matunda ya amani na utulivu.

"Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni Muungano wa nchi mbili ambao unaendelea vizuri huku ukiwa wa kupigiwa mfano katika bara la Afrika," alisema.

Wakizungumza katika mkutano huo, Rais wa Jumuiya ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Kanda ya Afrika, Rebecca Kadaga, aliwataka wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi ili kutimiza malengo ya demokrasia katika bara hilo.

Kadaga ambaye ni Spika wa Bunge la Uganda, alisema njia pekee ya kuimarisha demokrasia katika Bara la Afrika ni kutoa nafasi kwa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo katika ngazi za vyama vya siasa.

"Vyama vya siasa vitoe nafasi zaidi kwa wanawake kugombea nafasi za uongozi na huko ndiyo kuimarisha demokrasia," alisema.

Mkutano wa mabunge hayo unahudhuriwa na zaidi ya wajumbe 400 wakiwamo maspika wa mabunge hao ukibeba ujumbe; "Bunge mtandao kwa kuwezesha demokrasia".



Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akizungumza wakati wa kikao cha Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, kilichofanyika Zanzibar, jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati na Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi na Katibu Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, Stephen Kagaigai. **PICHA: OFISI YA BUNGE**.

## Wafanyabiashara walia kuporomoka bei ya shokishoki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA wa matunda aina ya shokishoki visiwani hapa wamesema kuwa wingi wa matunda hayo msimu wa mwaka huu, kumeporomosha bei na kupata hasara.

Wakizungumza na Nipashe, walisema msimu wa mwaka huu mashokishoki yamezaa kwa wingi na kusababisha bei kushuka.

Ali Machano, mkazi wa Kijiji cha Donge Karange, alisema mwanzo mwa msimu wa shokishoki ulipoanza walikuwa wakiuza shada moja Sh. 30,000, lakini hivi sasa wanauza Sh. 15,000.

Alisema pia kukosekana na kiwanda cha kusindika matunda Zanzibar, kunachangia wafanyabiashara na wakulima wa zao hilo kupata hasara.

"Shokishoki ni nyingi, nyingine zinaoza kwa kukosa soko, lakini Zanzibar ingekuwa na kiwanda cha kusindika matunda tungekuwa tunauza kiwandani," alisema.

Mkulima wa zao hilo, Salum Taimur Ali, alisema wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo wadudu waharibifu aina ya popo ambao hushambulia matunda hayo yakiwa shambani.

Alisema, licha ya wadudu waharibifu kushambulia zao hilo, lakini pia baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu wanaharibu kwa kuchuma zikiwa bado hazijakomaa.

Alieleza kuwa baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiliharibu soko la zao hilo kwa kufanya udanganyifu wa kuchanganya shokishoki tofauti ambazo zinatofautiana daraja.

"Hizi shokishoki zipo za daraja la kwanza ambazo ndio bora zaidi na zingine za kawaida hivyo baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakidanganya kwa kuzichanganya na wateja hulalamika," alisema.

Aliiomba serikali kuweka kiwanda cha kusindika matunda ili wakulima waweze kunufaika na kilimo.

# Mwakilishi ahamasisha uzalendo kwa vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Tunguu, Simai Mohammed Said, amewaeleza vijana wa Wilaya ya Kati Unguja na Zanzibar kwa jumla kwamba ustawi na maendeleo ya nchi utatokana na uzalendo, ukweli na uaminifu wao.

Akifungua mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kati uliofanyika huko Dunga, Simai, alisema hizo pia ndio silaha zitakazowajengea heshima mbele ya jamii na serikali.

Alieleza, kumekuwa na mdudu mbaya anayeinyemelea nchi ambaye ni kuibuka makundi ya vijana wanaojihusisha na vitendo viovu ikiwamo utapeli kwa tamaa ya kujitafutia fedha.

Simai ambaye pia ni Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, alisema tatizo la uhaba wa ajira linalowakabili vijana haliko Zanzibar pekee bali ni la dunia nzima, hivyo isiwe kisingizio cha kuwashawishi kujiingiza katika mambo yasiyokubalika katika jamii.

Hata hivyo, alisema njia pekee ya kuwakomboa vijana na kuwaletea maendeleo ni kuwa na fikra nzuri na kuzitekeleza kwa pamoja japo kwa mitaji midogo, ambayo baadaye itazalisha fedha za kutosha na kuwaondoa katika umaskini.

Aliwashauri vijana wa wilaya hiyo kichama, kuanzisha mfuko wao wa maendeleo akiahidi kuwachangia Sh. 1,000,000 na kusisitiza uchangiwe kidogo kidogo na kuwekewa utaratibu mzuri wa matumizi.

"Kwani kuna ubaya gani kwa vijana wa Wilaya ya Kati kuwa na daladala yao kama tutakuwa na fedha zetu. Binadamu hawi mdogo kwa kazi atakayoifanya, atakuwa mdogo kwa mawazo yake tu, hata mwanamke anaweza kuwa dereva wa daladala yetu. Tukifanya vizuri baada ya miaka mitano tutakuwa hata na gari tano," alifafanua.

"Mfanyakazi anaweza kuwa analipwa fedha kidogo, lakini akijua kucheza na senti lazima shilingi itakuja yenyewe tu, kama hajui atakuwa mtu wa kulalamika na kulia kwamba mambo magumu."

Aliutaka uongozi wa wilaya kuwatafuta vijana wenye elimu za viwango tofauti wakiwamo wanaojua lugha mbalimbali za kigeni ili awaunganishe na taasisi zinazohitaji kuajiri hasa sekta ya utalii ili nao wanufaike na uwekezaji unaofanyika nchini.

Aliahidi kuyafanyia kazi maombi yao ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili, ikiwamo vijana wa wilaya hiyo kufikiriwa sawa na wengine zinapotokea nafasi mbalimbali za ajira serikalini na kuwahimiza kujiendeleza kielimu.

Kwa upande mwengine, aliwataka watembee kifua mbele wakitambua kwamba zaidi ya CCM hakuna chama kingine chochote kitakachowajali na kuwapa matumaini ya maisha bora, hivyo wakitetea na kukilinda wakati wote.

Mapema Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Wilaya ya Kati, Said Hassan Shaaban, alisema katika kikao chao walijadili mambo mbalimbali ikiwamo jinsi ya kujiimarisha na kujiandaa na ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa taifa mwaka 2020.

Pamoja na kumshukuru mwakilishi huyo kwa misaada anayowapa vijana wilayani humo ikiwamo kuchangia mkutano huo, alisema bado kuna changamoto kadhaa wanazotaka zitafutiwe ufumbuzi.

Alisema uamuzi wao wa kuanzisha kundi maalumu la vijana wa wilaya hiyo umelenga katika mbegu njema itakayowajenga kizalendo ili kuhakikisha wanabaki kuwa waaminifu kwa Chama Cha Mapinduzi hivyo ni vyema kuwashika mkono ili wasisambaratike.

Alieleza kuwa, wazo lao la kumiliki kitega uchumi katika sekta ya kilimo liko katika mchakato wa kutafuta eneo, lakini akasema kwa kuwa vijana ndio nguvu ya ushindi wa CCM, zinapokuja nafasi mbalimbali za ajira wapewe kipaumbele kwani kufanya hivyo ni wajibu na sio kulipa fadhila.

Kwa upande wake Katibu wa Vijana wa CCM Wilaya ya Kati, Salma Omar, aliahidi kuyafanyia kazi mambo yote waliyoagizwa ili kuhakikisha Chama Cha Mapinduzi wilayani kinabaki kuwa imara na tegemeo la maendeleo ya kweli.

# Uboreshaji daftari la kura wapigwa kalenda

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UANDIKISHAJI wa maboresho ya daftari la kudumu la mpiga kura mkoani Shinyanga umeahirishwa kwa mara ya nyingine tena, kwa maelezo kuwa wahusika wanajiandaa kusimamia mitihani.

Taarifa za kuahirishwa huko zilieleza kuwa wasimamizi wa uandikishaji daftari hilo wamekwenda kujiandaa kusimamia mtihani wa kuhitimu elimu ya darasa la saba, ambao unafanyika mwezi huu.

Uandikishaji huo wa maboresho ya daftari la kudumu la mpigakura ulikuwa uanze mkoani Shinyanga Agosti 26 mwaka huu, lakini ukaahirishwa hadi jana Septemba 2, lakini umesogezwa tena mbele kwa mara ya pili.

Msimamizi wa uchaguzi mkoani Shinyanga Amosi Machilika, alisema jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu kuahirishwa kwa mara nyingine tena uandikishaji wa maboresho ya daftari la kudumu la mpigakura mkoani Shinyanga.

Kuandikisha wapigakura kunahusu watu waliofikisha umri wa miaka 18, na waliopotelewa na kadi za kupigia kura.

Alisema idadi kubwa ya wasimamizi wa uandikishaji wa maboresho ya daftari hilo la kudumu la mpigakura ni walimu, ambapo wamekwenda kujiandaa kusimamia mtihani wa darasa la saba na kusababisha uandikishaji huo kuahirishwa kwa mara ya pili tena hadi hapo itakapotangazwa tena.

Alisema sababu nyingine ambayo ni pamoja na watendaji wa kata ambao ndiyo wasimamizi wa usalama wa uchaguzi, kuitwa Ikulu kwenye mkutano na Rais John Magufuli, aliongeza.

Aidha, Agosti 15 mwaka huu Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Balozi Omari Ramadhani Mapuri, akiwa mkoani Shinyanga na wadau wa uchaguzi, alitangaza kuanza uandikishaji huo mkoani hapa Agosti 26.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Albert Jonkergouw (kulia), akiongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, walipokutana katika Mkutano wa Sita wa Jukwaa la Uongozi Afrika, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Awahimiza amani wakulima, wafugaji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KATIBU wa CCM mkoani Morogoro, amewataka wakulima na wafugaji kuzitumia mila na tamaduni zilizopo katika maeneo yao kuepusha mapigano na migongano isiyo na tija.

Kiongozi huyo wa Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, alisema hayo jana wakati akitoa salamu za chama katika Kijiji cha Kiduhi.

Alisema hayo akiwa katika kijiji hicho kilichopo kwenye kata ya Kilangali wilayani Kilosa kwenye sherehe za kumsimika rasmi kiongozi wa kabila la Wamasai 'Laigwanani' wa ukanda wa mikoa ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Dodoma.

Shaka aliwaambia viongozi wa CCM na serikali inayoongoza wanao wajibu wa kuwaweka pamoja wananchi wakiwa katika maelewano ili wafanye kazi kwa pamoja kwa upendo pamoja na mshikamano.

Aliwakumbusha kuwa lengo si kuwagawa au kuchochea migogoro katika kundi fulani kwani unarudisha nyuma suala zima la ustawi wa taifa na maendeleo ya nchi na wao pia.

Katika hatua nyingine, aliwaomba kumuunga mkono kwa vitendo Rais John Magufuli, kwa kuendelea kuishi kwa kupendana na kushirikiana kwa pamoja kama wafugaji na wakulima ili kuepusha uhasama na madhara yasiyo ya lazima miongoni mwao.

Alisema, mwezi Julai, Rais Magufuli wakati akiwa Kisaki aliendelea kuwaasa na kuwasihi kuhusu kuimarisha umoja na mshikamano, sambamba na uelewano kati ya wakulima na wafugaji.

"Jamani hatutaki kuona wananchi wakigombana au kuhasimiana, tabia ya kugombana, kupigana au kubaguana si sehemu ya silka, utamaduni wa Watanzania, bali maelewano ndiyo msingi hasa katika suala la maendeleo yetu," alisema Shaka.

"Leo wenzangu mmenihakikishia kuwa jamii hii mnamuunga mkono Rais Magufuli kwa mema na mazuri ya maendeleo anayoyafanya kwa taifa," alisema Shaka.

Alisema, kiongozi au serikali inapowakanya wananchi wake kuhusu jambo fulani si kama inawaogopa, bali inawataka wajali amani na wote waishi kwa mapatano katika jamii husika.

"Ikiwa kuna mtu anadhani inawaogopa huko ni kujidanganya asitoke mtu akawashawishi mpingane na dola, ishini kwa upendo, huku kila upande ukiheshimu upande mwingine," alisema Shaka.

Shaka aliwaambia Tanzania ina baraka toka enzi na asili na wingi wa makabila si tatizo kwao bali umoja wao na mshikamano walionao ndiyo msingi wa taifa lao.

Kiongozi aliyesimikwa rasmi kuwaongoza Wamasai Oleiboni Mtayani Simanga, kutoka Kijiji cha Kidui, Kata ya Kilangali Wilaya ya Kilosa alisema, atasimamia upatikanaji wa elimu, kushirikiana na serikali na kusaidia ili kufikisha huduma za kijamii kwa wananchi na kuhakikisha kuwa zinaimarika.

Aliongeza kuwa lengo ni wananchi wanakuwa na maisha bora pamoja na nyumba za kisasa za kuishi.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na wazee wa kimila kutoka mikoa yote sita kikanda, viongozi wa dini, wa serikali, wananchi mbalimbali pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi.

Aidha, alikuwapo Katibu Mwenezi wa CCM, Anthony Muhando, pamoja na viongozi kadhaa wa Chama Cha Mapinduzi na jumuiya zake mbalimbali.

# Femata yaomba msamaha wa kodi

**Na Boniface Gideon,** TANGA

SHIRIKISHO la Wafanyabiashara wa Madini nchini (Femata), limeomba serikali kuwasamehe kodi wachimbaji wadogo wa madini waliotapakaa katika mikoa mbalimbali.

Ombi hilo limetolewa na Rais wa Femata John Wambura, wakati wa mkutano wa sita wa wadau wa madini nchini uliofanyika mkoani Tanga.

Wambura alisema wachimbaji wadogo wa madini wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kutokuwa na mitaji na ukosefu wa vifaa vya kisasa vyakuchimbia madini.

Aliongeza kuwa wachimbaji hao wamekuwa wakichimba madini katika mazingira magumu sana hivyo endapo kama watapata msamaha huo utawawezesha kuongeza mitaji yao.

Aidha, katika hatua nyingine waliiomba serikali kuweka bei elekezi ya madini, kuanzishwa benki ya wafanyabiashara wa madini, pia kuwa siku ya madini kitaifa.

Alisema siku ambayo itajumuisha nchi mbalimbali za Umoja wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC), ili kupanua wigo wa soko la madini.

Wambura aliiomba serikali kuondoa changamoto ya ucheleweshwaji wa utoaji wa leseni.

Kwa upande wake Waziri wa Madini Doto Biteko, aliwataka wataalamu wa ofisi ya madini kuacha tabia ya kuwakatisha tamaa na kuwavunja moyo wachimbaji wadogo pale wanapotaka kuwekeza kwenye sekta hiyo.

"Naomba wataalamu wangu mhakikishe mnatoa huduma kwa wakati. Wapeni elimu wachimbaji wadogo na kuwasaidia kuwapa njia zitakazowawezesha kupata mikopo kwenye benki zetu," alisema Biteko.

Biteko alisema kumekuwapo na ujanja kwenye sekta hiyo kuanzia kwa wachimbaji, wafanyabiashara na baadhi ya wataalamu wa madini kwa kujihusisha na utapeli.

"Kumekuwapo na utapeli mkubwa kwa baadhi ya wenzetu wanaotaka kuharibu soko la madini yetu duniani. Wapo tuliowakamata, tupo macho muda wote kuhakikisha mtu hatoroshi madini wala kutapeli kwa njia ya mtandao," alisema Biteko.

ITV

JARIDA LA WANAWAKE

SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA MAMA MWINGIRA TOKA KIGAMBONI JIJINI D`SALAAM AKITENGENEZA NGUO ZA BATIKI NA PIA AKIFANYA BIASHARA YA KUSINDIKA MBOGAMBOGA.

## HABARI KIMATAIFA

## Wanafunzi wapanga kususia shule Hong Kong

**HONGKONG,** China

WANAFUNZI wa shule za sekondari katika Jiji la Hong Kong wanatarajia kugoma kwenda shule kama ishara ya kuunga mkono mwendelezo wa maandamano ya kuipinga serikali.

Hong Kong inaendelea kukumbwa na maandamano baada ya kutokea kwa vurugu mwishoni mwa wiki kati ya polisi na waandamanaji.

Maandamano mapya yanatarajia kufanyika leo, wanafunzi wakiwa katika mstari wa mbele.

Wanafunzi walipanga kuanza mgomo jana alasiri na kukusanyika kwenye uwanja uliopo kati kati ya mji wa Hong Kong.

Pamoja na madai mengine wanafunzi hao wanataka kufutwa kwa mashitaka yanayowakabili waandamanaji waliokamatwa.

Maandamano haya yanatarajia kudumu wiki mbili. Mwaka wa shule Hong Kong ulianza jana.

Waandamanaji wanataka mageuzi ya mfumo wa uchaguzi na uchunguzi huru ufanywe juu ya tabia ya vitendo vya polisi. **RFI**



## Watalii waliofariki kwenye hifadhi

**NAIROBI,** Kenya

MAMLAKA ya idara ya wanyama pori nchini Kenya (KWS) imesema miili ya watalii sita waliofariki Jumapili kutokana na mafuriko katika hifadhi ya taifa ya Hell's Gate imepatikana.

Imesema mtalii mmoja bado hajulikani alipo na shughuli za kumtafuta zinaendelea.

Watalii hao ambao raia watano ni wa Kenya, mmoja wa kigeni na muongozaji wao walikumbwa na maji ya mvua walipokuwa wakiitembelea mbunga hiyo ya wanyama ya Hell's gate.

Siku ya Jumapili, mbuga hiyo ilifungwa kutokana na mvua kubwa iliyokuwa inanyesha.

Vyombo vya habari nchini humo vimeripoti kuwa watu hao walikuwa miongoni mwa kundi la watu 12 waliokuwa wanazuru hifadhi ya Hells Gate, iliyopo kilomita 100 Kaskazini magharibi mwa Jiji kuu la Nairobi.

Vyanzo vya habari Kenya vinaeleza manusura waliwajulisha maofisa wa hifadhi tukio hilo na juhudi za kuwatatufa watu hao zilianza. **VOA**

# Antonio Guterres akamilisha ziara DRC

**KINSHASA,** Congo

KATIBU Mkuu wa Umoja wa mataifa (UN), Antonio Guterres, amekamilisha ziara yake mashariki ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), kwa kutembelea kituo cha afya wanakotibiwa wagonjwa wa ebola magharibi mwa mji wa Beni.

Katika ziara yake kwenye kituo hicho kilicho katika mji mdogo wa Mangina kilomita thelathini magharibi mwa mji wa Beni, Guterres aliwasihi manusura wa Ebola kuwahamasisha watu walio karibu nao kutokuwaficha majumbani wagonjwa, ili kusaidia kuitokomeza haraka homa ya ugojwa huo.

Baada ya kupokelewa na matabibu pamoja na manusura wa homa ya ebola katika kituo cha afya wanakotibiwa wagonjwa wa homa hiyo, Guterres amewahutubia manusura wa ebola katika kituo cha afya cha Mangina, na kutoa wito wa kusambaza ujumbe kuwa wote wanaofika katika kituo hicho wanaweza kupona.

**Pia litakuwa mojawapo ya maswala yatakayojadiliwa katika mkutano baina yake na Rais wa DRC, Félix Tshisekedi mjini Kinshasa.**

Aliwataka pia wananchi kutoficha dalili za homa ya ebola, waje na kutumia fursa ya kuushinda ugonjwa wa ebola kwa kupata tiba katika kituo hicho.

Kwa upande wake Gavana wa mkoa wa Kivu ya kaskazini, Charly Nzanzu Kasivita, aliwasihi watu wanaopinga uwapo na makali ya ebola kuondokana na dhana hiyo potofu, na kufika kupata matibabu katika eneo lililotengwa kwa ajili ya matibabu ya ebola

Hali ya usalama mdogo katika eneo hilo ni moja wapo ya vikwazo katika mpango wa kukabiliana na ebola, Guterres, alihaidi kuwa patafanyiwa mageuzi katika utendaji kazi wa tume ya Umoja huo nchini DRC MONUSCO ili raia wapate kunufaika na uwapo wa tume hiyo.

Pia litakuwa mojawapo ya maswala yatakayojadiliwa katika mkutano baina yake na Rais wa DRC, Félix Tshisekedi mjini Kinshasa.

Tume ya Umoja wa mataifa kwa ajili ya kustawisha amani katika DRC, ndio tume kubwa ya Umoja huo duniani na iliyo na vifaa tosha, lakini imekuwa ikilaumiwa na raia nchini humo kwamba haijafanya vyema katika utendaji kazi wake.

Imekuwa ikilaumiwa kushindwa kuyatokomeza makundi ya waasi katika mji na wilaya ya Beni, pamoja na lile la ADF kutoka Uganda, linalotajwa kuhusika na mauaji ya watu zaidi ya 2,000 katika eneo hilo kwa kuwakata kwa mapanga pamoja na risasi. **DW**



Katibu Mkuu wa Umoja wa mataifa, Antonio Guterres (katikati), akiwa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) alipotembelea kituo cha afya wanakotibiwa wagonjwa wa Ebola magharibi mwa mji wa Beni. **PICHA: REUTERS**

# Watu 100 wauawa nchini Yemen

**SANA'A,** Yemen

TAKRIBANI watu 100 wameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa baada ya mashambulio ya angani yaliofanywa na muungano unaoongozwa na Saudi Arabia kulenga kituo cha mahabusu kinachosimamiwa na waasi wa Kihouthi nchini Yemen.

Shambulio hilo la angani lililofanywa na muungano wa Saudi Arabia linatajwa kuwa baya zaidi kwa mwaka huu nchini Yemen.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la msalaba mwekundu ilieleza kuwa shambulio hilo limewaua watu 100 na kuwaacha wengine 40 wakiuguza majeraha.

Hata hivyo, muungano wa Saudia umekanusha kuwa shambulio hilo la angani lilikuwa linalenga kituo cha mahabusu na badala yake kudai kuwa lililenga kambi ya jeshi.

Kiongozi wa ujumbe wa Shirika la msalaba mwekundu nchini Yemen, Franz Rauchenstein alisema kuwa idadi ya vifo kutokana na shambulio hilo la angani huenda ikaongezeka.

Rauchenstein, alizuru eneo la tukio na kueleza kuwa ni watu wachache tu ndio walionusurika.

Kituo hicho kilicholengwa, kipo katika eneo la Kusini Magharibi mwa Wilaya ya Dhamar na kilikuwa kimehifadhi wafungwa 170.

Mjumbe maalumu wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Yemen, Martin Griffiths, alitoa wito kwa pande hasimu katika mzozo wa Yemen kukaa katika meza ya mazungumzo ili kumaliza vita hivyo.

Wito huo ameutoa ikiwa imepita siku moja tu baada ya kufanya mkutano na Waziri wa Mambo ya Nje wa Sweden, Margot Wallstrom katika Mji Mkuu wa Jordan wa Amman.

Ziara ya Wallstrom mjini Amman inalenga kutafuta muafaka wa maelewano baina ya pande hasimu nchini Yemen.

Awali, kulikuwapo makubaliano kati ya muungano unaoongozwa na Saudi Arabia na waasi wa Kihouthi wanaoungwa mkono na Iran ili kusitisha vita na kuleta amani, japo makubaliano hayo bado hayajatekelezwa kiukamilifu.

Marekani, na muungano huo wa Saudi Arabia ambao umekuwa ukipambana na waasi wa Houthi nchini Yemen wanaoungwa mkono na Iran tangu Machi 2015, umekosolewa vikali kimataifa kutokana na mashambulizi yake kuzilenga shule, hospitali, vituo vya kujivinjari na sehemu nyengine za umma na kusababisha vifo vya maelfu ya raia wasiokuwa na hatia.

Waasi hao wa Kihouthi wanaodhibiti eneo kubwa la kaskazini mwa Yemen ikiwamo Mji Mkuu sanaa waliilazimu serikali inayotambuliwa kimataifa kukimbilia uhamishoni mwaka 2014. **DW**

# Tanzania yasifiwa vita biashara wanyamapori

**Na Salome Kitomari,** aliyekuwa THAILAND

TANZANIA imetajwa kuwa mfano mzuri katika mapambano ya biashara haramu ya mazao ya wanyamapori na kuwezesha idadi ya tembo na faru kuongezeka kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.

Hayo yalisemwa kwa nyakati tofauti na wataalamu mbalimbali waliokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kutoka Thailand na Tanzania katika programu ya kubadilishana uzoefu kwa waandishi wa nchi hizo, iliyoandaliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID Protect) na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania.

Programu hiyo imelenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari kufichua ujangili wa wanyamapori kuanzia kwenye chanzo Afrika hadi kwenye watumiaji ikiwamo njia kuu ya kupitishia ambayo ni Thailand.

Mratibu wa kanda ya Asia na Pasifiki wa Umoja wa Mataifa inayojishughulisha na dawa za kulevya na uhalifu (UNODC), Giovanni Broussard, alisema Tanzania imeonyesha mfano kwa kuimarisha sheria ikiwa ni pamoja na kukamata waliokuwa hawakamatiki.

"Kwa Afrika tangu kuingia madarakani kwa serikali iliyopo sasa nchini Tanzania tunaona mabadiliko makubwa kwenye udhibiti wa biashara ya meno ya tembo, pembe za faru na wanyamapori kwa ujumla," alisema na kuongeza:

"Kwa maoni yangu mara zote tunavyoitisha mikutano kati ya Asia na Afrika unaona ujumbe mzito kutoka Tanzania, ni nchi iliyoamua kwenda kwenye mfumo wa kisheria wa kupambana na ujangili wa wanyamapori na mafanikio yanaonekana sasa," alisema.

Alisema, Tanzania imeonyesha njia katika kubadilisha mwelekeo wa namna ya kupambana na ujangili wa wanyamapori, kwa Asia hakuna nchi imefanya kama Tanzania inavyofanya kwa sasa, huku nyingine zikichukua suala hilo kama la utawala na mazingira.

Kwa mujibu wa Broussard, Tanzania ni moja ambayo imeweka wazi msimamo wake wa kupambana na ujangili kwa kuhakikisha mifumo ya utekelezaji wa sheria inashirikiana, jambo ambalo limesaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na biashara hiyo.

Alisema utayari wa serikali kupambana na ujangili huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuendelea kuwalinda tembo, faru na wanyama wengine kwa kuwa hawana namna ya kutolewa nje ya nchi hiyo na kwamba kinachotakiwa na nchi nyingine za Afrika kuiga utunzaji wa rasilimali wanyama.

Alishauri Tanzania kuimarisha ushirikiano na nchi za Asia ambako nyara nyingi hupelekwa, ili kuhakikisha kama kuna kontena au mizigo yoyote inakuja ukanda huo inakaguliwa kwa kina ikiwamo kuwasiliana na mamlaka husika.



Mafundi wa ujenzi wakiendelea na kazi ya kujenga mifereji ya maji taka katika Mtaa wa Salmin Amour Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wafanyabiashara wahamasishwa kongamano na Uganda wiki hii

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa Tanzania wameelezwa kutumia fursa ya kongamano la kwanza la biashara kati ya Tanzania na Uganda litakalofanyika jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo litazinduliwa na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni Septemba 6-7, mwaka huu ambaye amealikwa na Rais John Magufuli.

"Wafanyabiashara waelewe kuwa ni mwanzo mzuri wa kupenya katika soko la Sudani ya Kusini kwasababu wapo wafanyabiashara wa Uganda wanafanya biashara nchini Sudani ya Kusini," alisema Waziri wa Vowanda na Biashara," Innocent Bashungwa.

Aliendelea kusema kuwa mwelekeo wa Serikali ya Tanzania ni kujenga uchumi wa viwanda, hivyo ni fursa kwa Watanzania kutumia kongamano hili kwa sababu Serikali inazidi kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara nchini, kujenga viwanda na kufuatilia masoko mbalimbali lengo ni kutaka uuzaji wa bidhaa nchini Uganda uongezeke.

Rais wa Museveni ataambatana na wafanayabiashara kutoka nchini kwake ili kukutana na wafanyabiashara wa Tanzania. Bashungwa ameeleza kuwa lengo la kongamano hilo ni kutangaza fursa na kuhamasisha biashara na uwekezaji zilizoko Tanzania na Uganda., na kwamba Serikali itapata fursa ya kuongea na wafanyabiashara hao ili kuangalia changamoto za kufanya biashara katika nchi hizo mbili.

Pia Serikali zetu zitashirikiana kuzitatua, kuangalia fursa zilizopo, kuongeza biashara katika nchi hizo mbili na kuhamasisha uwekezaji.

"Sisi Tanzania tumekuwa tunawauzia chakula na vifaa vya viwandani, kwakuwa tunajenga uchumi wa viwanda ni fursa kwa Watanzania kushiriki kwenye kongamano hilo ambalo litakuwa na tija kubwa kwetu kama nchi," alisema na kuongeza:

"Rais wetu analeta wakuu wa nchi mbalimbali ikiwamo Uganda ili kuwaonesha fursa tulizonazo pamoja na kujenga mtandao mpana wa biashara", alisema Bashungwa.

# Waliovamia hifadhi watakiwa kuondoka

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ametoa siku moja kwa wananchi waliovamia maeneo ya hifadhi nchini baada ya tamko la Rais John Magufuli kuhusiana na hifadhi waanze kuondoka mara moja.

Amesema agizo hilo linawalenga wananchi waliojimegea maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, malisho na makazi kwa kisingizio cha kauli ya Rais John Magufuli aliyoitoa Januari 15, mwaka huu.

Kanyasu alitoa amri hiyo juzi alipokuwa akizungumza na wakazi wa Nyamgusu wilayani Geita mkoani hapa na kuwaonya waache tabia ya kupotosha kauli ya Rais kwa manufaa binafsi kwa kujitwalia maeneo mapya ya hifadhi.

Pia aliwataka wananchi hao wasubiri hadi pale Rais Magufuli atakapotoa ripoti iliyowasilisha kwake na kamati ya mawaziri wanane iliyokuwa ikishughulikia masuala ya maeneo ya hifadhi.

Alisema sasa kumeibuka kundi la watu ambao wanaingia katikati ya misitu ya hifadhi na kuanza kufyeka miti na kuanzisha makazi kwa madai ya kuwa Rais ametoa ruhusa ya kufanya hivyo.

Kanyasu alisema baadhi ya wananchi kwa kisingizio cha tamko la Rais, wameanza kuyamega maeneo ya hifadhi vipande vipande na kuanza kuyauza kwa wananchi wengine.

"Kama kuna mtu kakuuzia au umevamia mwenyewe eneo la hifadhi, nakupa siku moja anza kuondoka. Tukikukuta huko utahesabika ni mhalifu," alisema.

Kutokana na agizo hilo, Kanyasu aliwatahadharisha wananchi watakaokutwa ndani ya hifadhi watatakiwa kulipa gharama za miti itakayokutwa imekatwa bila kibali ikiwa pamoja na kuchukuliwa sheria kali.

Kanyasu pia aliwataka wananchi wasitumie vibaya tamko la Rais kuhusiana na hifadhi badala yake wasubiri utaratibu utakaotolewa hivi karibuni kutokana na mapendekezo ya kamati ya mawaziri.

Alisema mbali na vijiji na vitongoji 365 alivyokuwa amevitaja Rais, imebainika kuwa zaidi ya maeneo 800 yalivamiwa na wananchi ndani ya hifadhi.

Kwa mujibu wa Kanyasu, baada ya ripoti hiyo itakapotolewa kwa maeneo yatakayobainika yamepoteza sifa ya kuendelea kuwa hifadhi yatapangiwa matumizi bora ya ardhi na vijiji husika.

" Hatuwezi kulima kila eneo, hatuwezi kujenga kila eneo vilevile hatuwezi kulisha mifugo kila eneo hii itakuwa si nchi," alisisitiza Kanyasu.

Naibu Waziri aliyataja baadhi ya mikoa ambayo maeneo ya hifadhi yamevamiwa kwa kiasi kikubwa na wananchi baada ya tamko la Rais kuwa ni Geita, Morogoro, Kagera, Singida, Lindi na Mtwara.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NAFASI ZA KAZI

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma

Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

### VYETI VIMEPOTEA




EUNICE PAULO PALLANGYO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4152/0018 kilichotolewa na MOMELLA SEKONDARI mwaka 2016. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba P.4352/0015 kilichotolewa na VTC MSHIKAMANO mwaka 2017.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/KIL/RB/181018/2019.

115399902

### CHETI KIMEPOTEA



HILDA THOMAS KOMBA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2033/0028 kilichotolewa na VIWANDANI SEKONDARI mwaka 2014.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:

DOM/RB/8260/2017.

115400002

### KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**NASSORO L. NGULUNGULU** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **RAV4** Old Model **T 978 DKT** yenye Chassis namba **SXA117043288** na Injini namba, **3S2228422** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taafifa : **MS/RB/3167/2019**

215400702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Anaitwa **ALBERT MARTIN LIKOMAWAGI** amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili **MC 339 BNC.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/261111/2019.**

215400402

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MAN CITY HAIKUWA NA FEDHA KUNUNUA BEKI – GUARDIOLA



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City haikuweza kusajili beki wa kati kipindi hiki cha majira ya joto, kwa mujibu wa Pep Guardiola.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England walitumia zaidi ya pauni milioni 120 kipindi cha majira ya joto kuwaongeza kikosini mwao, Rodri, Joao Cancelo na Angelino, lakini sasa wanakabiliwa na tatizo kwenye safu ya ulinzi kama Aymeric Laporte atakuwa nje kwa muda mrefu kutokana na majeruhi ya goti.

City walijaribu kutafuta mrithi wa Vincent Kompany kwa kutaka kumsajili Harry Maguire, lakini ofa yao ilikataliwa na Leicester na matokeo yake akasajiliwa na Manchester United na Guardiola amesema hakukuwa na fedha za kufanya usajili wa beki wa kati.

"Hatukuweza kununua kama wapizani wetu," alisema Guardiola. "Klabu inafanya kazi vizuri kwa kila idara zake na wakati mwingine hatuwezi kufanya kama klabu nyingine vinavyofanya.

"Tunalipa fedha nyingi kwa ajili ya wachezaji wengi, ndio maana tunakuwa na kikosi kipana chenye ubora, lakini hatuwezi kufanya hivyo, unakuwa na fedha ambazo huwezi kusonga nazo mbele.

"Pengine kwa siku za usoni lakini sio sasa, huwezi kufanya chochote. Nasema sawa, huwezi kufanya kila jambo kwa wakati wote."

Laporte alipelekwa hospitali baada ya mchezo wa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Brighton Jumamosi.

# James mfano kwa wachezaji Man U-Ole

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anaamini kwamba, kinda Daniel James anatengeneza mfano wa kuigwa klabuni hapo kwa kujifua kwa bidii kwenye mazoezi na wengine wanapaswa kumuiga.

James, alisajiliwa kutoka Swansea City kipindi hiki cha majira ya joto, alifunga kwenye sare ya 1-1 Jumamosi dhidi ya Southampton wakati alipoingia ndani ya box na kumfunga kiurahisi Angus Gunn.

Hilo lilikuwa bao la tatu kwa James katika mechi nne, na kumfanya kuwa mfungaji bora wa kwa sasa na kuwazidi wachezaji wenye uzoefu kama Marcus Rashford na Anthony Martial ambao wote wana mabao mawili kila mmoja.

"Nafikiri ameweka mfano kwa kila mmoja," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa sasa ndie mfungaji wetu bora na hiyo imekuja baada kujituma kwa bidii kwenye mazoezi.

"Ni mnyenyekevu, anajituma na anajua kwamba anaweza kuimarika. Anaingia uwanjani kwa kutengeneza matokeo na hilo amekuwa akilionyesha tangu akiwa kwenye mazoezi."




# *Fifa yampambanisha tena Van Dijk, Messi na CR7*



**PARIS,** Ufaransa

SHIRIKISHO la Soka la kimataifa, Fifa, limetangaza wachezaji walioingia fainali katika kinyang'anyiro cha tuzo ya wachezaji bora wa dunia kwa mwaka 2019.

Tuzo hizo zitakazotolewa Septemba 23 mwaka huu katika jiji la Milan nchini Italia, zitakuwa na jumla ya vipengele 8 vyenye washindani watatu kwa kila kipengele.

Tuzo ya mchezaji bora wa kiume wapo Cristiano Ronaldo wa Juventus, Lionel Messi wa Barcelona na Virgil van Dijk wa Liverpool.

Tuzo ya mchezaji bora wa kike wanaowania ni Lucy Bronze (Olympique Lyonnais), Alex Morgan (Orlando Pride) na Megan Rapinoe (Reign FC), huku nafasi ya kocha bora kwa timu za wanaume inawaniwa na Pep Guardiola (Manchester City), Jurgen Klopp (Liverpool) na Mauricio Pochettino (Tottenham Hotspur).

Kocha bora wa timu za Wanawake wanaowania ni Jill Ellis (Marekani), Phil Neville (England) na Sarina Wiegman (Uholanzi, huku tuzo ya golikipa bora wa kiume inawaniwa na Alisson (Liverpool), Ederson (Manchester City) na Marc-André ter Stegen (Barcelona).

Kwa upande wa golikipa bora wa kike wanaowania ni Christiane Endler (Paris Saint-Germain), Hedvig Lindahl (Chelsea/Wolfsburg), Sari van Veenendaal (Arsenal/ Atletico Madrid).

Tuzo ya goli bora (Puskas Award) linawaniwa na Lionel Messi (Real Betis vs FC Barcelona), Juan Fernando Quintero (River Plate vs Racing Club) na Dániel Zsóri (Debrecen FC vs Ferencváros TC).

Kwa upande wa tuzo ya shabiki bora inawaniwa na Silvia Grecco (Brazil), Mashabiki wa timu ya taifa ya Uholanzi kwenye Kombe la Dunia kwa Wanawake na Justo Sánchez (Uruguay).

# Sare ya Real Madrid yamchefua Zidane

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane alionesha kutoridhishwa na kiwango cha kikosi chake, lakini alisifia jitihada walivyofanya kuweza kupata sare ya kufunga mabao 2-2 dhidi ya Villarreal kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, juzi Jumapili.

Garethi Bale alifunga mara mbili kuiwezesha Real Madrid kupata sare hiyo, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Wales alimaliza kwa kutolewa nje kwa kadi ya pili ya njano dakika za majeruhi.

Real walianza kufungwa dakika ya 11 wakati nahodha wake, Sergio Ramos alipopoteza mpira na haraka Gerard Moreno akauwahi na kufunga bao.

Bale alisawazisha dakika ya mwisho ya kipindi cha kwanza akiunganisha kjrosi ya Dani Carvajal, lakini Villarreal wakafunga la pili dakika ya 74 kupitia Moi Gomez, baada ya Benzema bao lake kukataliwa kuwa aliotea.

Bale tena akafunga dakika ya 88 kuweza kupata sare hiyo, lakini akatolewa nje baada ya kuonyesha kadi ya pili ya njano iliyozaa nyekundu.

Madrid imepata pointi tatu katika mechi zake tatu za ufunguzo, moja zaidi ya Barcelona, lakini kikosi hicho cha Zidane kimepitwa pointi moja na vinara Atletico Madrid, ambao wameshinda mecho zote tatu.

"Tulianza mpira kwa kasi ndogo, tulikuwa kwenye mchezo kwa dakika 15 tu, lakini mara zote tunatakiwa kuanza kwa kasi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini tuliweza kurudi mchezoni na kufanikiwa kufunga mabao na tukapa pointi moja.

"Hatukucheza vizuri kwenye safu ya ulizni, lakini jambo la msingi ni kwamba tuliondoka na pointi moja."







# INTER YATOA OFA KWA ICARDI KWENDA PSG

**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI Inter Milan, Mauro Icardi, amepewa ofa ya kwenda kwa mkopo katika Klabu ya Paris Saint-Germain, ambao wanamhitaji nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, kwa mujibu wa ESPN FC.

Nerazzuri hao walijaribu kumuuza kipindi hiki cha majira ya joto na wamemuondoa kwenye kikosi cha kwanza.

Yeye hayupo kwenye mipango ya kocha, Antonio Conte msimu huu, lakini licha ya yote hayo, Icardi mwenyewe amekataa ofa kadhaa za kutoka kwa klabu ziizokuwa zinamuwania.

Na sasa Inter Milan wametoa ofa kwa PSG, ambao wanatafuta mshambuliaji baada ya kuumia kwa Edinson Cavani na Kylian Mbappe. Mkurungenzi wa PSG, Leonardo anafikiria kumchukua Icardi kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Mabingwa hao wa Ufaransa wamebainisha kwamba, wanaweza kuuhimili mshahara wa mshambuliaji hiyo.

Icardi na mke wake, Wanda Nara, ambaye pia ni wakala wake wameonesha nia ya kutaka kuhamia jijini Paris.

Wakati dirisha la usajili lilikuwa linafungwa jana jioni, Icardi alikuwa na nafasi ya kukamilisha usajili wake huo.

Icardi amefunga mabao 121 katika mechi 219 alizoichezea Inter kwenye ligi Kuu ya Italia, Serie A.

# *Lukaku aitwa nyani akiipa ushindi Inter*

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku alikumbana na kelele za ubaguzi wa rangi kwa kuitwa nyani wakati alipofunga kwa penalti kipindi cha pili kuiwezesha Inter Milan kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Cagliari kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jumapili.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United alipigiwa kelele za kufananishwa na nyani katika uwanja wa nyumbani wa Sardegna Arena wakati akijiandaa kupiga penalty hiyo.

Mchezaji wa zamani wa Juventus, Moise Kean pia alikumbana na hali kama hiyo ya kubaguliwa kwa mashabiki wa Cagliari kwenye uwanja huo huo msimu uliopita.

Lukaku mwenye umri wa miaka 26 alimfunga golikipa Robin Olsen kwa kupeleka kushoto na mpira kujaa nyavu ya kulia zikiwa zimesalia dakika ya 20 mpira kumalizika na akakumbana na kelele hizo.

"Nafikiri nchini Italia elimu zaidi inatakiwa kutolewa kuhusu ubaguzi wa rangi," alisema kocha wa Inter, Antonio Conte wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Lautaro Martinez alianza kufunga bao la uongozi kabla ya Joao Pedro kusawazisha baada ya mapumziko.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG: SPURS INABAHATI KUCHOMOKA

Asema Arsenal ilistahili kushinda, Luiz naye adai mabeki wanapaswa kuwajibika na...

**LONDON,** England

STRAIKA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, anaamini Tottenham walikuwa na bahati nzuri kupata sare ya mabao 2-2 katika Uwanja wa Emirates juzi.

Spurs walijikuta wakiongoza kwa mabao 2-0 kipindi cha kwanza, wakitumia makosa ya mabeki wa Arsenal kuwaadhibu baada ya Bernd Leno kupangua mpira kizembe na kumkuta Christian Eriksen aliyeuzamisha kimyani huku Granit Xhaka akimchezea madhambi Son Heung-min ndani ya 18 na kuzawadiwa penalti iliyozamishwa nyavuni na Harry Kane.

**Lakini Alexandre Lacazette alijibu sekunde kadhaa kabla ya kuelekea mapumziko akifunga kwa shuti kali ndani ya 18 na Aubameyang aliihakikishia kuondoka na pointi dakika 19 kabla ya mechi kumalizika, akiunganisha nyavuni krosi kutoka kwa Matteo Guendouzi.**

Arsenal waliweza kumiliki kipindi chote cha pili, na kupata sare hiyo, na Aubameyang anahisi Spurs walikuwa na bahati kidogo ya kutoangukia kipigo.

"Nadhani katika kipindi cha kwanza tulistahili kufunga mabao mawili," aliiambia Sky Sports. "Tulifanya kazi nzuri.

"Ilikuwa mechi ngumu na nadhani tulistahili zaidi. Wakati unapoelekea mapumziko na ukiwa umefunga bao mara zote ni chanya, hivyo ilikuwa muhimu kufunga [kabla ya mapumziko]."

Aubameyang kwa sasa amefunga katika mechi saba mfululizo za Ligi Kuu England alizoanza katika Uwanja wa Emirates, mbio ambazo anazidiwa na Thierry Henry pekee, ambaye alicheka na nyavu katika mechi tisa mfululizo wakati Arsenal ikitumia dimba la Highbury.

Pia ni kinara wa ufungaji miongoni mwa wachezaji wa Arsenal waliopo katika kikosi hicho kwa sasa, mabao yake 44 yanayapiku yale ya Mesut Ozil.

Kocha Unai Emery bado anapendelea kumchezesha Aubameyang winga ya kushoto na alifanya hivyo dhidi ya Spurs, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Gabon anakuwa tayari kutekeleza jukumu lolote analopewa.

"Ilikuwa pasi murua kutoka kwa Guendouzi [kwa bao langu] - alinitazama na alijua nitakimbia," alisema. "Ninapenda kucheza nafasi ya ushambuliaji, lakini wakati timu inaponihitaji kucheza winga ninakwenda na kujaribu kwa kadri ya ubora wangu."

Katika hatua nyingine beki wa kati wa timu hiyo, David Luiz amesema safu ya ulinzi ya Arsenal inapaswa kuwajibika kwa makosa yao dhidi ya Tottenham.

Luiz alisema Arsenal inapaswa "kupevuka" na kutambua makosa yaliyowagharimu wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tottenham.

Luiz pia alikosolewa kufuati kipigo cha mabao 3-1 mwezi uliopita ugenini dhidi ya Liverpool, wakati mchezaji mwenza Sokratis na Xhaka walikosolewa kwa kuwa sehemu ya kuiruhusu Tottenham kupata mabao mawili Jumapili.

"Nadhani [kukosolewa] ni kawaida, katika kazi yangu yote imekuwa kama hivyo, na zaidi wakati unapokuwa beki," aliiambia Sky Sports News.

## ZISIKUPITE

### BARCA KUMRUDIA NEYMAR

BARCELONA imehitimisha mpango wake wa kutaka kumsajili Mbrazil Neymar, 27, kutoka Paris St-Germain na badala yake itarudi tena katika dili hilo. ***(ESPN)***

### AMTAKA IBRAHIMOVIC

KOCHA wa Napoli, Carlo Ancelotti, amesema atafungua milango ya kuinasa saini ya straika Msweden Zlatan Ibrahimovic, 37, kutoka LA Galaxy. ***(Sun)***

### MKHITARYAN KAAMKIA ROMA?

ROMA jana ilikuwa na matumaini ya kuinasa saini ya kiungo wa Arsenal, Muarmenia, Henrikh Mkhitaryan kwa mkopo. ***(Sky Italy - in Italian)***

### PSG, BARCA SHIDA IPO HAPA

LICHA ya Neymar kuahidi kuchangia pauni milioni 17.7 katika dau la Barca kumnunua, mazungumzo kati ya klabu hiyo ya Hispania na PSG yalivunjika kutokana na miamba hiyo ya Ufaransa kutaka dau kubwa zaidi. ***(Sky Sports)***

### FERNANDES AITESA REAL USIKU

REAL Madrid jana ilikuwa inajipanga kutoa pauni milioni 64 kabla ya dirisha la usajili kufungwa usiku ili kumpata kiungo wa Sporting Lisbon na Ureno, Bruno Fernandes, 24. ***(Mail)***

### NAVAS, AREOLA WAPISHANA

REAL Madrid pia jana usiku ilitaka kuinasa saini ya kipa wa Ufaransa Alphonso Areola, 26, kutoka Paris St-Germain, wakati mlinda mlango wa Costa Rica, Keylor Navas, 32, naye akihamia upande wa pili. ***(Mirror)***

### BOATENG KIMEELEWEKA JUVE?

BEKI wa Bayern Munich, Mjerumani Jerome Boateng, jana alikua amekaribia kukamilisha mpango wa kujiunga na mabingwa wa Italia, Juventus. ***(Bild - in German)***

### CAN, RAKITIC KUPISHANA

JUVENTUS bado haijanyoosha mikono juu ya kuipata saini ya kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic - na jana ilikuwa tayari kumtoa ofa Mjerumani Emre Can, 25, ili kubadilishana. ***(Sport - in Spanish)***

### DORTMUND YAISIKILIZIA LIVER

BORUSSIA Dortmund jana ilikuwa inajiandaa kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Bobby Duncan, 18, lakini ikitazama kama miamba hiyo ya Ligi Kuu England itakubali kuhitimisha mkataba wake. ***(Mirror)***

### PSG MACHO KWA ICARDI

PSG inavutiwa kuipata saini ya Mauro Icardi, 26, kwa mkopo kutoka Inter Milan. ***(RMC Sport - in French)***

### SKRTEL AACHANA NA ATALANTA

BEKI wa zamani wa Liverpool, Martin Skrtel amevunja mkataba na miamba ya Serie A, Atalanta wiki moja tu baada ya kutia saini ya kuitumikia klabu hiyo. ***(Mail)***

### UNITED, CITY ZOTE KWA EVJEN

MANCHESTER United itaingia katika mbio moja na majirani zao, Manchester City kuisaka saini ya kiungo wa FK Bodo/Glimt na Norway U-20, Hakon Evjen, 19, katika dirisha la Januari. ***(Mirror)***

## Watoto kufundishwa mbio za magari

**Na Moshi Lusonzo**

SERIKALI imekipongeza Chama cha Wamiliki wa Magari ya Michezo (AAT), kwa kuanzisha mpango maalum wa mafunzo ya udereva wa mbio za kasi kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mradi huo jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo nchini (BMT), Neema Msita, alisema mafunzo hayo ya miezi mitatu yatafungua njia kwa Tanzania kuwa na madereva bora wa mchezo huo katika miaka michache inayokuja.

Alisema mafunzo hayo yatakayowahusisha wanafunzi wenye umri kuanzia miaka 12 hadi 15, yatawezesha watoto wenye kipaji cha mbio za magari ya kasi na serikali ina wajibu wa kuwaangalia kwa ukaribu.

"Mafunzo haya hayatanufaisha AAT pekee bali nchi itapata wanamichezo mahiri na wenye uwezo wa kushindana na nchi zingine na ninaamini tutafika mbali," alisema Msita.

Msita amesema baraza lake litafuatilia ahadi ya Waziri wa Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe ya kuwapatia kiwanja eneo la Kigamboni kwa ajili ya kuanzisha kituo maalum cha mbio za magari nchini.

Awali Rais wa AAT, Nizar Jivan, aliiomba serikali kuangalia namna ya kuwapunguzia kodi katika vifaa vya kufundishia vinavyoletwa nchini kama msaada kutoka Shirikisho la Mbio za Magari duniani, FIA.

## Wushu kusaka vyama mikoani

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Wushu (Karate) Tanzania, kipo mbioni kutafuta vyama vya mchezo huo mikoani baada ya kubaini uwapo wa vipaji vingi ndani ya mikoa mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa chama hicho kitaifa, Mwarami Miteese, alisema wameamua kufanya hivyo baada ya kugundua kuwa mikoani mchezo huo una hamasa kubwa isipokuwa wanashindwa kufika mbali kutokana na kwamba hakuna wakufunzi wakubwa.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa hivi karibuni kamati ya utendaji inatarajia kukaa kikao kupanga mikakati ambayo itawasaidia watu wa mikoani na kudai, baada ya kupata vyama hivyo watatangaza tarehe rasmi ya kufanya uchaguzi mkuu wa viongozi.

"Tutafanya semina ya muda mfupi kwa watu wa mikoani ili waweze kunufaika na kujua jinsi ya kucheza michezo yetu ya Wushu angalau na wao waweze kunufaika na kujua jinsi michezo hiyo inavyotakiwa kuchezwa," alisema Mwenyekiti huyo.

Aidha, aliwataka Watanzania kuwa kitu kimoja na kuisapoti timu yao ya soka ya Taifa, Taifa Stars ambayo itashuka dimbani kesho kucheza na Burundi katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia Qatar 2022.

# TAIFA STARS MORALI JUU WAKIIFUATA BURUNDI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' imeondoka leo alfajiri kuelekea Burundi tayari kwa mechi yao ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, itakayopigwa kesho nchini humo huku ikiwa na matumaini kibao ya kuibuka na ushindi.

Stars itatua Burundi ikitarajiwa kupokewa na waandishi wa habari za michezo kutoka vyombo mbalimbali pamoja na Kundi la Stars Sapoti, walitangulia mapema kwa ajili ya kwenda kutoa hamasa nchini humo ili kuhakikisha Taifa Stars inashinda ugenini na kisha nyumbani.

**Akizungumza na Nipashe jana asubuhi baada ya kumaliza mazoezi ya mwisho, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma Mgunda, alisema wachezaji wote morali yao ipo juu na lengo lao ni kuhakikisha wanarudi na matokeo mazuri.**

"Leo tumefanya mazoezi ya mwisho, Mungu akipenda kesho alfajiri (leo) tutaondoka kuelekea Burundi ili tuwahi kufanya mazoezi siku moja kabla ya mechi ambapo tutakutana na wachezaji wetu wa kimataifa ambao tayari wapo Burundi wanaendelea kujifua," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema wanaupa umuhimu mkubwa mchezo huo na kuwataka Watanzania kuiombea timu yao ifanye vizuri na kuipeperusha vema bendera ya Taifa letu.

Baada ya mechi hiyo, timu hizo zitarudiana Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, na mshindi wa jumla atasonga mbele kwenye hatua inayofuata.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango (katikati mwenye kitambaa cheusi kichwani) akicheza ngoma na wakazi wa wilaya hiyo juzi katika kilele cha 'Wiki ya Elimu ya Mlipakodi', iliyofanyika kwenye Uwanja wa Sokoine. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Ngao ya Jamii yaifungua mdomo KMKM*

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufanikiwa kufungua msimu kwa kubeba Ngao ya Jamii, Kocha wa KMKM, Ame Msimu Mara, ameweka wazi kuwa katika msimu huu wa Ligi Kuu Zanzibar, uimara wa kikosi chake na namna walivyojipanga unampa matumaini ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe baada ya kikosi chake kukabidhiwa Ngao ya Jamii juzi, kufuatia kuichapa Malindi kwa mikwaju ya penalti 4-3, Mara alisema licha ya kutolewa katika hatua ya awali kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hiyo haimaanishi kikosi hicho ni dhaifu na kwamba kitashindwa kutetea ubingwa wao.

"Kikubwa mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi kila tunapocheza ili kuihamasisha timu, tumejipanga vizuri kutetea ubingwa wetu," alisema.

Katika mechi hiyo ya Ngao ya Jamii iliyopigwa kwenye dimba la Amaan juzi, ikiashiria kufunguliwa kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM ililazimika kushinda kwa changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Malindi ilikuwa ya kwanza kuandika bao kupitia mchezaji Mohamed Ahmed katika dakika ya 12, huku KMKM wakisawazisha dakika tano baadaye kupitia kwa Iliyasa Seleman.

KMKM ambao walikabidhiwa Ngao ya Jamii na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nunga, pia mchezaji wao Adam Ibrahim alitangazwa mchezaji bora wa mechi hiyo na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kumzawadi viatu.

# Michezo

Jumanne Septemba 3, 2019

Nipashe




Fifa yampambanisha tena Van Dijk, Messi na CR7 UKURASA 28

KUNA SWALI?...




Mshambuliaji wa Arsenal, Pierre Emerick-Aubameyang, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la kusawazisha dhidi ya Tottenham wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. Kulia ni mtoa pasi ya bao hilo la pili, Matteo Guendouzi akishangilia na kiungo mwenzake Dani Ceballos. **HABARI UK. 30**

## Simba SC yaiendea likizo Mtibwa

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuanza Ligi Kuu ya Vodacom kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru, ambao aliuita 'finyu', kutokana na kutaka angalau mabao matano, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems amekinoa kikosi chake kwa siku mbili na kisha kukipa mapumziko mafupi kwanza kabla ya kurejea kujiandaa kuivaa Mtibwa Sugar.

Aussems hakufurahishwa na ushindi huo dhidi ya JKT Tanzania, huku pia akieleza wachezaji wake walicheza 'kitoto' kutokana na kutovutiwa na kiwango walichokionyesha Alhamisi iliyopita katika mechi hiyo.

Hata hivyo, amewapa wachezaji wake mapumziko ya siku tatu hadi Alhamisi ndipo watarejea tena kuanza kujiandaa na mechi dhidi ya Mtibwa Sugar itakayopigwa Uwanja wa Uhuru Septemba 17, mwaka huu, kabla ya siku tano baadaye kuialika Lipuli katika dimba hilo.

"Kocha Mkuu Patrick Aussems, amewapa wachezaji mapumziko ya siku tatu. Mazoezi yataendelea Alhamisi Septemba 5, mwaka huu," ilieleza taarifa ya klabu hiyo jana.

Simba ambayo imetolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali na UD Songo ya Msumbiji, mkakati wake sasa ni kushinda mataji yote ya ndani watakayoshiriki na imeahidi kuendelea kuhakikisha inapata ushindi wa kishindo katika kila mechi.

# Yanga yafunguka kutimuliwa Zahera

**Na Shufaa Lyimo**

### ●●● Sababu kuitwa kwenye kikao zaanikwa, huku suala la kutua kwa Mserbia kuinoa nalo likielezwa...

WAKATI taarifa zikizidi kuzagaa huku baadhi ya vyombo vya habari (si Nipashe) vikiripoti kuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera amekalia kuti kavu na kwamba amepewa mechi tatu za kushinda vinginevyo atatimuliwa, uongozi wa Yanga umefunguka A-Z kuhusu sakata hilo.

**Awali chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, wakati tukitafuta ukweli kuhusu sakata hilo, kiliiambia Nipashe kuna taarifa za kuanza kutafutwa kocha Mserbia atakayeinoa klabu hiyo kutokana na mwenendo wa timu kufanya vibaya licha ya Zahera kusimamia suala zima la usajili.**

"Lakini pia uongozi hakufurahishwa na kocha kuukosoa hadharani licha ya baadhi ya mambo kukubaliana nao ikiwa ni pamoja na kupendekeza kambi iwekwe mikoa ya Kaskazini ili wachezaji wazoee hali ya baridi kabla ya kwenda kurudiana na Township Rollers ya Botswana kwenye Ligi ya Mabingwa," kilieleza.

Hata hivyo, Nipashe lilimtafuta Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela, ambapo alikanusha vikali taarifa hizo kwa kueleza kwamba si kweli kuwa kocha Zahera amepewa mechi tatu za kuhakikisha anashinda bali juzi kulikuwa na kikao cha Kamati ya Utendaji na kocha aliitwa ili kutambulishwa rasmi kwa wajumbe na pia kutoa mikakati ya kuelekea mechi dhidi ya Zesco Septemba 14, Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mwakalebela alisema kwa ujumla uongozi una imani na kocha huyo na wana ushirikiano mzuri hivyo habari kwamba amepewa mechi tatu zipuuze vikali.

Mwakalebela alisema habari hizo hazina ukweli wowote na badala yake zinasambazwa na watu wachache ambao hawaitakii mema timu yao.

"Hizo habari za kwamba tunaachana na Mwinyi Zahera si kweli tunamtambua Zahera kuwa mpaka sasa ndiye kocha wetu mkuu hakuna kitu kama hicho hayo ni maneno ya uzushi sasa hivi tunajiandaa na mchezo wetu dhidi ya Zesco United," alisema Mwakalebela.

Aidha, alisema timu yao inatarajiwa kuelekea mkoani Mwanza kesho kwa ajili ya kuweka kambi mpaka Septemba 11, mwaka huu, ikiwa ni pamoja na kucheza mechi za kirafiki ambazo zitakuwa ni mwendelezo wa maandalizi ya mchezo wao huo dhidi ya Zesco.

"Timu yetu inaendelea na mazoezi kama kawaida tukiwa tunajiandaa na safari yetu ya Mwanza ambapo tutakwenda kuweka kambi na kucheza michezo ya kirafiki tunaomba Watanzania wazidi kutupa ushirikiano katika mchezo huo ili tuweze kuipeperusha vema bendera ya Taifa," alisema.

Kwa upande wa leseni za wachezaji wao ambao hawakucheza mchezo wa raundi ya kwanza, alisema bado hazijafika na kwamba wanaendelea kuzifuatilia na kudai endapo zikiwa tayari Watanzania watajulishwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >